# UPANDE WA PILI WA RIWAYA TEULE ZA SHAFI ADAM SHAFI; DHAMIRA ZILIZOFICHAMA

**Gora Akida Haji**

**Tasinifu Iliyowasilishwa Kwa Ajili Ya Shahada Ya Uzamili Katika Fasihi Ya Kiswahili Katika Chuo Kikuu Cha Dodoma**

**Chuo Kikuu Cha Dodoma**

**Oktoba, 2015**

# ITHIBATI

Aliyesaini hapo chini anathibitisha kuwa amesoma tasnifu hii inayoitwa "***Upande wa Pili wa Riwaya Teule za Shafi Adam Shafi: Dhamira Zilizofichama***", na anapendekeza kuwa inafaa kukubaliwa na Chuo Kikuu cha Dodoma kwa Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

**………………………………**

**Prof. Joshua S. Madumulla**

**(Msimamizi)**

**Tarehe………………………………..**

## IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi, Gora Akida Haji, ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu asili na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine ndani na nje ya nchi, kwa ajili ya kutunikiwa shahada inayofanana na hii au nyingine yoyote.

**Saini: ………………………………**

Hairuhusiwi kuzalisha, kunakili, wala kusambaza sehemu yoyote ile bila ya kibali cha maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu Cha Dodoma.

## TABARUKU

Kwa baba yangu, Akida Haji Kombo:

Tofauti ya kifaranga kinapototolewa, na jogoo ambaye angestahili kuitwa baba wa kifaranga hicho kuchinjwa, na baba wa mtoto ambaye ni binadamu kupoteza maisha yake kwa njia kama hiyo, ni dhima, sababu na hadhi ya viumbe hivi. Jogoo katu hadhulumiwi kwa hilo; ni stahiki yake. Kwa sababu ya majaliwa, ninastahiki kushukuru na kuzikiri shida nilizopita za uyatima. Si kusamehe na sitosahau katu tendo hili. Nakuombea baba yangu Mwenyezi Mungu akusamehe dhambi zako kutokana na ukubwa wa dhuluma uliyofanyiwa.

Kwa mama yangu, Hadia Gora Shamte:

Uliyepata shida tokea mbegu ya uzazi ilipotunga katika fuko lako la uzazi; ukaendelea kusononeka hadi nilipojimudu. Ni wewe uliyekosa raha ya kula, kulala na hata kutembea. Uliniomba nisilie kwa shida yoyote ili nisije kukuliza na wewe, huku ukiniahidi kutunza machozi yangu, ukifa nikulilie. Mungu akulipe kila la kheri na akuzidishie umri ulio na Baraka.

Kwa babu yangu,  Kalamu Juma Gora:

Uliyebeba ubaba kamili katika malezi yangu ndani ya moyo wako; ukabeba pia uaminifu, huruma na hidaya kwangu ndani ya kifua chako; mapenzi ya dhati. Huruma na thamani ya kweli kwa mayatima huweza kuziba pengo la ukiwa kwa mayatima hao. Katu hukushuhudia matunda ya mti huu hata kama, uliyaona maua yake. Allah atakulipa kilicho bora zaidi.

Kwa mke na watoto wangu:

Sikuwafanyia haki pale nilipokuacheni katika mazingira magumu ya kimaisha, fikira zenu zikiwazonga kwa kukosa upendo wa baba, hata kama ni wa siku moja.

Nyote watajwa hapo juu, ninakupendeni kwa mapenzi ya dhati sana, na ndiyo maana ninakuombeni kuipokea kazi hii kama ni TABARUKU kwenu.

## SHUKRANI

Kwanza ni wajibu wangu kumshukuru Allah (S.W) Muumba mbingu, ardhi na vyote vilivyomo ndani yake. Yeye ndiye aliyeniumba na kunipa mfumo wa maisha, kunijaaliya uzima, afya pamoja na kunipa maarifa ya kuweza kukamilisha utafiti huu.

Pili, natoa shukrani za dhati kwa uongozi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kupitia msimamizi wangu, Prof. J. S. Madumulla, ambaye alijitolea kuniongoza na kunisimamia kwa kunipa mawazo, fikra, pamoja na mwongozo wake na ndio ulionisaidia na kunipa msukumo wa kufanya kazi hii hadi kufikia kiwango hiki nilichofikia.

Tatu, napenda kumshukuru mke wangu mpenzi, Bi Rehema Haji Foum, kwa kunivumilia, kunitia moyo na kuitunza familia yetu vizuri katika kipindi kigumu cha masomo mpaka kukamilisha utafiti huu. Pamoja na wanangu, Umm-Khadija, na Sumaiya kwa kuvumilia na kukosa rubaa ya baba yao kwa kipindi chote cha masomo.

Pia, nawashukuru wale wote walionisaidia na kunitia moyo kwa hali moja na nyingine, wakiwemo wenzangu wa karibu ambao tulishauriana kila hatua za tafiti zetu, wakiwemo Simba Haji Gora, Ussi Juma Ussi, Haji Majid Haji, Abdi Ramadhani Mberwa, na wengineo. Wengine walionisaidia ni Fatuma Haji Foum, Asia Kheir Hussein, Subira Shaaban Amour, Mwl. Mkali, Mwl. Issa Hassan Haji na Saada Soud Salum. Shukrani zaidi ziende kwa wale waliochaguliwa kuwa sampuli ya utafiti huu na wakakubali kujaza dodoso bila pingamizi, wakajibu maswali ya usaili bila ya shida na wala vikwanzo vyovyote. Sina cha kuwalipa, ila ni kuwaombea dua kwa Mungu, awalipe kheri duniani, na kesho akhera. Na bila ya kumsahau Mwl. Bi Sayfa Abdalla Mohammed aliyeweza kupitia mswada wa kazi hii yote na kuuhariri kabla ya kupelekwa kwa msimamizi.

Mwisho, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitatoa shukurani kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kunipa kibali cha ruhusa ya kufanya utafiti katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar, Vyuo Vikuu vyake pamoja Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar. Ninawashukuru wale wote walionisaidia kazi hii kwa hali moja au

nyingine bila hata ya kuwataja; na hii si dalili ya kuwadharau hata kidogo kwa mchango wao muhimu katika kazi hii. Msingi wa shukrani hizi ni kuwaombea wote hawa kwa Allah ili awafungulie milango ya kheri na baraka duniani, na kesho akhera.

## YALIYOMO


**ITHIBATI** .......... **i**
**IKIRARI NA HAKIMILIKI** .......... **ii**
**TABARUKU** .......... **iii**
**SHUKRANI** .......... **iv**
**YALIYOMO** .......... **v**
**ORODHA YA VIFUPISHO** .......... **viii**
**IKISIRI** .......... **ix**
**SURA YA KWANZA** .......... **1**
**UTANGULIZI** .......... **1**
1.1 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu Zilizotumika katika Utafiti Huu .......... 1
1.1.1 Kufichama .......... 1
1.1.2 Mtindo .......... 1
1.1.3 Maana/Dhamira .......... 2
1.1.4 Maana iliyofichama .......... 2
1.1.5 Dhamira iliyofichama .......... 2
1.1.6 Upande wa Pili wa Kazi ya Fasihi .......... 3
1.1.7 Matumizi ya Lugha .......... 3
1.2 Historia Fupi ya Shafi Adam Shafi .......... 3
1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti .......... 5
1.4 Tamko la Tatizo la Utafiti .......... 8
1.5 Malengo ya Utafiti .......... 9
1.5.1 Lengo la Jumla .......... 9
1.5.2 Malengo Mahsusi .......... 9
1.6 Maswali ya Utafiti .......... 9
1.7 Manufaa ya Utafiti .......... 10
1.8 Muhtasari wa Sura ya Kwanza .......... 10
**SURA YA PILI** .......... **11**
**MAPITIO YA MAANDIKO** .......... **11**
2.1 Utangulizi .......... 11

2.2 Maandiko Kuhusu Maana au Dhamira Zilizofichama katika Kazi za Fasihi kwa Jumla ....................................................................................................11
2.3 Maandiko kuhusu Kazi za Shafi Adam Shafi ................................................18
2.4 Mapengo Yanayojitokeza Kutokana na Mapitio ya Maandiko ......................19
2.5 Muhutasari wa Sura ya Pili ..............................................................................20
**SURA YA TATU ..........................................................................................21**
**MBINU ZA UTAFITI ....................................................................................21**
3.1 Utangulizi ..........................................................................................................21
3.2 Mpango wa Utafiti ............................................................................................21
3.3 Eneo la Utafiti ....................................................................................................21
3.4 Walengwa wa Utafiti ........................................................................................22
3.4.1 Jamii ya Watafitiwa ..........................................................................................22
3.4.2 Sampuli ya Watafitiwa ......................................................................................22
3.5 Ukusanyaji wa Data ..........................................................................................23
3.5.1 Njia na Zana za Kukusanyia Data ....................................................................23
3.5.2 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data ....................................................................24
3.5.3 Udhibiti, Uchambuzi na Uunganishaji wa Data ..............................................25
3.6 Nadharia Zilizotumika ......................................................................................25
3.6.1 Maana ya Nadharia hizi ....................................................................................25
3.7 Mipaka ya Utafiti ..............................................................................................28
3.8 Mapungufu Yaliyojitokeza Katika Utafiti na Utatuzi Wake ..........................28
3.8.1 Watafitiwa Kutozifahamu kwa Kina Kazi za Mwandishi Huyu ....................28
3.8.2 Madodoso Kutorudi kwa Wakati na kwa Ukamilifu ......................................29
3.8.3 Uchache wa Rejea na Maandiko Juu ya Kazi za Shafi Adam Shafi ..............29
3.9 Muhtasari wa Sura ya Tatu ..............................................................................29
**SURA YA NNE ..............................................................................................30**
**UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI ......................30**
4.1 Utangulizi ..........................................................................................................30
4.2 Upande wa Pili wa Riwaya Teule ....................................................................30
4.2.1 Muhutasari wa Vitabu Teule ............................................................................30
4.2.1.1 Kuli ..................................................................................................................30
4.2.1.2 Vuta n'Kuvute ..................................................................................................34
4.2.1.3 Haini ................................................................................................................40

4.2.2.1 Dhana ya Maana na Dhamira ....................................................................45
4.2.2.2 Dhana ya Maana na Dhamira Zilizofichama ...............................................46
4.2.2.3 Vipengele Vinavyojenga Dhamira Zilizofichama Katika Kazi za Fasihi kwa Jumla ..........................................................................................47
4.2.2.4 Njia za Kuchambua Dhamira Zilizofichama katika Kazi za Fasihi ...............54
4.2.3 Dhamira Zilizofichama katika Kazi Teule ...................................................56
4.2.3.1 Dhamira Zilizofichama Kupitia Methali .....................................................56
4.2.3.2 Dhamira Zilizofichama Kupitia Nyimbo......................................................64
4.2.3.3 Dhamira Zilizofichama kupitia Vifungu vya Maneno yenye Maana ya Kimafumbo ..........................................................................................71
4.2.3.4 Dhamira Zilizofichama kupitia Jina la Kitabu ..............................................79
4.2.3.5 Dhamira Zilizofichama kupitia Majina ya Wahusika....................................83
4.3 Miktadha Iliyomsukuma Mwandishi Kutumia Mtindo Huu ..........................87
4.3.1 Kitaaluma ..........................................................................................89
4.3.2 Kijamii..............................................................................................92
4.3.3 Kisiasa ..............................................................................................94
4.4 Athari za Mitindo yake kwa Wasomaji wa Kazi Hizi ...................................96
4.4.1 Athari Chanya.....................................................................................96
4.4.2 Athari Hasi.........................................................................................98
4.5 Muhtasari wa Sura ya Nne.......................................................................100
**SURA YA TANO.............................................................................................102**
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO..........................................102**
5.1 Utangulizi .........................................................................................102
5.2 Muhutasari wa Tasinifu ..........................................................................102
5.3 Utoshelevu wa Nadharia.........................................................................104
5.4 Mchango wa Tasnifu hii .........................................................................105
5.5 Maoni ya Utafiti kwa Jumla ....................................................................107
5.6 Mapendekezo juu ya Tafiti Zijazo............................................................108
**MAREJEO.......................................................................................................110**
**VIAMBATANISHO...........................................................................................112**
A: Picha za Utafiti ...................................................................................112
B: Zana Zilizotumika Kukusanyia Data .........................................................113
B. 1 MUONGOZO WA USAILI KWA WATAALAM WA FASIHI ...............113

B.2 MUONGOZO WA HOJAJI KWA WANAFUNZI WA FASIHI WA SEKONDARI NA VYUO ........ 114
C: MAELEZO YA MAFUPI YA MTAFITI NA UTAFITI: ........ 117

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| SUZA | State University of Zanzibar |
| SU | Summeit University (let, University College of Education of Zanzibar) |
| ZU | Zanzibar University |
| UWAVITA | Umoja wa Watunga Vitabu Tanzania |
| BAMVITA | Baraza la Maendeleo ya Vitabu Tanzania |
| C C M | Chama Cha Mapinduzi |
| n.k | Na kadhalika |
| ASP | Afro-Shiraz Party |
| h.t. | haina tarehe |
| w.h.j. | wametajwa hapo juu |

## IKISIRI

Tasnifu hii ililenga kuchunguza "Upande wa Pili wa Riwaya teule za Shafi Adam Shafi" kwa kuangalia dhamira zilizofichama. Utafiti uliofaywa uliongozwa na malengo matatu ambayo ni: Kuchunguza upande wa pili wa riwaya teule za Shafi A. Shafi kwa kuangalia dhamira zilizofichama katika kazi hizo; Kuchunguza na kubainisha miktadha mbalimbali iliyomsukuma Shafi A. Shafi kutumia mtindo huo katika kazi zake hizo; na Kubainisha athari za mtindo uliotumika katika kazi za Shafi A. Shafi kwa wasomaji wake.

Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data ni udurusu wa maktaba, usaili na mahojiano ili kupata taarifa juu ya dhamira zilizofichama katika riwaya. Nadharia zilizotumika katika utafiti huu wakati wa ukusanyaji na uchambuzi wa data ni nadharia ya U-muundo na Umarx.

Matokeo ya jumla ya utafiti huu yalionesha dhamira zilizofichama katika kazi teule kama zifuatazo: harakati za kupigania uhuru kuwa ngumu kutokana na vibaraka vya kikoloni kufaidika na utawala huo, ushiriki wa wasomi katika harakati za kupigania uhuru huo, kusalitiwa kwa wasomi baada ya kupatikana kwa uhuru huo pamoja na suala la ukweli kuhusu harakati za mapinduzi ya Zanzibar.

Kutokana na matokeo haya, utafiti huu unashauri mambo yafuatayo: kwanza ni kuzisoma kazi hizi kwa makini ili kuweza kubaini kwa kina juu ya mambo yaliyofichama katika kazi hizi. Pili kazi hizi huweza kutumika kama rejea katika kuijua historia ya Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

Sura hii imetoa utangulizi mzima wa utafiti huu, imeeleza historia kwa ufupi ya mwandishi wa kazi teule ambaye ni Shafi A. Shafi. Kutoa ufafanuzi juu ya istilahi zilizotumika katika utafiti huu, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali yanayoongoza utafiti huu pamoja na manufaa ya utafiti kwa mtafiti na jamii kwa jumla.

## 1.1 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu Zilizotumika katika Utafiti Huu

### 1.1.1 Kufichama

Ni neno linalotowa mnyambuliko wa neno mfichamo, Wamitila (2003) anaeleza kuwa mfichamo ni dhana inayotumiwa kuelezea mtindo wa uandishi au usemaji ambapo lugha inayotumiwa haisemi mambo waziwazi. Kitula na Ahmed (2008) katika kufafanua neno fiche wanasema kuwa maana ya kifilosofi ya methali huwa na maana fiche yenye undani, sio maana ya jumla ya maneno yake.

Hivyo, tasnifu hii inaeleza dhana ya kufichama kuwa ni kutoa maana ya lugha au mtindo katika mwelekeo zaidi ya mmoja kimaana. Yaani, maana za mitindo au lugha ambazo wahakiki wengi hawazitilii maanani; bali kwa mujibu wa utafiti huu, zina maana iliyozama zaidi katika kuibua dhamira zilizofichama.

### 1.1.2 Mtindo

Ni upekee wa mwandishi katika kuisana kazi yake na kumtofautisha na mwandishi mwingine. Uchanganuzi wa mtindo unahusisha kuangalia uteuzi wa msamiati,

tamathali za usemi, mbinu za kibalagha na mbinu nyingine (Wamitila, 2003). Kwa kuongezea, Senkoro (2011) anaeleza kuwa mtindo ni ile namna ambayo mwanasanaa huipa kazi yake ya kifasihi sura ya kifani na kimaudhui kwa njia ambayo msanii mwingine asingeweza kufanya hivyo, hata kama jambo linaloongelewa na wasanii hawa wawili ni lile lile moja. Maelezo haya yana maana kuwa mtindo huweza kujitokeza katika pande zote mbili – maudhui na fani. Kutokana na ufafanuzi huo tunaweza kuchambua mtindo kwa kuzingatia vipengele vya tamathali za usemi, methali, taswira na mbinu nyingine zinazoweza kutoa maana za ndani (iliyofichama).

### 1.1.3 Maana/Dhamira

Maana na dhamira ni maneno yenye maana moja kifasihi kwa kumaanisha wazo kuu la mwandishi alilolikusudia kuwasilisha kwa hadhira yake (Wamitila, 2003). Senkoro (2011) anaeleza kuwa katika dhamira kuu tunaweza kugundua dhamira ndogo ndogo zinazoambatana na dhamira kuu. Katika tasnifu hii maneno haya, maana na dhamira, yametumika sambamba na kuzingatia dhamira ndogo ndogo zinazopatikana katika kazi teule.

### 1.1.4 Maana iliyofichama

Kifasihi, maana ni wazo au mawazo yanayopatikana katika kazi ya kifasihi. Katika tasnifu hii inatafsiri maana iliyofichama kuwa ni mawazo ya ndani yanayopatikana kwa kuchambua vipengele vya mtindo na lugha katika kazi teule za kifasihi.

### 1.1.5 Dhamira iliyofichama

Kwanza, dhamira ni wazo kuu la mwandishi analohusisha na lengo lake la kuandika kazi ya kifasihi. Katika tasnifu hii, dhamira iliyofichama inatafsirika kuwa ni wazo la

mwandishi lililofumbwa kifasihi na kupatikana kwa kuchambuliwa kiundani kwa vipengele vya mtindo na lugha katika kazi teule.

### 1.1.6 Upande wa Pili wa Kazi ya Fasihi

Ni maana ya kazi ya kifasihi inayopatikana baada ya kuchambua vipengele vya mtindo na lugha vilivyojengwa kwa mtindo wa kitamathali na kutoa maana ya ndani katika vipengele hivyo.

Katika utafiti huu, Upande wa pili wa kazi ya fasihi ulipatikana baada ya kuchambua na kutoa dhamira zilizofichama katika kazi teule za Shafi Adam Shafi.

### 1.1.7 Matumizi ya Lugha

Ni namna ya kutumia lugha kisanii katika kazi ya kifasihi hasa kwa kuzingatia utumiaji wa tamathali za semi, taswira, ishara, methali, mafumbo, misemo, simo na uteuzi mzuri wa maneno. Vipengele ambavyo huweza kutoa maana sahili na maana ya ndani (maana batini). Madumulla (2009) anaeleza kuwa jambo kubwa katika mtindo wa hadithi ni jinsi msanii anavyoweza kutumia lugha. Kwa maana kuwa lugha au matumizi ya lugha ni sehemu ya mtindo katika kazi ya fasihi.

## 1.2 Historia Fupi ya Shafi Adam Shafi

Shafi Adam Shafi ambaye jina lake halisi ni Adam Shafi Adam, alizaliwa mwaka 1940 Mwembe Kisonge, Mjini Zanzibar. Baba yake Mzee Shafi Adam Hila alikuwa ni mfanyabiashara katika maeneo ya Kwahajitumbo, mjini Zanzibar. Alikuwa ni Mzanzibar mwenye asili ya Comoro. Mama yake Bi Riziki Mbaye alikuwa ni mama wa nyumbani aliyejishughulisha na biashara ndogo ndogo.

Adam Shafi alisoma skuli ya msingi ya French Comorian School (kwa sasa skuli ya Hamamni) toka darasa la kwanza hadi la sita. Baadaye alijiunga skuli ya Gulioni Primary School (sasa ni sehemu iliyojengwa Benki Kuu ya Tanzania (BOT)) na kusoma darasa la saba hadi la nane. Baada ya kufaulu mwaka 1957 alipata nafasi ya kujiunga na Chuo cha Seyyid Khalifa Teacher Training College (sasa ni Nkrumah kampusi ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar – SUZA). Katika chuo hiki walikuwa wakisoma miaka minne, kwa ajili ya kusoma masomo ya sekondari pamoja na mafunzo ya ualimu wa msingi, kwa kiwango cha cheti. Katika chuo hiki Adam Shafi alipata hamasa ya kwenda kusoma nchi za nje; pia, kuandika kazi za kifasihi pamoja na hamu ya kujishughulisha na harakati za kisiasa. Hivyo, mwaka wa tatu wa chuo, Adam Shafi aliamua kukimbia chuoni kwa lengo la kwenda Uingereza kwenda kusoma, kwa njia ya magendo. Kuanzia hapo ndipo rasmi alipoingia katika changamoto za kimaisha na hatua kwa hatua alianza rasmi kuingia katika harakati za kisiasa.

Pamoja na vikwazo mbalimbali, Adam Shafi alifanikiwa kusoma Diploma ya juu katika fani ya siasa ya uchumi katika chuo cha Fritz Heckert mwaka 1963 huko Ujerumani. Pia alipata mafunzo ya uandishi wa habari katika vyuo tofauti kama Prague, nchini Czechoslavakia (sasa jamhuri ya Czech) mwaka 1964 hadi mwaka 1965, nchini Sweden mwaka 1982 na nchini Marekani mwaka 1983. Adam Shafi alibahatika kushiriki kikamilifu katika harakati za siasa ya Zanzibar kwa kushiriki katika vyama vya wafanyakazi na hata vyama vya kisiasa kabla ya mapinduzi ya Zanzibar ya 1964.

Harakati za uandishi wa vitabu alizianza rasmi akiwa katika Chuo cha Seyyid Khalifa na kufanikiwa kutoa kitabu chake cha kwanza mwaka 1978 cha *Kasri ya Mwinyi*

*Fuad*. Kazi nyingine alizotunga ni *Kuli* (1979), *Vuta N'kuvute* (1999), *Haini* (2003) na *Mbali na Nyumbani* (2013). Kwa sasa, anaendelea na mswada wa kitabu kinachotarajiwa kupewa jina la "Mtoto wa Mama."

Adam Shafi, pamoja na kushiriki katika harakati za ukombozi wa Zanzibar, baada ya kuuwawa rais wa kwanza wa Zanzibar, hayati Abeid Amani Karume, alituhumiwa kushiriki katika njama za mauaji. Hivyo, alifungwa miaka mitatu; baada ya kufunguliwa alifukuzwa kazi aliyokuwa akifanya katika kampuni ya Publishing Center mwaka 1974. Baada ya matukio hayo aliamua kuhamia Dar es Salaam, ambako mpaka sasa yuko huko kimaisha.

Adam Shafi katika kuendeleza tasnia ya fasihi, ukitoa utungaji wa vitabu, amewahi kuwa mwenyekiti wa Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania (UWAVITA) kuanzia 1998 hadi 2002. Pia, amewahi kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Maendeleo ya Vitabu Tanzania (BAMVITA) mwaka 2002. Adam Shafi ni miongoni mwa watu wachache waliowahi kuwa wanasiasa mashuhuri pia, kuwa wachangiaji wakubwa wa maendeleo ya fasihi Tanzania.

## 1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Upande wa pili wa kitu chochote unakuwa ni upande uliofichama au usioonekana kwa wakati ule au kwa mara moja. Dhana ya hii katika kazi ya fasihi ni mpya kiistilahi, bali ni ya kawaida sana kidhana. Upande wa pili katika fasihi ni mwelekeo wa pili wa kazi ya fasihi, ikiwa mwelekeo wa kwanza ni ule mwelekeo anaotoa msomaji kwa mara ya kwanza baada ya kuisoma kazi husika. Na mwelekeo wa pili au Upande wa pili ni ule mwelekeo ambao huutoa msomaji au mhakiki baada ya kusoma kazi kwa kina na kuzingatia vipengele vyote vya fani na maudhui kwa kuangalia dhamira zilizofichima.

Katika utafiti uliofanyika dhana ya Upande wa Pili iliangalia dhamira zilizofichama katika kazi za fasihi. Kwa kawaida, fasihi haitumii lugha ya moja kwa moja katika kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa. Hali hii hutoa maana inayofahamika kwa haraka. Pia, huweza kutoa maana isiyofahamika kwa haraka (iliyofichama), hadi maana hiyo itafsiriwe au ilinganishwe na dhana au maneno yaliyotumika katika kazi hiyo. Maana katika kazi ya fasihi huelezea wazo linalopatikana katika kazi hiyo. Wazo hilo huweza kuwa dhahiri au lenye kujificha kutegemea na umahiri wa mwandishi katika kuisana kazi yake kimtindo, ujenzi wa wahusika na matumizi ya lugha.

Dhamira zilizofichama hupatikana kwa kuchambua mtindo uliotumika, ujenzi wa wahusika na kuchambua vipengele vya lugha kama methali, tamathali za semi, mafumbo, taswira, simo na vinginevyo. Vipengele hivi kwa pamoja huitwa lugha ya kitamathali. Kazi yenye sifa hizi huweza kutoa maana ya moja kwa moja na maana au dhamira zilizofichama. Dhamira zilizofichama zinatoa mwelekeo mwengine wa kazi hiyo ambao ndio tunaouita upande wa pili wa kazi ya fasihi.

Upande wa pili wa kazi ya fasihi pia unajengwa na dhamira zilizofichama. Dhamira ni dhana inayoelezea wazo la mwandishi linalotokana na lengo lake juu ya kuiandika kazi hiyo. Maana na dhamira ni dhana zenye uhusiano na kufanana sana katika uga wa kifasihi. Dhamira katika fasihi zinaweza kupatikana kwa kuangalia uhusiano wa wahusika katika kazi pamoja na matumizi ya lugha kama ilivyo katika maana. Pia kudhihirika au kifichama kwa dhamira kunategemea usanii katika ujenzi wa wahusika matumizi ya lugha na mbinu nyingine za kisanii.

Kwa jumla, dhana ya upande wa pili katika fasihi iliangalia dhamira zilizofichama katika kazi za fasihi. Dhana hii iliweza kugunduliwa kwa kupitia uchambuzi wa matumizi ya methali, taswira, semi, ujenzi wa wahusika, majazi, tamathali za semi na

mbinu nyingine za kisanii. Kila msanii hutumia mtindo maalum ambao huweza kumtofautisha na kazi za msanii mwingine.

Dhana ya mtindo ni pana ambayo huweza kubeba uumbaji wa wahusika, matumizi ya lugha, utumiaji wa mandhari na mbinu nyingine za kifani (kama vichekesho, ucheshi na matumizi ya nafsi). Vipengele hivi navyo vinasaidia kutoa maana na dhamira zilizofichama na kuifanya kazi ya kifasihi kuwa na upande wa pili. Upande wa kwanza wa kazi ya fasihi ni ule unaoonekana kwa jicho la kwanza la usomaji, na kwa kutoa maana ya maneno kwa maana ya kikamusi au ya kikawaida. Na upande wa pili ni ile maana inayopatikana kwa usomaji wa jicho la ndani au la pili na kutafsiri methali, taswira, jazanda, tamathali za semi, wahusika na uhusika wao, lugha za mafumbo na vipengele vingine kama hivi, ili kuibua dhamira zilizofichama. Utafiti huu uliifanyia kazi dhana hii kupitia utanzu wa riwaya katika fasihi andishi ya Kiswahili.

Riwaya ni kisa changamano ambacho kina mawanda mapana zaidi katika fani na maudhui yake (Senkoro, 2011). Sifa hii ndiyo inayoitofautisha riwaya na hadithi fupi, Ngano na insha ambazo zote hizi ni nathari katika fasihi ya Kiswahili. Shivji (2000) anaongezea sifa za riwaya kuwa, ndiyo inayoweka wazi siri za jamii, kuanika aibu za waheshimiwa, na kusema kwa uwazi ule ukweli usioweza kusemekana. Haya yote yanafanywa na mwandishi stadi wa fasihi.

Utafiti huu uliziangalia riwaya teule za Shafi A. Shafi. Sababu ya kuchagua mwandishi huyu ni ustadi wake katika kazi za fasihi na pia, ni mtunzi maarufu na mzoefu katika kuisarifu lugha ya Kiswahili. Kazi zake nyingi ameandika moja kwa moja kutokana na tajiriba na matukio yaliyotokezea katika jamii yake. Aidha, wahakiki wengi wanamuangalia na kumhakiki kwa upande mmoja tu, upande wa kwanza (kwa jicho la kwanza). Mwandishi huyu amekuwa ni mhakiki mzuri wa kuihakiki jamii yake na

kuiandikia. Suali ni kwamba, je, jamii inapata maana au dhamira halisi na zile zilizofichama za kazi hizi?

Shafi A. Shafi ameandika kazi nyingi hasa za riwaya, zikiwemo; *Kasri ya Mwinyi Fuadi*, *Vuta n'kuvute, Kuli, Haini*, na *Mbali na Nyumbani*. Utafiti huu ulishughulika na *Vuta n'kuvute, Haini* na *Kuli*. Hii ni kwa sababu; kwanza, zimesawiri matukio ya jamii kwa upana zaidi; pia, zimekuwa maarufu na kufanya zihitajike sana na jamii, na bado hazijapata uhakiki wa kina zaidi.

## 1.4 Tamko la Tatizo la Utafiti

Wahakiki mbalimbali wamechambua na kuhakiki kazi za Shafi A. Shafi wakiwemo Senkoro, (2011), Masebo na Nyangwine (2010), na Khatibu (1983). Tahakiki zao zimeelezea kuwa Shafi A. Shafi ametumia vipengele mbali mbali vya mtindo na lugha kama methali, misemo, simo, majazi na vinginevyo. Pia kuna madai kuwa amezungumzia zaidi dhamira ya ukombozi na ametumia lugha nyepesi na iliyowazi. Hali hii inatokana na jamii kuwa na tatizo la kuiangalia fasihi kwa upande mmoja tu, na kuacha kuzichambua kazi hizi kifasihi zaidi.

Jamii ya wanafasihi imekuwa na juhudi kubwa ya kuchambua kazi za kifasihi kwa kuzingatia dhamira zilizofichama na zile zilizowazi. Uchambuzi huu hufanywa hasa kwa kazi zilizojengwa kwa mfumo wa kitamathali kama zile za Shaaban Robert; *Kusadikika* na *Kufikirika,* kama anavyochambua Senkoro, (2011). Tatizo linalojitokeza ni wahakiki na wanafasihi kwa jumla la kutochambua mafumbo yaliyofichama katika dhamira nyingine katika kazi ambazo hazikutumia lugha ya kitamathali. Tatizo hili limejitokeza kwa Senkoro, (2011), Masebo na Nyangwine (2010), na Khatibu (1983) katika kuhakiki kazi za Shafi Adam Shafi. Ili kuondoa matatizo haya, utafiti huu

umeangalia Upande wa Pili wa kazi za Shafi A. Shafi kwa kuchambua kwa kina maana na dhamira zilizofichima katika kazi zake za kifasihi. Utafiti huu ulizamia zaidi katika vipengele vya mtindo na lugha (matumizi ya tamathali za semi, methali, mafumbo, majina ya wahusika na majina ya kazi zenyewe) yaliyotumika katika kazi hizi. Utafiti ulijikita na kuzamia katika riwaya za Shafi A. Shafi ambazo ni *Vuta n'kuvute*, *Haini* na *Kuli*.

## 1.5 Malengo ya Utafiti

### 1.5.1 Lengo la Jumla

Kuchunguza dhamira zilizofichama katika kazi za kifasihi

### 1.5.2 Malengo Mahsusi

a) Kuchunguza Upande wa Pili wa riwaya teule za Shafi A. Shafi kwa kuangalia dhamira zilizofichama katika kazi hizo;

b) Kuchunguza na kubainisha miktadha mbalimbali iliyomsukuma Shafi A. Shafi kutumia mtindo huo aliotumia katika kazi zake, na

c) Kubainisha athari za mtindo uliotumika katika kazi za Shafi A. Shafi kwa wasomaji wake.

## 1.6 Maswali ya Utafiti

Maswali yaliyoongoza utafiti huu ni:-

a) Ni mambo gani yanayojenga Upande wa Pili wa kazi ya fasihi na kutoa dhamira zilizofichama katika kazi za Shafi A. Shafi.

b) Je, ni sababu zipi zilizomsukuma Shafi A. Shafi kutumia mtindo na lugha aliyotumia?

c) Je, vipengele vya mtindo na lugha ambavyo vimetumika katika kazi za kifasihi za Shafi A. Shafi vina athari gani kwa wasomaji wake?

## 1.7 Manufaa ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kutoa manufaa yafuatayo:-

a) Kuelezea dhana ya Upande wa Pili katika fasihi na mambo yanayojenga dhana hii katika fasihi ya Kiswahili;

b) Kusaidia kuzihakiki kwa kina/jicho la pili kazi teule za Shafi A. Shafi ikiwa ni miongoni mwa kazi maarufu za fasihi ya Kiswahili;

c) Kusaidia wanafasihi kuvijua vipengele vinavyojenga Upande wa Pili wa kazi za fasihi, ili kuvizingatia wakati wa kutunga kazi zao na kuzifanya kuwa zenye utajiri wa kimaudhui, na;

d) Matokeo ya utafiti huu ni fursa kwa mtafiti kutunukiwa Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili.

## 1.8 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura hii imeeleza utangulizi mzima wa utafiti huu. Vipengele vilivyoelezwa ni historia fupi ya mwandishi wa kazi teule ambaye ni Shafi A. Shafi, ufafanuzi juu ya istilahi zilizotumika katika utafiti huu, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, kutoa malengo ya utafiti, masuali yanayoongoza utafiti huu pamoja na manufaa juu ya utafiti huu. Utangulizi huu umetoa fursa ya kuangalia mapitio ya kazi mbalimbali katika sura inayofuata.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imeelezea kuhusu maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada hii. Maandiko haya yamegawanyika katika makundi mawili makubwa: La kwanza limejumuisha maandiko yanayozungumzia maana au dhamira zilizofichama katika kazi za fasihi kwa ujumla. Kundi la pili limejumuisha maandiko yanayozungumzia kazi za kifasihi za Shafi A. Shafi. Maandiko haya yametoa mwangaza juu ya dhana nzima ya dhamira zilizofichama katika kazi za fasihi pamoja na kuona namna watafiti walivyoziangalia kazi za Shafi A. Shafi. Hali hii imesaidia kutoa pengo la utafiti na kupata fursa ya kufanyika utafiti huu.

## 2.2 Maandiko Kuhusu Maana au Dhamira Zilizofichama katika Kazi za Fasihi kwa Jumla

Wamitila (2003) anaeleza kwa kina juu ya dhana ya maana na kufafanua kama ni kitu funge kilicho kwenye kazi ya kifasihi ambacho huweza kupatikana na mhakiki au msomaji. Pia kaigawa maana katika aina mbalimbali; aina kubwa ni maana halisi na maana batini/iliyofichika. Maana batini kailinganisha na maana ya kitamathali. Hii ndio maana iliyofichika na huchambuliwa kwa kuangalia tamathali za semi na mbinu nyingine zilizotumiwa. Hata hivyo, mwandishi amezifafanua maana kijumla zaidi kama kawaida ya kamusi.

Songoyi na Masele (2013) wanafafanua kuwa maana ipo katika viwango viwili kama wanavyoeleza:-

> *Another important point to remember is that most of the poems operate in two level of meaning. This is the result of the use of poetic devices and the figures of speech in particular which always bring different meaning to the readers due to the level of understanding and experience. And through the use of figures of speech such as allusion, similes, metaphors and others the readers can come up with varieties of messages. But, note that every interpretation might be possible depending on the explanation and convincing points or concrete examples from a poem.* (Songeyi and Masele, 2013:91)
>
> Jambo jingine muhimu ni kuwa mashairi mengi yanatoa maana katika viwango viwili. Haya ni matokeo ya matumizi ya vijenzi vya ushairi na tamathali za semi mahsusi, ambazo kawaida hutoa maana tofauti kwa wasomaji kutokana na viwango vya ufahamu na uzoefu. Na kutokana na tamathali za semi kama vile mdokezo, sitiari, tashibiha na nyinginezo, wasomaji wanaweza kutoa ujumbe tofauti tofauti. Lakini, kumbuka kwamba kila tafsiri inawezekana kutegemeana na maelezo na dondoo zenye kushawishi au mifano makini kutoka katika shairi. (Tafsiri yetu)

Maelezo haya, yanatusaidia kuthibitisha kuwa kuna maana sahili na maana fiche. Kwa kuwa ushairi nao ni utanzu wa fasihi, pia matumizi haya ya sitiari, tashibiha, taswira na mbinu nyingine za kisanaa kama hizi huweza kutumika katika tanzu nyingine kwa muktadha na maana zile zile. Mulokozi na Kahigi (1979) wanasisitiza maelezo haya kwa kusema, tamathali ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilisha maana dhahiri za maneno ili kuleta maana maalum iliyofichikana (ya kishairi). Burton (1962)

anaeleza kuwa katika kupata maana ya ndani (iliyofichama) muhimu ni kuchambua lugha na mtindo uliotumika kwa kuangalia taswira na tamathali za semi pamoja na kuangalia vichocheo vilivyomsababisha mwandishi kutunga kazi yake ya kifasihi; na si kuangalia maudhui moja kwa moja ya kazi hiyo. Mwandishi anaamini kuwa kila shairi lina maana mbili, ile iliyo wazi na ile iliyojificha. Maelezo haya anayatilia nguvu kwa kudai kuwa ushairi ndio utungo pekee unaoshehenezwa na tamathali za semi, taswira, ishara, jazanda na mbinu nyingine za kitamathali kuliko tanzu nyingine. Kutokana na maelezo haya, mwandishi anaamini kuwa maana au dhamira zilizofichama zinapatikana zaidi katika mashairi kuliko katika tamthiliya na nathari kwa jumla.

Nguro (2005) anachambua kwa jumla vipengele mbalimbali vinavyoficha maana na dhamira na kujenga Upande wa Pili wa kazi ya fasihi, bila ya kuvihusisha na matini nyingine kama vile tamthiliya, nathari na ushairi. Vipengele hivyo ni uumbaji wa wahusika, jazanda, sitiari, kinaya na methali. Anaeleza kuwa kipengele kama cha wahusika hutumika kueleza mambo ya aibu na ya kashifa bila ya kumuudhi mzungumzwaji. Pamoja na maelezo haya, mwandishi hakuonesha vipi vipengele hivi vinaweza kutoa maana ya juu na ile iliyofichama. Labda kwa hili tuwaangalie wahakiki na wachambuzi namna wanavyovihusisha na kutoa maana hizo.

Utangulizi wa Sengo katika Haji (1994) na Mulokozi katika Mohamed (2003) na TUKI (2012) wanachambua fasihi kuwa ni kitu chenye pande mbili, ule ulio dhahiri na ule uliofichama. Wanaeleza kuwa upande wa pili wa fasihi unajengwa na vitu tofauti kama vile taswira, jazanda, mafumbo, na matumizi ya tamathali za semi. Shairi la “Uokolewe” linafafanua, lakini kwa mficho wa aina yake, dhamira ya Kimbunga juu ya uchumi wa nchi. Pia “Chaka” ni shairi lenye maana mbili, maana sahili ya chaka ni

msitu uliozongana, pamoja na maana ya ndani ambayo ni tabia hasi za uongozi au za jamii kwa ujumla (Haji, 1994: viii).

Sengo anaongezea kuwa, fasihi huweza kutolewa maana na dhamira kwa jicho la fasihi na sio kupitia fasihi nyingine. Hii ina maana kuwa fasihi huhakikiwa kulingana na jamii lengwa. Mulokozi katika Mohamed (k.h.j.) ameongezea kwa kusema kuwa "haikuwa nia yetu kumhakiki kwa undani mtunzi huyu, na hatukufanya hivyo….ili kumwelewa na kumfaidi ipasavyo, inabidi msomaji na mhakiki amwingie akiwa na zana thabiti za kupigia mbizi na kuogelea katika bahari ya ushairi. Maelezo haya yanadhihirisha wazi mhakiki kaichambua kazi kwa maana sahili au mtazamo wa juu juu na kumtaka msomaji na mhakiki mwingine aichambue na kuihakiki kazi hii kwa maana ya ndani/iliyofichama. Marejeo haya bado yanautia nguvu utanzu wa ushairi kuwa ndio zaidi wenye kujengwa kupitia maana au dhamira zilizofichama na kutuonesha kama kwamba utanzu huu ndio tu wenye haki ya kutumia lugha za kitamathali.

Waandishi hawa wanakubali kuwa kuna maana halisi na maana iliyofichama ambayo ndiyo inayotoa dhamira zilizofichikana, hata kama maelezo yao yanajikita zaidi kwa upande wa ushairi kuliko katika tamthilia na riwaya. Kezilahabi (1983) anaeleza kuwa historia ya fasihi yaelekea kuonyesha kuwa tanzu hizi yaani ushairi (kama tendi) na riwaya zilikuwa pamoja na uhusiano mkubwa kwa muda mrefu. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa vipengele vinavyojenga upande wa pili wa kazi za ushairi ndiyo hivyo hivyo vinavyojenga upande wa pili wa kazi za riwaya. Madumulla (2009) anasisitiza kuwa, katika riwaya tamathali ya usemi huweza kuwa na maana fiche kutokana na kugeuzwa maana yake kamili ili kuwakilisha maana nyingine. Pia, anasema kuwa wahusika, hasa wa kimapinduzi, huweza kutusaidia kupata maana na

dhamira fiche kwa sababu ni wahusika wenye muamko mkubwa na ufahamu mpana wa maisha yao.

Simiyu (2011) anaelezea mafumbo, misimu na methali kuwa, ni semi bainifu zenye kujenga maana fiche. Anaeleza kuwa maana wazi hupatikana katika maneno yaliyotumika moja kwa moja na maana fiche hupatikana kutokana na matumizi ya semi hiyo. Anatoa mfano wa methali ya “Ng’ome akivunjika mguu malishoni hukimbilia zizini kusaidiwa” iliyotumika katika kazi ya *Kusadikika* ya Shaaban Robert anasema:

> Methali hii imejenga maudhui ya riwaya hii kwa ncha mbili. … Lakini katika methali huweza kuwepo maana ya juu na nyingine ya ndani iliyojificha. Maana ya kwanza, inaelekea kuwa katika *Kusadikika* Shaaban Robert alinuia wasomaji na wahakiki wake wapate ujumbe wa kejeli yake kwa kupitia maana ya ndani ya methali aliyoidondoa. Maana hii inawaasa wana-Kuasdikika kuwa ni juu yao kutumia nguvu zao wenyewe (nahii ndio “zizi”) maana ya pili ina ncha mbili; ya kwanza inashughulikia juhudi za watawaliwa wa Kusadikika za kuisihi serikali ya kikoloni iwasikilize malalamiko yao, ya pili ina husu mgongano utokeao mahakamani baina ya Karama na Majivuno (mgongano baina ya watawaliwa na wakoloni) (Senkoro, 2011).

Madondoo haya yanatupa mwanga na kutoa njia kuhusu namna gani tunaweza kuihakiki na kuchambua kazi kwa kuangalia dhamira zilizofichama katika kazi za riwaya; na si kuchukulia vipengele vya mtindo na lugha kuwa ni vya kuipamba kazi ya fasihi au kutoa dhamira sahili tu kama zinavyohakikiwa nyingi ya kazi za fasihi.

Pia, dondoo hizi zinatiliwa mkazo na King’ei (1987) kwa kuchambua jazanda na taswira zilizotumika katika kazi za Ebrahim Hussein na kuzitolea maana na dhamira

zilizofichika katika jazanda hizo. Kwa upande wake, Wamitila (2004) anachambua zaidi kwa kusema kuwa kuna metheli zenye maana sahili na zile zenye maana batini (fiche). Anafafanua zaidi kwa kusema kuwa, ili kupata methali zenye maana batini, ni vyema kuangalia zile methali zilizotumia tamathali. Kwa mfano "Kawia ufike" na "Haraka haraka haina baraka" ni methali zenye maana sahili. Na methali za "Ukilima pantosha utavuna pankwisha" na "Ukelele wa Shundi ni mmoja" ni methali zenye pande mbili – maana sahili na maana fiche. Kiango (1987) anachambua kazi *Tone la Mwisho* na kutuonesha namna gani ucheshi unavyoweza kutoa maana fiche na kutoa ujumbe mzito kwa wasomaji wa kazi hiyo.

Maneno (h.t.) anaenda mbali zaidi kwa kusema kuwa ukitoa fani za lugha pia kuna uteuzi wa maneno na mbinu ya kichekesho. Hivi ni vipengele ambavyo huweza kutoa maana na dhamira zilizofichama. Anachambua kichekesho katika tamthiliya ya *Mashetani* ya Ebrahim Hussein na kuvichambua vicheko hivyo katika maana na dhamira tofauti kulingana na mazingira vilipotolewa vicheko hivyo. Vipo vicheko vinavyoashiria furaha, kejeli na vile vinavyoashiria ushindi juu ya hadaa fulani.

Ama kwa upande wa Mgeni (1983), anaona kuwa dhamira zilizofichama huweza kupatikana kutokana na yale mambo ambayo si ya kawaida na yanayoweza kuleta ugumu kwa wasomaji. Kwa mfano katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ya Muhamed S. Abdalla ametumia misemo kama vile "kinyume cha mambo" na "shibe kumuamini njaa". Misemo hii inadokeza maana ya ndani ambayo huweza kutafsiriwa kulingana na muktadha ilipotumiwa. Kwa upande wa King'ei (2004), anaona dhamira zilizofichama huweza kupatikana kutokana na matumizi ya maneno yasiyo maarufu na yasiyo rasmi katika Kiswahili sanifu. Maneno haya huweza kutokana na lahaja au maneno ya kigeni kiasi cha kumfanya msomaji aingie ndani zaidi na kuchambua

maana ili kupata maana ya wazi na maana fiche. Wafula (1997) na Margareti (1997) wanaenda ndani zaidi katika kuchambua dhamira zilizofichama. Hii ni kwa sababu wanaona kuwa ili kupata dhamira fiche ni lazima mtu aanze kwa kuangalia jina la kitabu na jalada lake. Pia katika kuchambua wahusika na majina yao ni lazima utoe umuhimu wa mwandishi kumpa jina hilo muhusika anayemchambua. Wote hawa wamechambua dhamira zilizofichama zinazopatikana katika kazi ya kifasihi; na wanakubaliana kuwa tunaweza kuzipata kupitia vipengele vya mtindo na lugha anayotumia mwandishi katika kuwasilisha kazi ya kifasihi.

Tunaweza kujumuisha haya kwa maelezo ya Masebo na Nyangwine (2010), kuwa kazi ya sanaa inahitaji uchambuzi na ufafanuzi ili kugundua mazuri yanayowekwa katika kazi hizo. Kazi hii hufanywa na mhakiki. Hii ina maana kuwa kazi ya sanaa si kazi tu ya kusomwa na kupata kilichokusudiwa, bali inahitaji kusomwa kwa kina na kuichambuliwa ili kupata upande wa pili wa kazi hiyo. Semzaba (1997) anaongezea kwa kusema kuwa kizazi cha kila jamii huzipa sanaa zao umbo na maana kutokana na shughuli zake muhimu za maisha katika uchumi, maisha ya jamii, utamaduni na kadhalika. Pamoja na maelezo hayo, wahakiki na wachambuzi wengi walioangaliwa na utafiti huu wanaonekana kudokeza tu juu ya vipengele vyenye kutoa dhamira zilizofichama. Hata wale waliochambua namna ya kupata maana fiche katika vipengele vya lugha au mtindo bado walivichambua na kutafsiri kama ni mfano na si namna gani vinavyotoa maana/dhamira moja kwa moja katika kazi ya fasihi kwa jumla kama sehemu ya uhakiki wa kazi hiyo. Utafiti ulikusudia kuchambua dhamira zilizofichama na kuwa ni egemeo la kupata upande wa pili wa kazi teule za Shafi A. Shafi.

Kwa kuwa utafiti uliangalia riwaya, ni vyema kufahamu kuwa riwaya ni nathari iliyo ndefu na yenye uchangamani wa kifani na kimaudhui. Utanzu huu, unaweza kubeba

vipengele vyote vilivyochambuliwa hapo juu. Pia uliweza kutoa dhamira zilizofichama, kama inavyoelezwa na Mlacha na Madumulla (1991) tofauti ya hadithi fupi na riwaya ni kuwa riwaya hujengwa kutokana na uhusiano tata wa wahusika na dhamira. Neno "tata" ni neno lenye maana kuwa vipengele vya wahusika na dhamira vinaweza kutoa maana zaidi ya moja. Kama walivyoongezea kwa kusema kuwa riwaya, kama kazi zote nzuri za fasihi, inaweza kusaidia kufafanua na kutoa mambo yaliyojificha au yasiyoonekana katika maisha ya kila siku. Maelezo haya yote yanathibitsha kuwa katika riwaya tunaweza kupata upande wa pili wa kazi husika kupitia maana na dhamira zilizofichama kama ilivyoazma ya utafiti huu wa kutafuta upanda wa pili wa kazi teule za Shafi.

## 2.3 Maandiko kuhusu Kazi za Shafi Adam Shafi

Senkoro (2011) na Khatibu (1983) katika uchambuzi wao wa kazi za Shafi A. Shafi wanadai kuwa lugha aliyotumia ni nyepesi hata kama katumia tamathali za semi, misemo, methali, ishara na majazi katika majina ya wahusika. Sababu ya wepesi wa lugha hiyo ni kutokana na uwiano mdogo kati ya fani na maudhui, ambapo maudhui ni makubwa wakati fani ni nyepesi.

Mussa (2007) amemuelezea Shafi kuwa ameandika riwaya zake kwa kufuatilia jamii ya Zanzibar na mabadiko yake kisiasa. Pia ameongezea kwa kusema kuwa riwaya za Shafi zimejikita zaidi katika dhamira ya ukombozi wa jamii ya Zanzubar.

Maelezo haya yamechukuliwa kijumla kwa sababu hata hizo methali na misemo iliyorembwa kwa uchache katika kazi hizo haikufafanuliwa kuwa inaweza kutoa maana zaidi ya moja au la. Aidha, hawajaeleza kuhusu miktadha iliyomsukuma mwandishi kutumia lugha hiyo na ina athari gani kwa wasomaji wa kazi hizo. Pia, wameleza kuwa kazi hizi zimejikita zaidi katika suala la ukombozi. Hii ni dhamira kuu

tu ya mwandishi, kazi ya fasihi hujumuisha dhamira ndogo ndogo nyingi ambazo wakati mwingine hufichama katika vipengele vya mtindo na lugha alivyotumia mwandishi.

Wamitila (2003) anamtathimini Shafi katika kazi zake kuwa katumia mandhari halisi na kutoa uwezo wa kishabihikweli. Anamlinganisha na waandishi wengine wa Zanzibar kwa kueleza kuwa kazi zake zina wepesi wa lugha na uchache wa tamathali hasa katika kazi zake za mwanzo. Kazi hizi zinafanana katika sifa za kimtindo na kazi za akina S. A. Muhamed na M. S. Mohamed kama wasifu wa lugha, mandhari na kisemantiki. Maelezo haya ni ya kulinganisha; hivyo, wepesi wa lugha ni kulingana na kazi nyingine. Pia, maelezo haya yanasaidia kujenga hoja ya utafiti huu kutafiti ikiwa ni kweli wepesi wa lugha katika kazi za Shafi zilitokana na uanagezi katika utungaji au ni mtindo aliokusudia kuutumia katika kazi zake.

## 2.4 Mapengo Yanayojitokeza Kutokana na Mapitio ya Maandiko

Baada ya kupitia maandiko ya wataalam mbalimbali wa kifasihi, wataalam wanathibitisha kuwepo kwa maana na dhamira zinazofichama kupitia vipengele mbalimbali vinavyopatikana katika mtindo na lugha. Hata hivyo maandiko haya yamegundua mapengo yafuatayo:- Kwanza, wahakiki wengi katika kueleza vipengele vya lugha na mtindo hawakuchambua na kueleza namna vipengele hivyo vinavyotoa maana na dhamira zilizofichama katika uhakiki wao. Pili, wahakiki wa kazi za Shafi A. Shafi, pamoja na kukiri kutumia kwake vipengele vya mtindo na lugha kama methali, tamathali za semi, majazi, ishara, taswira na vingine, wameshindwa kutuonyesha namna vipengele hivi vinavyotoa maana na dhamira zilizofichama kupitia vipengele hivyo.

Tatu, hawakueleza chochote juu ya miktadha iliyomsukuma mwandishi kutumia mtindo na lugha ya aina hiyo na kuieleza ina athari gani juu ya wasomaji na wahakiki wa kazi za Shafi A. Shafi. Utafiti huu umeziba mapengo yaliyodhihirishwa hapo juu.

## 2.5 Muhutasari wa Sura ya Pili

Sura hii imezungumzia juu ya maandiko kwa kuangalia dhamira zilizofichama na kuelezea vipengeleo vinavyoweza kutoa dhamira hizo. Pia, sehemu hii imefafanua juu ya dhana ya mtindo kwa upana na kuona namna mtindo unavyoboresha kazi za kifasihi. Sura hii imeangalia pia, watafiti mbalimbali walioangalia kazi za Shafi A. Shafi. Vile vile sura imebainisha mapengo yaliyojitokeza katika maandiko haya. Sura hii inatupa fursa ya kuingia sura ya tatu ambayo itaelezea mbinu za njia za kufanyia utafiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii imefafanua mpango wa jumla wa utafiti kwa kujumuisha vipengele vya mpango wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, jamii ya watafitiwa, mchakato wa ukusanyaji data, zana na njia za ukusanyaji, uchambuaji wa data pamoja na nadharia zilizotumika kuchambulia data hizo. Pia, sura hii imeelezea mipaka ya utafiti huu pamoja na changamoto zilizoukumba utafiti huu.

## 3.2 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani na uwandani. Mwelekeo wa uatafiti ulikuwa wa kiufafanuzi (kitaamuli) na haukuhusisha taarifa za kitakwimu. Data zilikusanywa kutoka katika kazi tatu za Shafi A. Shafi ambazo ni *Kuli*, *Vuta N'kuvute* na *Haini*. Kupitia kazi hizi ufafanuzi na uelezaji wa kina juu ya maana na dhamira zilizofichama ulitolewa. Mtafiti alikwenda uwandani kuchunguza na kupata vielelezo kwa kuwahoji na kuwasaili wanataaluma wa fasihi na waliowahi kuzisoma na kuzihakiki kazi za Shafi. Utafiti huu ulitumia mahojiano kwa wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita, wanafunzi wa stashahada na shahada ya kwanza. Pia, ulitumia usaili wa ana kwa ana kwa wataalam na wahakiki wa fasihi ya Kiswahili.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika mjini Zanzibar. Eneo hili liliteuliwa kwa sababu mbalimbali. Kwanza, urahisi wa kupata huduma za maktaba, ambazo ni maktaba kuu ya Zanzibar

na maktaba za vyuo kama Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo kikuu cha Zanzibar (Z.U.) na University College of Education of Zanzibar (UCEZ) ambacho sasa kinaitwa Sumeit University. Pia, kwa zile data za uwandani, eneo hili lilikuwa ni chachu ya kupata wanafunzi na wataalam waliosoma na kuhakiki kazi za Shafi A. Shafi. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Dar es Salaam kwa jumla lilitumika kama eneo la ziada kwa ajili ya kupata wataalam na rejea mbalimbali pamoja na kumpata mwandishi husika ambaye ni Shafi Adam Shafi kwa sababu, ndiko anakoishi kwa sasa.

## 3.4 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti huu ni wa makundi mawili, jamii ya watafitiwa kwa ujumla wake na sampuli ya watafitiwa.

### 3.4.1 Jamii ya Watafitiwa

Data za utafiti huu zilipatikana kutoka katika makundi yafuatayo:-

a) Kutoka katika kazi teule za Shafi A. Shafi;
b) Kutoka kwa wanafunzi;
c) Wataalam na wahakiki, na;
d) Msanii teule.

### 3.4.2 Sampuli ya Watafitiwa

Uteuzi wa sampuli ulifanyika kwa kutumia mbinu ya sampuli lengwa. Sampuli lengwa, hii ni mbinu inayomruhusu mtafiti kupata sampuli ya kutafitiwa kulingana na jinsi wanavyokidhi haja ya utafiti, mbinu hii inajikita zaidi katika mahitaji ya utafiti kuliko matamanio ya mtafiti, pia ni njia inayochagua watafitiwa wachache katika jamii ya watafitiwa ili kuwakilisha jamii hiyo (Enon, 1998; na Kothari, 2004).

Mbinu hii ilifaa kwa sababu utafiti ulilazimika kuwatafuta wataalam wa Fasihi ya Kiswahili tena wale ambao wamewahi kuzipitia kazi hizi kwa kuzisoma kuzihakiki au kuzitafiti kazi za Shafi Adam Shafi. Kwa upande wa wanafunzi utafiti ulitafuta wanafunzi wanaosoma somo la Kiswahili ambao wamesoma kazi za Shafi Adam Shafi angali moja kati ya zinazotafitiwa. Mbinu hii ilikuwa ni muwafaka zaidi kutumika katika utafiti huu, kwa sababu mbinu hii inatumika katika utafiti wa kiufafanuzi (kitaamuli). Hivyo, sampuli iliyotumika ni:-

a) Kutoka katika kazi tatu za Shafi A. Shafi
b) Kutoka kwa wanafunzi arubaini (40); ambao kumi (10) wanafunzi wa kidato cha tano, kumi (10) wa kidato cha sita, kumi (10) wa Stashahada na kumi (10) wa Shahada ya Kwanza.
c) Wataalam na wahakiki kumi (10) wa kazi za kifasihi, na;
d) Msanii teule.

## **3.5** Ukusanyaji wa Data

Mbinu na zana mbalimbali zilitumika katika mchakato wa kukusanyia data na kuzichanganua.

### 3.5.1 Njia na Zana za Kukusanyia Data

Mbinu zilizotumika kukusanyia data za utafiti huu ni udurusu wa kimaktaba, usaili na mahojaji. Zana zilizotumika ni mwongozo wa udurusu wa kimaktaba, mwongozo wa usaili na muongozo wa mahojiano, kalamu, karatasi, penseli, madaftari na kinasa sauti pia zilitumika. Kwa upande wa data zilizokusanywa maktabani, zana zilizotumika hapa ni mwongozo wa udurusu, kalamu, penseli, karatasi, vitabu, kompyuta pamoja na kinyonyeo. Njia zilizotumika ni usomaji, uchambuzi wa matini na unukuzi. Kalamu,

penseli na karatasi zilitumika kuandikia data zilizokusanywa ambazo ni data za msingi na upili. Kompyuta na kinyonyeo vilitumika kwa ajili ya kuhifadhia kumbukumbu na kuchapia kazi. Vitabu vilikuwa vya aina mbili, vile teule na vile vya kuongezea maarifa ya ziada hivi ni mahsusi kwa kuvisoma na kukusanya data mbalimbali za msingi na za upili. Pia, utafiti ulitumia usaili na udodosaji, udodosaji ulifanywa kwa wanafunzi wa kidato cha tano, kidato cha sita, stashahada na wale wa Shahada ya Kwanza. Usaili ulifanyika kwa wanataaluma wa Fasihi na kutoa data zilizosaidia kukamilisha utafiti huu. Usaili ulihitaji kuwa na MP3 kwa ajili ya kunasia sauti pamoja na madaftari, kalama na karatasi kwa kuandikia na kuwekea dondoo muhimu.

### 3.5.2 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data

Katika ukusanyaji wa data, utafiti huu ulifuata taratibu na miko yote ya utafiti. Kwanza, mtafiti aliomba ruhusa kwa mamlaka yanayohusika pamoja na maeneo yaliyofanyiwa utafiti huu. Pili, mtafiti alijitambulisha kwa watafitiwa na kuwasomea maadili yaliyofuatwa katika utafiti huu. Kisha, mtafiti aliomba ridhaa kwa watafitiwa pamoja na kuwataka mashirikiano yao na kutoa data za kweli na zenye kukidhi haja ya utafiti.

Data za maktabani zilikusanywa kwa kufuata muongozo wa usomaji na kupitia tasnifu za tafiti, vitabu mbali mbali, makala, majarida na vielelezo vingine. Data za uwandani zilikusanywa kwa kufuata muongozo wa usaili na hojaji kupitia sampuli iliyopatikana kwa mujibu wa taratibu za kuwapata sampuli lengwa kama ilivyokwisha chambuliwa katika kipengele cha jamii ya watafitiwa.

### 3.5.3 Udhibiti, Uchambuzi na Uunganishaji wa Data

Data zilizopatikana katika utafiti huu zilidhibitiwa kutumia madaftari, kalamu na kinasa sauti kwa wakati wa usaili. Taarifa zilizohojiwa kupitia mahojaji zilihifadhiwa na kufupishwa katika daftari maalum. Pia, data za maktabani nazo zilinukuliwa katika madaftari kwa lengo la kufanyiwa uchambuzi. Data hizi zote zilichambuliwa kwa mbinu ya ufafanuzi na kuunganishwa kwa utaratibu maalum. Kothari (2009), kwa kuwanukuu Selltiz na Johoda, anaeleza kuwa uchanganuzi wa data ni mchakato unaofavywa kwa njia ya kufupisha data zilizokusanywa na kuziunganisha kwa namna ya kuweza kujibu maswali yaliyokusudiwa. Baada ya uchambuzi wa data hizi ulifanyika uunganishaji wa data. Uunganishaji huu ndio mchakato wa kuandika kwa tasnifu hii. Mchakato wa utafiti huu ulifuata nadharia ya Umuundo na Umarx.

## 3.6 Nadharia Zilizotumika

Utafiti huu ulitumia nadharia mbili, nadharia ya U-muundo na nadharia ya Umarx.

### 3.6.1 Maana ya Nadharia hizi

Nadharia ya Umuundo ni nadharia inayolenga zaidi kuichambua na kuihakiki kazi ya fasihi kwa kuzingatia muundo wa kazi ya fasihi. Wafula na Njogu (2007) wanadai kuwa umuundo unashughulika na lugha. Kiisimu, kuwepo kwa sanaa ni ushahidi unaoonyesha kwamba lugha inaweza kuvyaziwa miundo mingi kadri mtumiaji wake anavyotaka. Lugha inaweza kuvuka vizingiti vingi kimaana. Dhima kubwa ya wahakiki ni kubainisha na kuchanganua utata kama kipengele kinachomuwezesha mwanasanaa kutumia maneno machache kuwasilisha dhana pana au kutumia maneno mengi kuwasilisha maana ndogo. Nadharia hii imeazishwa na kuendelezwa kati ya miaka ya 1960 na kupata umaarufu katika uwanda wa fasihi mwishoni mwa miaka

hiyo. Mwazilishaji wa nadharia hii ni Ferdinard de Saussure na kuendelezwa na waitifaki wengine ambao ni Roland Barthes, Levi-strauss na Tzvetan Todorov (Mushengyezi, 2003).

Misingi ya nadharia hii, ambayo ilikuwa mwega uliosaidia kuchambua data za utafiti huu ni:-

a) Umuundo ni nadharia inayochambua vipengele vya kiisimu, kikiwemo kipengele cha semantiki ambacho huchambua maana. Kifasihi, maana hizi zinaweza kufasiliwa kama maana dhahiri na maana ya kitamathali. Ujuzi wa semantiki unapaswa kufasiri lugha ya kimafumbo kama ilivyotumika katika kazi za kifasihi za kitamathali. Pia, semantiki hutuwezesha kufahamu jinsi lugha isiyokuwa ya mafumbo inavyogeuka na ikawa ya mafumbo.

b) Kwa wahakiki wa kimuundo, viashirii vina maana na uzito mkubwa kuliko viashiriwa. Hii ina maana gani? Mhakiki wa kimuundo anaelekea kuvutiwa zaidi na jinsi maana inavyozushwa au kukuzwa kuliko na maana yenyewe.

c) Msingi wa kiutamaduni/kirejelezi; msingi huu unajegwa na urejelezi wa sifa fulani za kiutamaduni katika kazi fulani kutokana na kutumia vitu fulani vinavyoeleweka na msomaji. Kwa njia hii, kazi inayochambuliwa inapata nguzo muhimu za kiutamaduni.

Utafiti huu ulitumia misingi hii katika kuchambua dhamira zilizofichama. Kwa kuwa nadharia hii inajikita kuchambua maana katika kazi ya kifasihi kwa kuchambua mafumbo na kufanya lugha isiyo ya kimafumbo kuifanya kuwa ya kimafumbo, ilisaidia sana kuchambua data zilizopatikana kupitia riwaya teule za Shafi A. Shafi.

Nadharia ya pili ni nadharia ya Umarx. Nadharia hii inahusishwa na mawazo ya Karl Marx (1818 – 83) na Friedrich Engels (1820 – 95).

Umarx ni falsafa ya kiupembuzi ambayo inasisitiza jinsi mazingira ya kuishi yanavyochukua nafasi ya kimsingi yakilinganishwa na mawazo au imani katika maisha ya binaadamu. Umarx unahusu nyanja mbalimbali kama uchumi, historia, jamii na mapinduzi (Wamitila, 2003). Waitifaki wengine wa nadharia hii ni G. Lukacs, Theodor Adrno, Tery Eagleton. Kwa upande wa Afrika ya Mashariki, ni pamoja na Ngugi wa Thiong'o na Okot p'Bitek. Misingi ya nadharia hii ambayo ilitumika sambamba na misingi ya nadharia ya Umuundo katika kuchambua data za utafiti huu ni:-

a) Historia ya jamii ni muhimu kuzingatiwa katika fasihi. Hivyo, uchambuzi wa riwaya, tamthiliya na ushairi utakuwa bora ikiwa uchambuzi huo utazingatia tajiriba ya watu ya kimaisha, siasa yao, mahusiano ya kiuchumi pamoja na mjengeko wa jamii yao.

b) Kazi ya fasihi huweza kuonyesha imani za jamii, muundo wa jamii au changamoto zake. Ili kukuza na kuonyesha imani/mapendekezo ya wafanyakazi na watumishi wengine, ambao ndio wanaonyonywa na kukandamizwa.

Utafiti huu ulitumia nadharia mbili ili kuweza kufikia malengo ya utafiti huu. Nadharia ya kwanza ilitumia (Umuundo), misingi yake ili jikita zaidi katika kukushanya na kuchambua lengo la kwanza. Na nadharia ya Umarx, misingi yake ilisaidia kuchunguza na kubainisha miktadha iliyomsukuma Shafi A. Shafi kutumia mtindo uliotumika katika kazi zake. Pia, kuchambua athari za mtindo huo kwa wasomaji wake. Nadharia hizi zilisaidia kwa sababu, misingi ya nadharia moja ilikuwa haijitoshelezi kuchambua data za malengo ya matatu peke yake.

### 3.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza jinsi Upande wa Pili wa Kazi za Fasihi ulivyojitokeza katika kazi za Shafi A. Shafi kwa kuangalia maana na dhamira zilizofichama. Kazi ambazo zilichambuliwa moja kwa moja katika utafiti huu ni *Vuta n'kuvute, Kuli* na *Haini*. Riwaya ya *Kasiri ya Mwinyi Fuadi* na *Mbali na Nyumbani* ziliangaliwa kwa ujumla wake tu. Pia katika uchambuzi wa vipengele vya kazi ya fasihi, utafiti huu ulijikita katika kuchambua mtindo na lugha aliyotumia mwandishi kwa kuangalia vipengele vile tu vyenye kutoa dhamira iliyofichama. Kwa upande wa data za uwandani, utafiti ulitumia mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar kwa ajili ya kupata Shule na Vyuo Vikuu vitatu kwa ajili ya kupata wanafunzi wa somo la fasihi.

### 3.8 Mapungufu Yaliyojitokeza Katika Utafiti na Utatuzi Wake

Mchakato wa utafiti huu umepita katika vikwanzo na matatizo mengi mambayo mengine yaligeuka kuwa changamoto, mengine yaliweza kutatuliwa, na mengine kubakia kuwa vikwazo.

#### 3.8.1 Watafitiwa Kutozifahamu kwa Kina Kazi za Mwandishi Huyu

Watafitwa wengi hawazifahamu kazi za Shafi Adam Shafi kwa kina pamoja na kuwa baadhi ya kazi hizi zimo katika mtaala wa kielimu kwa wanafunzi wa Fasihi wa kidato cha tano na cha sita. Watafitiwa wengi wanadai kuwa wamesoma kazi moja tu, *Kuli* ambayo ili kuwemo katika mtaala wa kielimu au *Vuta n'Kuvute* ambayo imo katika Mtaala wa kielimu hadi sasa. Tatizo hili lipo kwa wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita, wanafunzi wa vyuo na hata wahadhiri wa somo la Fasihi. Tatizo hili linaweza kusababisha mapungufu ya hapa na pale katika kazi hii. Mtafiti amelazimika kuzisoma kwa kina kazi hizi ili kuziba mapengo katika mapungufu hayo.

### 3.8.2 Madodoso Kutorudi kwa Wakati na kwa Ukamilifu

Ujazaji wa madodoso umekuwa mgumu na wenye kugharimu muda na fedha nyingi. Hii ni kwa sababu wahojiwa wengi wanapopewa dodoso hawajali na wala hawathamini muda wa mtafiti. Kiasi cha kusababisha utafiti kuchukua muda mkubwa kuwa upo hatua ya kukusanya data.

Hali hii inalazimisha kutoa madodoso mengi iwezekanavyo ili kuweza kufidia madodoso yaliyopotea, kuharibika au kotorejeshwa kwa makusudi na watafitiwa. Mtafiti aliweza kupambana na tatizo la upotevu wa madodoso kwa kutoa madodoso mengi ambayo robo yake hayakurudi. Tatizo la kuchukua muda mkubwa limebakia na kuweka kasoro ya utafiti huu kwa kuvuruga ratiba iliyopangwa katika utafiti huu, hata hivyo mtafiti katumia muda wa ziada ili kazi imalize kwa wakati.

### 3.8.3 Uchache wa Rejea na Maandiko Juu ya Kazi za Shafi Adam Shafi

Shafi Adam Shafi ni miongoni mwa waandishi maarufu na wenye mchango mkubwa katika uwanja wa Fasihi na lugha ya Kiswahili. Lakini, bado mwandishi huyu kazi zake hazijafanyiwa tafiti za kutosha. Hali hii inasababisha kukosekana kwa data za upili.

## 3.9 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Sura hii ilifafanua mpango wa jumla wa utafiti kwa kujumuisha vipengele vya mpango wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, jamii ya watafitiwa, mchakato wa ukusanyaji data, zana na njia za ukusanyaji, uchambuaji wa data pamoja na nadharia zilizotumika kuchambulia data hizo. Pia, sura hii ilieleza na kutaja mipaka ya utafiti na kumalizia kwa changamoto zilizoukumba utafiti huu. Katika sura ijayo utafiti unazungumzia uwasilishaji, uchambuzi na uchanganuzi wa data.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii, data zilizokusanywa zimewasilishwa na kujadiliwa ili kujibu maswali ya utafiti, hivyo kufikia malengo ya utafiti. Uwasilishaji wa data umegawanywa katika sehemu zifuatazo: mosi, ni muhtasari wa uchambuzi wa riwaya teule za Shafi Adam Shafi ambazo ni *Kuli* (1979), *Vuta n'Kuvute* (1999), na *Haini* (2003). Pili ni uchambuzi wa dhamira zilizofichama na kujenga upande wa pili wa riwaya hizi kama zilivyoelezwa katika malengo ya utafiti huu. Tatu ni mjadala wa sababu zilizomsukuma mwandishi kutumia mtindo na lugha aliyotumia. Na nne ni kueleza athari za mtindo huo kwa wasomaji wa kazi hizi.

## 4.2 Upande wa Pili wa Riwaya Teule

### 4.2.1 Muhutasari wa Vitabu Teule

#### 4.2.1.1 Kuli

*Kuli* ni kazi ya Shafi Adam Shafi iliyochapwa kwa mara ya kwanza mwaka 1979 na Tanzania Publishing House. Kazi hii ina jumla ya sura kumi na mbili na mhusika wake mkuu ni Rashidi. Katika sura ya kwanza, mwandishi anaanza kwa kuelezea hali ya maisha ya muhusika Majaliwa ambaye alikuwa na umri wa miaka hamsini na tano, akifanya kazi ya ukuli bandarini. Wakati akiwa na umri huu Majaliwa na mkewe Bi Mashavu walibahatika kupata mtoto wao wa pekee aliyeitwa Rashidi. Majaliwa, kama makuli wengine, alikuwa na maisha magumu, maisha ya chungu jiko kupitia kazi hiyo

ya ukuli. Sura hii inamalizia kwa kuonesha kifo cha Majaliwa pamoja na hali ngumu ya Bi Mashavu na mtoto wake, Rashidi.

Sura ya pili inaanza kwa kutuonesha ugumu wa maisha anaopambana nao Rashidi kila uchao, uliotokana na uyatima alioachiwa na Mzee Majaliwa bila ya kuacha urithi wa maana. Katika sura hii ya pili, ya tatu na ya nne mwandishi anaonesha namna gani Rashidi anavyopambana na maisha kishujaa kwa kutumia nguvu na tambo lake la mwili. Rashidi anapata umaarufu kutokana na uhodari wake wa kazi za ukuli. Ni mtu mwenye kujiamini katika kufanya kazi na hata kusema katika kudai haki yake. Ujasiri huu ndio unaootesha mizizi ya kugombania uhuru na kuanza kudai haki zao za msingi ambazo walinyimwa na mabepari wa kizungu. Kama mwandishi anavyomuelezea:

> Sikiliza Mzee Tindo, Rashidi aliaza “sisi siku nyingi tumefanya kazi pamoja na weye. Tunakuona kama mzee wetu, sisi tunahisi kazi tunayoifanya ni kubwa na malipo tunayopata ni madogo basi tunahisi bora sasa tufanye utaratibu tuongezwe pesa. (uk 49).

Hakuwa jasiri wa maneno tu, bali hata vitendo kama inavyoelezwa:

> Mzee Tindo na wenzake walipofika mbele ya lango la nyumba hiyo walifanya hofu kuingia ndani, lakini Rashidi bila ya kujali kitu chochote ndiye aliyekuwa wa mwanzo kukiuka kizingiti cha lango hilo na kuingia ndani. (uk. 51).

Hali hii ilikuwa ni hatua ya kwanza ya kutafuta uhuru. Kwa mara ya kwanza Rashidi alifukuzwa kazi na kubaki nyumbani bila ya shughuli ya kufanya, na akiranda randa kusaka kazi. Hali hii ilizidisha umasikini katika familia yao. Hata hivyo, baadaye, Rashidi anapata kibarua cha kulipwa kwa kutwa. Sura hii inaonyesha namna gani makuli wanavyodhalilishwa na mabeperi wao kwa kupewa kazi ngumu, kulipwa

malipo madogo; na kubwa zaidi ni kupambana na vipigo. Kuhusu hali hii Mwandishi anaeleza hivi:

> George alimpiga teke kubwa yule kuli aliyesimama upande ule uliojigonga na yule kuli aliinukia juu ya masanduku hayo. (uk. 61).

Mizizi ya suala la ukombozi imechipuka katika sura hizi kwa kuonyesha harakati za akina Faraji za kuwaelimisha makuli na kuwataka wawe na umoja katika kujikomboa. Faraji anatumia vikaratasi katika kusambaza taarifa na ujumbe wa ukombozi. Pia Rashidi anashawishiwa na Faraji akubali kwenda kusoma. Rashidi bila ya pingamizi anakubaliana na hili.

Sura ya sita inaonesha idhilali wanazopata makuli kutoka kwa mabepari kwa kueleza kisa cha Mafi ambaye anapata ajali kazini na kufariki baharini. Boss Georg hakushituka kwa hili wala hakujali. Hali hii ilichochea moto ndani ya nyoyo za wafanyakazi, viongozi wa chama cha wafanyakazi na wapigania uhuru.

Sura ya nane inaonesha kuwa moto uliowashwa ulikwisha vamka. Sura hii inaelezea namna viongozi wa chama cha wafanyakazi walivyowaunganisha makuli na kuwashajihisha katika kudai haki zao. Hali hii ilipelekea mgomo wa wafanyakazi wa bandarini (makuli). Mgomo huu ulichukua takraban siku kumi. Hatma ya mgomo huu ni kupatiwa ahadi za kuboreshewa maslahi yao. Siku zilipita bila ya kutekelezwa kwa ahadi hizo. Kwa upande wa Rashidi hali yake ya kimaisha ilizidi kuwa ngumu kutokana na mgomo huu pamoja na tukio la kuondokewa na mama yake mzazi, Bi Mashavu. Mwandishi anasema "Hali hii ya maisha kwa kina Rashidi ilizidi kuwa mbaya kwa muda wa zile siku kumi za ngomo." (uk. 97). Katika kipindi hiki cha Rashidi kutokuwa na baba na mama, anaanza kuchukuliwa na rafiki yake Salum.

Rafiki huyu anamtia katika ulimwengu wa starehe na anasa, anampeleka katika ngoma za usiku na vilabuni hadi anakuwa mlevi wa matusi mtaani kama tunavyosawiriwa na mwandishi:

> Ah! Wewe Rashidi unathubutu kufanya hivyo! Sijakufikiria hata kidogo! Umenifuata kwetu ilhali umelewa namna hiyo. Umekusudia kuja kunivunjia heshima yangu siyo? (uk. 122).

Haya ni malalamiko ya Amina kwa Rashidi, mtu aliyemtegemea kuwa na tabia njema. Na ndio maana alimkubali kuwa mchumba wake.

Sura ya Tisa inazungumzia madhila ya makuli wanayopata kazini kwao, zaidi inaeleza suala la uchumba wa Rashidi kwa Amina. Suala hili limezungumziwa kwa kina tokea matayarisho ya posa hadi kuoana kwao. Pia, sura ya kumi, imeelezea maisha ya ndoa ya Rashidi na Amina. Pia imeelezea kilele cha migogoro ya wafanyakazi na wazungu. Mwandishi anaonesha mapambano ya wazi wazi kati ya makuli na mabepari wao, chama cha wafanyakazi na wakolini kwa jumla.

> Nani unamwambia blal ful ng'ombe we! Yule mfanyakazi alijibu na hapo Georg na mfanyakazi huyo walivaana maungoni na kuanza kububurushana. (uk. 150).

Viongozi wa chama cha wafanyakazi walijipanga na kuweka mkakati wa kudai haki za wafanyakazi. Waliandaa rasimu ya madai na kuiwasilisha katika kampuni ya wazungu inayomiliki bandari. Makuli nao walielimisha familia zao juu ya dhana ya ukombozi.

Sura ya kumi na moja ndiyo iliyojenga kilele cha kazi hii. Chama kilifanya harakati za kutayarisha mgomo. Walifanikiwa kufanya mgomo na hatua ya kwanza mgomo ulizusha mapambano baina ya makuli na askari kwa kupigana huko bandarini. Baada

ya vurugu hizi, serikali ya kikoloni ilikipiga marufuku chama cha wafanyakazi kuweka mikutano ya aina yoyote. Hali hii ilisababisha hali ngumu ya maisha katika familia za makuli, hasa akina Rashidi ambao walikamatwa na kutiwa ndani. Chama kililazimika kuhudumia familia za waliotiwa ndani na hata wale walio huru ambao hawana kitu. Hali hiyo ngumu ya maisha ilipelekea viongozi wa chama kuitisha mkutano mkubwa wa makuli. Bila ya mafanikio yoyote mkutano ulisababisha vurugu kubwa baina ya wafanyakazi na askari wa kikoloni waliovamia mkutano ule. Mwandishi anaeleza:

> Bakari alipogeuka upande wa pili kutaka kumsukuma askari aliyetaka kumvuta mguu, alipigwa risasi ya kifua na askari mwingine aliyekuwa amejibaza kichochoroni kwa mbali kidogo. (uk. 184).

Hizi zilikuwa juhudi za Waingereza za kuzivunja juhudi za wazalendo na wenyeji wa Zanzibar za kutafuta uhuru wao.

Sura ya kumi na mbili inaeleza mchakato wa kesi ya Rashidi ya kumuhujumu afisa wa polisi katika mgomo wao wa mwanzo. Rashidi akiwa ndani anapata taarifa ya mgomo mwingine, vifo vya baadhi ya viongozi wa chama na hali ngumu ya maisha ya familia yake. Alipata taarifa hizi kupitia barua aliyopenyezewa gerezani kutoka kwa mke wake. Kesi inatolewa hukumu kwa Rashidi kufungwa miaka mitatu na kazi ngumu. Na hii ikiwa ni hatima ya riwaya hii.

#### 4.2.1.2 Vuta n'Kuvute

*Vuta N'kuvute* ni kazi ya Shafi Adam Shafi iliyochapwa kwa mara ya kwanza mwaka 1999, na kampuni ya Mkuki na Nyota Publishers. Kitabu hiki kina jumla ya sura ya kumi na nane na kukamilishwa kwa tamati. *Vuta N'kuvute* ni riwaya ya tatu kutungwa na kuchapishwa miongoni mwa kazi za Shafi Adam Shafi. Kazi hii ni kazi ya kwanza

kuaza kupata ubora katika ubunifu baada ya kupata uzoefu kupitia mawazo ya wachambuzi na wahakiki kutoka katika kazi zake mbili za mwanzo. Kazi hii imetolewa sanifu mpya 2014 ambayo tofauti yake kubwa ni kupungua kurasa kulinganisha na ile ya kwanza. Tofauti hii huweza kumchanganya mpitiaji wa kazi hii ikiwa atatumia sanifu mpya kwa kuwa marejeo ya kazi hii yamejikita katika chapisho la kwanza la 1999. Riwaya hii kama zilivyo riwaya zake nyingine, ametumia mtindo wa matukio ya kihistoria, kutumia fasihi simulizi ndani ya fasihi andishi kwa kutumia nyimbo za kila aina, methali, mtindo wa barua pamoja na matumizi ya monolojia na diyolojia.

Sura ya kwanza inaaza kwa kumueleza Yasmini na mumewe Bwana Raza. Mwandishi anaanza kwa kuchora taswira ya uzuri wa Yasmini. Taswira hii ambayo inajenga mvuto na hamu ya kusoma kazi hii, ili msomaji aone hatima ya kazi hii. Yasmini ni mtoto wa Kihindi mwenye umbo la kuvutia.

> Yasmini alikuwa na kijuso kidogo cha mdawari mfano wa tungule na macho makubwa ambayo kila wakati yalionekana kama yanalengwa lengwa na machozi. Alikuwa na pua ndogo, nyembamba na chini ya pua hiyo ilipangana midomo miwili mizuri iliyokuwa haitulii kwa tabia yake ya kuchekacheka. (uk. 1).

Sura hii imeeleza mazingira yote ya ndoa ya Yasmini na mume wake wa kwanza, Bwana Raza, na namna alivyokuwa akiishi naye. Bwana Raza alikuwa mtu mzima, alikuwa Muhindi kama alivyo Yasmini na alikuwa mfanyabiashara. Hata hivyo, hakuwa chaguo sahihi la Yasmini kuishi naye kama mume. Bwana Raza aliamua kuhama Zanzibar kwenda Mombasa Kenya kwa ajili ya kuboresha biashara yake. Baada ya kufika Mombosa ndoa yao inakumbwa na matatizo ya hapa na pale kutokana

na kutoridhika kwa Yasmini kuolewa na Bwana Raza. Yasmini alivutika na mji wa Mombasa, naye akawavutia vijana wa Mombasa kama ilivyotokea kwa kijana Bukheti, ambaye ni jirani yake. Hatima ya yote, Yasmini aliamua kumtoroka Bwana Raza na kurudi kwao Zanzibar.

Katika sura ya pili mpaka ya tano, mwandishi anatuonesha namna Yasmini anavyoingia Unguja kutoka Mombasa. Anafika kwao na kufukuzwa na mjomba wake kwa kuwa kamtoroka Bwana Raza. Kuanzia hapo Yasmini anahamia uswahilini na kupokelewa na Mwajuma, shoga yake wa zamani aliyekuwa mteja wa Bwana Raza. Yasmin anaishi maisha mapya getoni kwa Mwajuma. Huko anakutana na mazingira mageni na magumu, anakutana na watu wapya kwake na kujuana nao, wengine wanakuwa marafiki na baadaye kuwa wapenzi. Mwandishi anatuelezea juu ya maisha ya Yasmini na Mwajuma:

> Siku zilivyozidi kupita ndipo ushoga baina ya Yasmin na Mwajuma ulivyozidi kustawi mfano wa bustani iliyokuwa ikitiliwa maji kila siku. Baina yao hapakuwa ugomvi wa kutofautiana na wote wawili wakawa na maisha ya bahati nasibu, leo wapate kesho wakose. (uk. 44).

Sura ya sita mpaka ya kumi na mbili zinatuonesha namna Denge anavyoendesha mapambano ya kuwapinga wakoloni wa Kiingereza waliokuwepo Zanzibar, kwa kushirikiana na akina Mambo, Chande, Yasmin na wengineo. Mwandishi anaeleza:

> Najua sana kama polisi wananitafuta kila n'napokwenda lakini nimewashinda ujanja. Hata wakinikamata wakanifunga kazi hii itaendelea kwani siko pekee yangu, tupo wengi Zanzibar, Darsalama, Ulaya kila pahali duniani. (uk. 108).

Mapambano hayo yalifanywa kwa njia mbalimbali na kushirikisha wazalendo na wafanyakazi wanaodhalilishwa. Walisambaza vikaratasi kwa ajili ya kuelimisha wazalendo, na kutoa propaganda juu ya wakoloni. Pia, walitumia maandamano, migomo na hata kuwafanyia fujo wakoloni katika sehemu zao za starehe. Wakoloni nao walitumia njia na mbinu mbalimbali za kuvunja jitihada za wazalendo. Pamoja na haya wakoloni walishindwa kuvunja juhudi hizo kama anavyoeleza mwandishi:

> Waliingia ndani na baada ya kuingia tu Yasmin alimkabidhi Denge yale makaratasi. "Koplo Matata kanambiya niyalete kwako lakini wewe usijue kama nimeyeleta. (uk. 137).

Wakati Yasmin akitumiwa na wakoloni, anaamua kuwasaliti na kuungana na mpenzi wake Denge wanajaaliwa kupata mtoto wa kiume. Mtoto huyu baadaye alipelekwa Donge kwa mama yake Mwajuma, kwenda kulelewa. Pia anapambana na Shihab, mtu ambaye anakufa na kuoza kwa uzuri wa Yasmin hadi kuamua kumtamkia kuwa anampenda kwa ajili ya ndoa. Yasmini anaolewa na Shihab lakini bado anampenda Denge. Shihab anamuhamishia Yasmin Tanga na kumtawisha. Yasmin anampenda Denge, ila Denge anapenda harakati zake za ukombozi. Denge ni mkuu wa harakati na muunganishaji wa harakati hizo baina ya wale walio Dar es Salaam na walioko Ulaya na wale walio Zanzibar.  Denge anamkumbuka Yasmin baada ya harakati zake, wakati anataka kupumzika. Kwa ufupi, Denge anajali harakati zake za ukombozi zaidi kuliko mapenzi, kama mwandishi anavyoeleza:

> Alichukua moja na kumpa Mambo "soma" alimpa karatasi moja iliyokuwa imechapwa kwa maandishi makubwa. Alisoma, "kufa au kupona tunataka uhuru". (uk. 166).

Hali hii inaonesha namna gani alikuwa na simanzi ya ukombozi zaidi kuliko kumfikiria Yasmin.

Sura ya kumi na tatu mpaka ya kumi na nane inaonesha namna matukio yanavyoshuka chini, kwa kukamatwa na kutiwa ndani wanaharakati wa kupigania uhuru. Wakoloni walianza kuwakamata akina Denge na wenzake. Waliwafungulia kesi zisizokuwa na ushahidi. Hali hii haikuwavunja moyo, walipotoka ndani waliendelea na harakati kama kawaida. Yasmini akiwa na mume wake Shihab huko Tanga, maisha ya utawa yalianza kumshinda na kufanya jitihada za kumtoroka, kama alivyofanya kwa Bwana Raza. Kwa Shihab yalikuwa makubwa zaidi kwa kupatwa na kihoro kwa kudhani Yasmini kafariki baada ya kusikia ndege aliyoambiwa kuwa atapanda Yasmin imeanguka na abiria wote wamefariki. Yasmin alikuwa na nia ya kupanda ndege ile, lakini hamu ya kutaka amuone Denge ilikuwa haijakatika. Alikuwa bado hajamuona kipindi kirefu.

Mvuto wa Yasmini kwa Bukheti haukuishia Mombasa. Ilibidi amfuate Unguja na kumsaka nyumba hadi nyumba. Alifanikiwa kumkuta, kiu yake ikaanza kuridhika. Yasmin hakuwa na mapenzi na Shihab wala Bukheti bali alikuwa amevutika na Denge aliyemfanya kuwa mwanaharakati wa kupigania uhuru na kusaliti ubaguzi wa Wahindi wa kutotaka kuolewa na Waswahili. Yasmin anampenda Denge, na Denge sasa yuko gerezani. Pia, Bukheti anampenda Yasmin roho amlipe pumzi. Yasmin alimtaka Bukheti ashiriki katika mchakato wa kumtorosha Denge kutoka gerezani. Mipango ya Denge kutoroka gerezani ilipangwa na Mambo, Panzi, Yasmini na washirika wengine. Hali hii ilitoa vuta n’kuvute kati ya kupigania uhuru na mapenzi. Yasmin akivutwa na Bukheti na yeye anamvuta Denge kama inavyoelezwa:

> Denge alipanda ngazi, Mambo ameizuia ngazi kwa chini, Yasmin ameizuia ngazi kwa juu, Bukheti anamvuta mkono Denge kumsaidia kupanda jahazi. Alipanda mpaka juu akaingia ndani, alipoingia ndani akaangukia juu ya mikono ya Yasmin, wakakumbatiana wameng'ang'aniana kama kupe akiing'ang'ania ngozi… Yasmini na Bukheti walishuka kutoka jahazini na kuingia ndani ya mashua, Denge amesimama anatazama wezake. (uk. 273 – 274).

Haya yalikuwa mafanikio ya kumtorosha Denge gerezani. Suala hili lilikuwa ni faraja kwa Bukheti na kuwa fursa ya kuazisha harakati za uchumba kwa Yasmin. Kwa kuwa Denge hakuwa na mapenzi ya kweli kwa Yasmin alikuwa na mapenzi na harakati zake tu. Aliridhia suala la uchumba wa Bukheti kwa Yasmin na kuibariki ndoa yao.

Tamati ya kitabu: Bwana Raza anaoa mke Mombasa na mambo yake yanakuwa mazuri kwake. Anapata mtoto na kumuita Yasmin. Denge anaondoka Zanzibar na Yasmin anakwenda Tanga kuchukua vitu vyake na urithi kutoka kwa marehemu Shihab. Bukheti anamshawishi mjomba wake aende kumposea Yasmin. Posa yake inakubaliwa baada ya mvutano mzito wa kuvunja ubaguzi wa Muhindi kwa Mswahili, ubaguzi usio na msingi wowote. Bukheti anamuoa Yasmin, na kufanya sherehe kubwa na kufurahia ndoa yao. Bukheti anahamia Zanzibar rasmi na kuwa ni mfanya biashara ya madoriani. Yasmin na Denge wanabaki kukumbukana kupitia mtoto wao na salamu wanazotumiana kama anavyoeleza:

> Baada ya miezi mitatu Yasmin akapata kadi kutoka kwa Denge akampa hongera kwa kuolewa na kumtakia kila la kheri na mafanikio katika maisha. (uk. 346).

Hii ndio hatima ya “vuta n’kuvute” ya kupata ujaliwacho na kukosa ukipendacho, kwani Yasmin anakosa Denge na kupata Bukheit; na Denge anahama Zanzibar na kuhamia ughaibuni.

### 4.2.1.3 Haini

*Haini* ni riwaya iliyoandikwa na Shafi Adam Shafi na kuchapishwa mwaka 2003 na kampuni ya Longhorn Publishers, chapa nyingine zimetolewa 2010 na 2011. *Haini* ni kazi ya nne ya Shafi Adam Shafi kutungwa. Katika kazi hii mwandishi ametumia mtindo wa matukio ya kihistoria, kutumia fasihi simulizi ndani ya fasihi andishi kwa kutumia nyimbo za kila aina, methali, pamoja na matumizi ya monolojia na diyolojia.

Riwaya hii ina sura ishirini na saba. Muhusika mkuu wa riwaya hii ni Hamza. Mwandishi anaanza kazi yake kwa kuichora picha halisi ya siku ya kuuwawa kwa muhusika Kigogo. Anajaribu kueleza hali ilivyokuwa maeneo ya mji wa Zanzibar, hususan maeneo ya Darajani na Kisiwanduwi ambapo yalifanyika hayo mauwaji hadi Mnazi Mmoja, hospitali kuu ya Zanzibar. Katika sura hii ya kwanza, mauwaji yanafanyika na Hamza yupo kwake Malindi akizungumza na marafiki zake, Fadhili na Pango. Kilichowashitua ni kusikia milio ya risasi, walipoangalia nje wanaona watu wanakimbia huku na kule. Hamza na wezake walitoka nje na kuanza kukimbia bila ya kujua watu wanakimbia kitu gani. Hamza alikimbilia kwa mkewe, Bi Khadija. Bi Khadija alikuwa kwao kaenda kujifungua mtoto wao wa kwanza. Huko mtaa wa Kisima majongowe. Kwa siku hii, Hamza alilala kwa wakwe zake aliko mke wake. Hadi muda huo hajajua nje kumetokea nini? Alichokisia redioni ni amri ya kutotoka nje baada ya magharibi. Siku ya pili yake mapema, Hamza wanagongewa mlango na askari na kuambiwa kuwa yuko chini ya ulinzi. Bila ya kujua lolote linaloendelea kwa watu wa nyumba ile, Hamza alikamatwa na kupelekwa gerezani. Baada ya hapo,

mwandishi anatuonesha maisha ya gerezani, maisha ya kamata kamata kwa mwenye hatia na asiye na hatia.

Sura ya pili mpaka sura ya kumi na saba zinaonesha dhili na mateso wanayopata watuhumiwa; kila aina ya mateso waliyaonja wao. Huku wakihamishwa kutoka selo moja kwenda nyingine na gereza moja kwenda nyingine kulingana na mtu anavyotaka kuteswa na wenye mamlaka ya kufanya hivyo. Tunaambiwa:

> Lo!" Haramia alishituka "kumbe wamineleta huku ili niwe ndiyo mwisho wa maisha yangu. Maisha yangu yamalizike kwa kuwa chakula cha chatu, watu wasijue nimepotelea wapi." Anachacharika pale alipokaa, anawaza jinsi gani Kanali Bunju anaweza kuwa katili kiasi cha kumgeuza binaadam mwezake kuwa chakula cha chatu. (uk. 171).

Kazi hii ilihadithia maisha ya gerezani kwa kuonesha namna watu wanavyopokea mateso. Pia, anaeleza namna binadam anavyoweza kusahau dhiki zake wakati bado yupo katika dhiki ile. Wakati mwingine watuhumiwa walicheza, walifurahi na kutaniana kama kwamba hawapo katika kizuwizi, kama mwandishi anavyoeleza:

> Ili kwao siku zisiwe zinadorora, wamewekewa michezo namna mbali mbali ya kuwaburudisha na kuwaondolea ukiwa mle chumbani. Dhimna, karata, dama na huwachangamsha siku nzima (uk. 202).

Kwa kuwa watuhumiwa wengi wao walikamatwa bila ya makosa ya msingi na kukosekana kwa ushahidi juu ya lile wanalotuhumiwa, walilazimishwa na wakubwa wa magereza kukiri makosa watakayokwenda kusomewa mahakamani kwa kuhadaiwa kuwa kukiri kosa ni njia rahisi ya kuachiliwa huru. Mwandishi anasema:

> Sisi tunajuwa kwamba huhusiki lakini ombi letu ni kukutaka ukubali. Ujidai kama vile umo na unawajua wengine. “Tuna orodha ya majina hapa tutakupa na wote hao tumeshawatungia hadithi kuthibitisha vipi wanahusika” alieleza Kanali Mapepe kwa sauti ya upole iliyojaa busara tele. (uk. 82).

Hii ilikuwa mbinu tu ya kuwatia kwenye hatia; na yule aliyekataa kukubaliana na hali hii awekwa mazingira magumu zaidi ya yale aliyokuwa nayo; na ikibidi walibadilishwa selo au gereza kabisa. Kama yalivyomkuta Hamza anapotuambia:

> “Mimi siwezi kukubali mtego huo” alisema Hamza, “Unasemaje” aliruka Kanali Bunju, akasimama kutoka pale alipokuwa amekaa. Alinyanyua bastola yake akafyetua risasi mbili. Zote zikapiga ukutani. Kama “*Cow boy*” aliyeingia baa kufanya fujo ... Mpeleke chumba cha giza aliamrisha Kanali Bunju. (uk. 82).

Mambo haya yalikuwa ya kawaida kwa waliopinga kushirikiana nao na hata kuuliwa kabisa.

Katika sura ya kumi na nane na kumi na tisa mwandishi anaturejesha nyuma kwa kututoa gerezani na kutupeleka mitaani na kwenye familia ya Khadija, mke wa Hamza. Katika familia hii pamoja na ya jamii kwa jumla maisha yalikuwa magumu. Vitu vilikuwa adimu na shida kuvipata hata kama mtu anapesa yake. Kama anavyoeleza kuhusu adha ya chakula: “Chakula hicho hutolewa kwa mujibu wa ukubwa wa kila ukoo.” (uk. 178). Hadithi juu ya mahaini zilienea kila kona ya jamii, wake na watoto wa mahaini waliishi kama mayatima na ulitima kwa kuwa mbali na baba na waume zao pamoja na kutengwa na jamii. Walionekana kama ni sehemu ya mahaini. Familia za mahaini hazikutulia, ziliandamana kwa siri kutafuta njia za kuwatoa watu wao. Walikwenda kwa waganga, waliwafuata wakubwa, na hata kufuatwa wao kwa lengo la

kutoa rushwa ya ngono na wakubwa kwa ujira wa kufanyiwa mpango wa waume zao kutoka garezani. Mwandishi anaeleza:

> "Ndio salamu zenyewe hizo ulizoniitia?" Khadija aliuliza. "Sikiliza bwana mimi ni mke wa mtu, n'na mume wangu na mume wangu amefikwa na matatizo yuko jele kwa muda mrefu … wewe kama kweli binadam nisaidie kwa shida yangu hiyo. Nisaidie mume wangu atolewe. Alisema Khadija.

Jitihada hizi hazikuishia mitaani bali hata katika gereza. Huko watuhumiwa waliomba dua, na kujitia tamaa angalau ya kutiana moyo, ya kuwa siku moja watatoka gerezani.

Sura ya ishirini mpaka ya ishirini na sita zinaelezea mshuko wa kasi wa kilele cha matukio. Kesi zilipelekwa mahakamani na kuanza kusikilizwa. Harakati za wakuu wa magereza za kuwataka mahaini wakiri makosa waliyopangiwa ziliongezeka marudufu. Huku kukiwa na watu waliokubaliana kabisa na mtego huo. Wapo walioushitukia kuwa ni mtego wakiwa tayari wameingia katika mtego huo. Kama inavyoelezwa; "Waongo wakubwa. Tukubali tusikubali watatunyonga tu." (uk. 202). Wanajamii kusikia hatua hii ya mahaini kupelekwa mahakamani nao waliwatolea hukumu yao. Wengine wakawapa hukumu ya kunyongwa. Wengine wakawaombea dua ili wasalimike na hukumu hiyo.

Mahakama ilijipanga kwa kutayarisha jopo la mahakimu wazoefu. Mawakili wa serikali walitayarishwa waliomahiri kwa kumtia mtu hatiani kama inavyoelezwa:

> Mahakimu wa mahakama hizo akawateua yeye mwenyewe na watatu katika hao ndio waliopo hapo, mwuza samaki, mwuza maziwa na mwalimu wa chuoni. Wanahukumu kesi ya mahaini waliomuuwa Kigogo mwenyewe, mfadhili wao aliye watoa huko walikotoka kwenye soko la samaki, mikeka ya chuoni na kwenye kibao cha baiskeli, akawaweka juu ya viti, vile vya heshima, akawapa na satua ya kutoa hukumu waitakayo kwa kesi yoyote ile. (uk. 232 – 233)

Hatima ya yote hayo, katika sura ya ishirini na saba, mwandishi anaonyesha hukumu ya kesi yote. Wakatokea walionusurika na wale waliobainika na hatia ya uhaini. Waliosalimika ni wale walioushitukia mtego wa panya na kuuruka mapema. Na waliokutwa na hatia ni wale waliokosa subira na uvumilivu wakiwa gerezani. Wakapata tamaa ya kutolewa gerezani na kuokolewa maisha yao na wale maadui wao. Kumbe ilikuwa ni mtego na kujitoa hatiani kwa wakubwa wasije kuwa waliwakamata watu bila ya hatia. Kwa kuhitimisha tukio hili mwandishi anaeleza

> Leo tumekuja kukuoneni na madhumuni ya kuja kwetu ni kuja kuthibitishieni ile ahadi yetu kwamba aliye kuwemo hatoki na asiyekuwemo haingii (uk. 266).

Hamza anabahatika kuwa miongoni mwa watu wasio na hatia ya uhaini na hivyo anatoka gerezani. “Na hata hao waliobakia nao pia watatoka tu”. Alimalizia Hamza kufustia tukio hilo la kuachiliwa. (uk. 267).

### 4.2.2 Dhamira Zilizofichama

#### 4.2.2.1 Dhana ya Maana na Dhamira

Utafiti umebaini kuwa sehemu kubwa ya jamii haijui uhusiano wa moja kwa moja kati ya maneno maana na dhamira. Wengi wao wanajua na kutumia istilahi ya dhamira katika uchambuzi wa kazi ya fasihi kuliko matumizi ya neno maana. Pia, kuna baadhi ya wanafasihi ambao wanachanganya dhana baina ya maudhui na dhamira katika kutoa maana na hata kuchambua kazi za kifasihi. Aidha, utafiti ulibaini kuwa baadhi ya wanafasihi huamini kuwa dhamira ni maudhui au lengo au dhima au kusudio. Maana imechanganya dhana nyingi ambazo ni tofauti katika uwanja wa fasihi. Kuna dhamira, maudhui, na dhima; hizi ni dhana tofauti na huweza kuchambuliwa katika hali mbali mbali katika uchambuzi wa kazi ya fasihi.

Dhamira ni dhana iliyo maarufu katika kuchambua kazi ya fasihi, kiasi kwamba utafiti uliweza kuibuia mitazamo mbalimbali juu ya maana ya dhamira. Maana zilizoibuliwa zinafanana sana kimaana na kutofautiana kwa istilahi zilizotumika katika kuchambua dhana hii. Miongoni mwa maana zilizoibuliwa na utafiti huu ni kama zifuatazo:- mosi, dhamira ni malengo ya mwandishi aliyojiwekea ili yafikiwe kwa wasomaji/jamii katika kazi yake. Pili, dhamira ni kusudio la kazi ya fasihi alokusudia mwandishi kulifikisha kwa jamii husika. Tatu, dhamira ni ujumbe wa jumla wa kazi ya fasihi unaotoa fundisho na majumuisho ya kazi hiyo. Nne, dhamira ni ili namna msomaji anavyotafsiri kazi ya fasihi na kupata maana kutokana na kazi ya fasihi ilivyo. Tano, dhamira ni idili zinazopatikana katika hisi ya msomaji au msikilizaji baada ya kusoma au kusikiliza kazi ya fasihi. Na sita, dhamira ni wazo la mwandishi ambalo analikusudia liwafikie hadhira wake.

Kwa jumla, maana hizo zote ni sahihi katika kujenga dhana nzima ya dhamira. Dhamira ni dhana pana, ambayo huweza kutafsiriwa kwa namna mbalimbali na

kulenga dhana ile ile. Kwa kujumuisha, utafiti huu unaieleza dhana ya dhamira kuwa ni lengo/kusudio, ujumbe, idili au wazo la mwandishi ambalo hupatikana katika kazi ya fasihi kupitia uhakiki au uchambuzi wa kazi hiyo. Dhamira ni kipengele ambacho hupatikana katika maudhui ya kazi ya fasihi au ni sehemu ya maudhui ya kazi ya fasihi. Katika kazi ya fasihi huweza kupatikana dhamira kuu kama wazo kuu la mwandishi, ikiambatana na dhamira ndogo ndogo za kazi hiyo.

#### 4.2.2.2 Dhana ya Maana na Dhamira Zilizofichama

Utafiti umegundua kuwa kwa jumla dhamira iliyofichama ni dhana mpya katika jamii ya wanafasihi wengi. Fasihi hutoa dhamira au maana, hizi kwa kawaida huweza kupatikana kwa uwazi wakati wa kuchambua kazi husika. Dhamira hizi huweza kuficha dhamira nyingine ndani yake kupitia vipengele mbalimbali vya kifasihi na ufundi wa kisanaa uliotumiwa kujenga kazi hiyo ya kifasihi. Dhana hii ya dhamira zilizofichama, huweza kuelezwa kwa mitazamo mbalimbali kama ifuatayo:

a) Ni dhamira za ndani ambazo mwandishi anaziwasilisha kupitia lugha maalum au mtindo maalum kama vile lugha ya picha na vipengele vingine kama hivyo. Dhamira hizi huhitaji ujuzi wa kutosha wa kufikiria na kuweza kuchambua vipengele vya lugha na mtindo kwa kina katika kazi ya fasihi.
b) Ni dhamira ambazo hupatikana baada ya kuchambua mafumbo, kuhusisha maana za methali na mtukio ya jamii, utamaduni na hata historia ya jamii hiyo.
c) Ni yale mawazo ambayo mwandishi hakuyaweka wazi na kuwaachia wasomaji wa kazi yake kufikiria kwa undani kilichokusudiwa.
d) Ni dhamira ambazo zinapatikana ndani ya dhamira zilizotolewa kimafumbo.

Kwa jumla, dhamira zilizofichama ni dhamira zinazopatikana kwa kuchambua kuhakiki na kutafsiri baadhi ya vipengele vya fasihi ambavyo huweza kutoa maana au

mtazamo wa kimawazo zaidi ya mmoja. Dhamira hizi huweza kuibuka ndani ya dhamira zilizo wazi. Hii ina maana ya kuwa ni dhamira zinazotoa maana ya juu na maana ya ndani. Dhamira ya wazi au maana ya juu huweza kujenga upande wa kwanza wa kimaana katika kazi ya fasihi na dhamira iliyofichama au maana ya ndani huweza kujenga upande wa pili wa kazi ya fasihi.

#### 4.2.2.3 Vipengele Vinavyojenga Dhamira Zilizofichama Katika Kazi za Fasihi kwa Jumla

Utafiti umebaini kuwa kuna vipengele mbalimbali ambavyo huweza kujenga dhamira zilizofichama. Kuma vile vipengele vinavyopatikana katika fani ya kazi ya fasihi na vile vinavyopatika katika maudhui ya kazi ya fasihi. Vyote hivi vinategemea na umahiri wa kuvitumia katika kazi husika. Kipengele fulani huweza kutumiwa katika kazi ya fasihi na kutoa dhamira iliyofichama na kipengele hicho hicho kikatumiwa katika kazi nyingine lakini kisiweze kutoa dhamira iliyofichama kutokana na jinsi kilivyotumika. Miongoni mwa vipengele ambavyo utafiti umegundua kuwa huweza kutoa dhamira zilizofichama ni pamoja na vifuatavyo:-

##### 4.2.2.3.1 Methali

Methali ni semi fupi zinazotumiwa kubeba ukweli na hekima katika jamii. Methali ni semi maarufu ambazo hutumiwa kunogesha kazi ya fasihi, hususan tamthilia na riwaya. Methali huweza kugawika katika makundi mawili; kuna methali zenye kutoa maana zaidi ya moja bila hata ya kutegemea muktadha wa matini ya fasihi. Kitula na Ahmed (2008) katika utangulizi wanaeleza kuwa:

> Methali huwa na maana fiche yenye undani bali sio maana ya jumla ya maneno yake. Kiini cha maana hutegemea ufasiri wa sitiari ambayo ni lugha ya

> tamathali. Kuna maana ya juu na maana fiche inayotegemea uwezo wetu wa kuelewa falsafa/fundisho lililomo.

Maelezo haya yanatoa uthibitisho kuwa metheli zenye kutoa maana zaidi ya moja bila ya kutegemea muktadha wa matini ni zile zilizotumia tamathali za semi ndani yake. Vile vile ziko methali ambazo haziwezi kutoa maana zaidi ya moja isipokuwa zitakapotumika vizuri katika matini fulani ya kifasihi. Hizi ni zile methali zisizotumia tamathali za semi katika ujengekaji wake kilugha.

Methali ni miongoni mwa vipengele ambavyo hutoa dhamira zilizofichama, hususan zile methali zenye kutoa maana zaidi ya moja bila ya kutegemea mandhari ya matini ya kazi ya fasihi. "… methali huweza kuwapo maana ya juu na nyingine ya ndani iliyojificha" (Senkoro, 2011:20). Hii ina maana kuwa maana ya ndani iliyojificha ndio inayojenga dhamira zilizofichama pale ilipotumika methali hiyo katika kazi ya fasihi au hata mazungumzo ya kawaida. Kitula na Ahmed (W.h.j.) wameongezea kwa kusema kuwa methali hutumiwa ili kufafanua maana, kutilia mkazo hoja au wazo fulani, kukamilisha, kuunga mkono au hata kuthibitisha kauli fulani. Maelezo haya yanathibitisha kuwa methali haitumiki bure bure katika matini au hata mazungumzo fulani ila, huwa ipo kwa lengo maalum kama ilivyokwisha elezwa.

Mifano ya methali zinazotoa maana zaidi ya moja bila ya kutegemea matini ya kazi ya fasihi ni:

i) Mke ni nguo, mgomba kupaliliwa.

Maana ya juu: ni kwamba mke anahitaji matunzo kama nguo, na mgomba unahitaji kupaliliwa kama kawaida ya mazao ya shambani.

Maana ya ndani; a) Mke ndio hifadhi/stara ya mwanamume, na mgomba au shamba kwa jumla ni jambo linalohitaji kutunzwa kwa kupaliliwa. b) Uzuri wa mwanamke unatokana na mapambo, kama nguo na mapambo mengine, na uzuri wa mimea kama mgomba ni kutunzwa kwa kupaliliwa na kutiliwa mbolea.

ii) Mti hupozwa na tundaze.

Maana ya juu: ni mti hudhuriwa kwa sababu ya matunda yake yaliyokuwemo.

Maana ya ndani; Jambo lolote huathirika kutokana na mambo yake wenyewe. Kwa mfano mtu huweza kuathirika au kuadhibika kwa sababu ya mtoto wake, kama kufungwa kwa sababu ya mtoto wake. Methali hii pia inatoa ujumbe unaotokana na methali inayosema “Kikulacho ki nguoni mwako.”

iii) Hawi Musa kwa kuchukua fimbo.

Maana ya juu: ni mtu hatokuwa kama Musa[1] kwa sababu ya kuchukua fimbo[2] kama alivyokuwa akichukua Musa.

Maana ya ndani: a) Mtu hawezi kuwa mtukufu au mwema kwa kujifananisha na watu watukufu au watu wema. b) Wema wa mtu unatokana na vitendo anavyofanya, na sio kwa kujifananisha au kutamani kuwa mwema katika jamii. Methali hii pia huweza kutoa ujumbe unaopatikana katika methali inayosema, “Ada ya mja kunena muungwana ni vitendo”

iv) Maji yakimwagika hayazoleki.

Maana ya juu: ni maji yakesha mwagika hayazoleki.

---

[1] Musa ni nabii aliyepelekwa kwa wana wa Israil na kupewa kitabu cha Tawreti.

[2] Hii ni fimbo maalum aliyokuwanayo Nabii Musa na kuitumia katika kuonyesha miujiza ya kuthibitisha unabii wake mbele ya Muungu wa haki.

Maana ya ndani: ni maneno yakesha toka mdomoni hayawezi kurudia tena na jambo likisha haribika ndio lishaharibika lililobakia ni kujirekebisha kwa ajili ya jambo jingine.

v) Kambare mkunje angali mbichi.

Maana ya juu: Kambare mkunje wakiti bado yuko mbichi anapoweza kukunjika.

Maana ya ndani: a) Tatizo lolote litatuliwe katika hatua ya kwanza ya tatizo hilo, kabla ya kukomaa kwa tatizo hilo. b) Tabia njema na maarifa bora kwa binadam hujengwa wakati mtu yupo katika hatua ya utoto.

Maana ya juu ya methali hizi inatokana na maana ya kikamusi ya msamiati uliotumika katika methali hiyo; na maana ya ndani inatokana na maana ya tafsiri ya taswira, jazanda na semi nyingine zilizotumika katika methali husika.

Aina nyingine ya methali ni zile ambazo haziwezi kutoa maana zaidi ya moja, isipokuwa inapokuwa katika matini fulani na kutumika kisanii. Mfano wa methali hizo ni hizi zifuatazo:-

i) Haraka haraka, haina Baraka.
ii) Kawaida ni kama sheria.
iii) Anayetafuta hachoki.

Methali hizi zinahitaji usanii wa hali ya juu wa kuzitumia katika matini fulani ili ziweze kutoa maana zaidi ya moja kwa sababu hazikutumia taswira, jazanda, tashibiha au tamathali nyingine ya usemi. Maana iliyofichama huweza kupatikana kutokana na muktadha wa matumizi ya methali hizi zitakapotumika kisanii.

#### 4.2.2.3.2 Majina ya Wahusika na Uhusika Wao

Wahusika ni watu, wanyama ama viumbe wengine wenye uhai au wasio uhai waliokusudiwa kuwakilisha dhana, mawazo au tabia za watu katika fasihi (Senkoro, 2011). Wahusika hupewa majina; majina haya huweza kuwa ya wanyama, wadudu, viumbe visivyo na uhai au majina halisi ya kibanadam.

Utafiti huu umegundua kuwa kipengele kingine ambacho huweza kutoa dhamira zilizofichama ni uteuzi wa majina ya wahusika. Kuna majina ya aina mbili: aina ya kwanza ni majina ya kawaida, haya hayatoi maana au picha yoyote kwa uhusika wa mhusika. Majina haya mara nyingi yanakuwa ni majina ya binadamu ambayo huwasilisha matendo mbalimbali ya wanajamii. Aina ya pili ni majina ya mafumbo au yenye kutoa maana fulani kwa uhusika wa muhusika huyo. Majina ya mafumbo ni pamoja na majina ya wanyama, wadudu, viumbe visivyo na uhai na hata majina halisi ya kibanadam yenye kudokeza maana fulani. Mfano wa majina yenye kutoa maana ni Karama, Majivuno, Buruhani, Fadhili, Sungura, Fisi, Zimwi na mengine kama hayo na kama yalivyotumika katika kazi mbalimbali kama vile *Kusadikika.*Mfano wa majina ambayo hayatoi maana ni Juma, Fatma, na John.

Uhusika wa wahusika ni namna au mbinu inayotumiwa na mwandishi kuwasawiri na kuwashirikisha kimatendo wahusika katika kazi yake. Hali hii pia huweza kumsaidia mchambuzi au mhakiki wa kazi ya fasihi kupata maana na dhamira zilizofichama. Kwa mfano uhusika wa Juma katika kazi ya *Mashetani* ya Ibrahim Hussein, unaweza kupata dhamira zilizofichama kwa namna alivyohusishwa katika matukio ya kazi hii.

#### 4.2.2.3.3 Vicheko na Ucheshi

Kazi ya fasihi huweza kutumia vicheko kuashiria jambo fulani ambalo linaweza kuwa la kufurahisha au kuhuzunisha na linaweza kuwa na uhalisia wa kicheko au kejeli katika vicheko hivyo. Kutokana na hali hiyo, vicheko huweza kutoa maana zaidi ya moja, kwa kutoa maana dhahiri na maana iliyofichama. Kwa mfano, katika kazi ya *Mashetani* ya Ibrahim Hussein, kumetumika vicheko kama kejeli; na vicheko hivi huweza kutafsirika katika mitazamo na maana mbali mbali.

Ucheshi ni mpangilio wa maneno katika kazi ya fasihi au sanaa nyingine ambao huwa unalengo la kuchekesha au kumfurahisha msomaji au msikilizaji. Ucheshi aghalabu hutumika kupitisha jambo zito kwa lugha nyepesi au kusahaulisha jambo zito lenye kuhuzunisha na kuliona la kawaida. Ucheshi ni mbinu moja ambayo imekuwa maarufu katika fasihi, mbinu hii hutumika zaidi kwa kazi zenye kutoa falsafa ya hali ya juu, katika jambo fulani. Kwa mfano, mwandishi E. Kezilahabi ametumia mbinu hii katika kazi zake kama vile Rosa Mistika, Kichomi, n.k.

#### 4.2.2.3.4 Mandhari

Mandhari katika fasihi inajumuisha wakati na mahali ambapo matendo ya wahusika yamefanyika katika hadithi au tamthiliya. Haya ni mazingira ambayo wahusika hujengewa nayo na kuonesha matendo yao kwa kuhusishwa jamii fulani katika maendeleo ya kisiasa, kielimu, kiuchumi na hata kiutamaduni katika wakati maalum. Mwandishi huweza kujenga mandhari haya kimafumbo kwa lengo la kutoa upana zaidi katika kuchambua au kuhakiki kazi husika. Hali hii humuwezesha mchambuzi au mhakiki kutoa dhamira zaidi ya moja juu ya kazi ile. Mfano wa kazi hizi ni pamoja na kazi za Shaban Robert kama *Adili na Nduguze*, *Kusadikika*, na *Kufikirika*.

#### 4.2.2.3.5 Jina la Kitabu

Jina la kitabu la kazi ya fasihi ni anuwai kamili ambayo mwandishi hukusudia kudokeza kwa muhutasari wa hali ya juu, kuhusu maudhui yanayopatikana katika kazi yake. Majina haya huweza kuwa ya mafumbo au majina ya kawaida. Majina ya mafumbo pamoja na kuwa yanadokeza juu ya maudhui lakini pia huweza kutoa maana/dhamira zilizofichama ndani ya jina hilo. Mfano wa majina haya ni kama vile *Kimbunga*, *Mashetani*, na *Nyuso za Mwanamke*. Pia, majina ya kawaida nayo huweza kudokeza dhamira zilizofichama kutokana na usanii atakaotumia mwandishi katika uwasilishaji wa kazi yake.

#### 4.2.2.3.6 Uteuzi wa Maneno

Uteuzi wa maneno ni miogoni mwa vipengele muhimu katika ujenzi na upambaji wa kazi ya fasihi. Mbinu hii husaidia kujenga mvuto wa kazi ya fasihi kwa wasomaji na kujenga uchangamfu wa kutaka kuendelea kuisoma kazi hiyo. Mbinu hii husaidia kujenga lugha ya mafumbo na kumuwezesha mchambuzi wa kazi hiyo kutoa dhamira ya wazi na dhamira zilizofichama. Mbinu hii imekuwa ikichambuliwa zaidi katika uchambuzi wa mashairi, pia hutumika katika riwaya na tamathilia.

#### 4.2.2.3.7 Matumizi ya Tamathali za Semi

Tamathali za semi ni mbinu nyeti na ya msingi katika kusanaa kazi ya fasihi kwa kuongeza utamu wa lugha na mvuto wa mtindo. Senkoro (2011:12) anafafanua kuwa "tamathali za semi ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu katika maana, mtindo au hata sauti katika maandishi ama kusema." Zipo baadhi ya tamathali za semi ambazo zinaweza kutumika katika kazi ya

fasihi na kutoa maana na dhamira zilizofichama. Mfano wa tamathali za semi hizo ni dhihaka, kejeli, kijembe, msisitizo bayani na sitiari.

#### 4.2.2.4 Njia za Kuchambua Dhamira Zilizofichama katika Kazi za Fasihi

Utafiti umebaini njia zifuatazo za kuchambua dhamira zilizofichama:

##### 4.2.2.4.1 Kuchambua na Kuhakiki Vipengele vyenye Kutoa Dhamira Zaidi ya Moja

Njia mojawapo ya kuibua dhamira zilizofichama ni kuchambua na kuhakiki vipengele vinavyoweza kutoa maana/dhamira zaidi ya moja. Vipengele hivi ni methali, majina ya wahusika na uhusika wao, vicheko na ucheshi, mandhari, jina la kitabu, uteuzi wa maneno na matumizi ya tamathali za semi kama vilivyokwisha fafanuliwa hapo juu. Vipengele hivi vyenyewe vinajitegemea kutoa dhamira za wazi pamoja na zile zilizofichama.

##### 4.2.2.4.2 Kutumia Muktadha na Mpangilo wa Matukio Yaliyojengwa katika Kazi Husika

Usanii wa kujenga matukio unatofautina kutoka kwa mwandishi mmoja na mwingine. Tukio ni jambo au mkasa ambao ni kiini au chanzo cha mwandishi kilichomshawishi kuandika kazi ya kifasihi. Matukio huweza kupangwa na kupewa mririko maalum, ambayo kifasihi unaitwa ploti. Uhusishaji wa matukio husaidia kujenga maana/dhamira zilizofichama wakati wa uchambuzi wa kazi husika. Mpangilo wa matukio katika usimulizi humsaidia mchambuzi au mhakiki wa kazi ya fasihi kujua uhusiano wa matukio katika hadithi, matukio muhimu yanayofaulisha hadithi na kujua hadithi hii inakusudia kutatua tatizo gani?

Mchambuzi na mhakiki wa kazi ya fasihi, kwa kujua vipengele hivyo hapo juu anaweza kuibua dhamira zilizofichama katika matukio hayo.

#### 4.2.2.4.3 Matumizi ya Nadharia katika Uchambuzi wa Kazi ya Fasihi

Nadharia ni sayansi au sanaa inayohusika na kanuni za kijumla na mikabala fulani au hata kanuni fulani zinazotumiwa katika uchambuzi wa suali fulani (Wamitila, 2003). Kifasihi, nadharia ni mawazo yanayotumika kuwa ni muongozo wa kuchambua au kuhakiki kazi ya kifasihi. Kila nadharia ina misingi yake maalum ambayo ndiyo inayomuongoza mhakiki au mchambuzi wa kazi ya fasihi kuchambua kwa muongozo wa nadharia hiyo. Katika hali hii, kuna misingi inayosaidia kuchambuwa kazi ya fasihi na kuibua dhamira zilizofichama. Kwa mfano nadharia ya U-muundo, nadharia hii inaeleza kuwa ujunzi wa semantiki unapaswa kufasiri lugha ya kimafumbo kama ilivyotumika katika kazi za kifasihi za kitamathali, pia semantiki hutuwezesha kufahamu jinsi lugha isiyokuwa ya mafumbo inavyogeuka na ikawa ya mafumbo. Pia, misingi ya nadharia hii inaeleza kuwa kwa wahakiki wa kimuundo viashirii vina maana na uzito mkubwa kuliko viashiriwa. Hii ina maana gani? Mhakiki wa kimuundo anaelekea kuvutiwa zaidi na jinsi maana inavyozushwa au kukuzwa kuliko na maana yenyewe. Mushengyezi (2003) anaongeza kwa kusema kuwa katika nadharia ya umuundo kuna misingi ambayo hugeuka kuwa chombo cha kujengea maana ya kazi ya fasihi na wakati huo huo inatoa maana ya kifasihi yenyewe. Hii ina maana kuwa lugha katika fasihi ni fumbo lenye kutoa maana ya wazi na maana ya ndani baada ya kuchambuliwa kwa misingi hiyo. Maelezo ya nadharia hii pamoja na misingi kama hiyo huweza kumsaidia mchambuzi wa kazi ya fasihi kupata dhamira zilizowazi na zilizofichama.

### 4.2.3 Dhamira Zilizofichama katika Kazi Teule

Utafiti umegundua kuwepo kwa dhamira zilizofichama katika kazi teule na zimeibuka kupitia vipengele vikuu vitatu, ambavyo ni kupitia methali, nyimbo na vifungu vya maneno vyenye maana ya kimafumbo. Pia kazi hizi zimeathiriwa japo kwa uchache na vipengele kama jina la kitabu majina ya wahusika na vicheko. Vipengele vyote hivi vilichambuliwa kwa kuangalia maana ya jumla na kuhusisha na muktadha uliotumiwa kipengele hicho, ili kuibua dhamira iliyofichama.

#### 4.2.3.1 Dhamira Zilizofichama Kupitia Methali

Methali ni kipengele cha lugha ambacho pia huweza kutumika kama kipengele cha kujengea mtindo wa mwandishi. Hiki ni kipengele maarufu ambacho huweza kusaidia kujenga dhamira zilizofichama katika kazi za kifasihi. Pamoja na kuwa kazi hizi zimetumia methali zenye kutoa maana za wazi zaidi kuliko ile iliyofichama, lakini kutokana na muktadha uliotumiwa kipengele hiki kimesaidia sana kujenga dhamira zilizofichama katika kazi teule kama inavyoonekana hapo chini.

##### 4.2.3.1.1 Riwaya ya *Kuli*

*Kuli* ni riwaya ya pili kutungwa na kuchapishwa miongoni mwa kazi za Shafi Adam Shafi. Riwaya hii, kama zilivyo riwaya zake nyingine, imetumia mtindo wa matukio ya kihistoria, kutumia fasihi simulizi ndani ya fasihi andishi kwa kutumia nyimbo, methali, ametumia mtindo wa barua pamoja na matumizi ya monolojia na diyolojia. Pamoja na uchanga wa mtunzi katika ubunifu wakati akiandika kazi hii, utafiti umebaini kuwa upo upande wa pili wa kazi kutokana na dhamira zilizofichama zinazopatikana katika kazi hii. Miongoni mwa methali zenye kujenga upande wa pili na kutoa dhamira zilizofichama ni hizi zifuatazo:-

i) “Kibaya chako si chema cha mwezako” (uk. 158)

Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo, methali hii, inafasiliwa kwa kuangalia maana dhahiri na maana ya kitamathali. Kwa maana ya dhahiri, hii ni methali inayotoa maadili juu ya mtu kuthamini kitu chake vyovyote kilivyo mbele ya kitu cha mwezake.

Kuhusu maana ya kitamathali, ambayo ndiyo dhamira iliyofichama, methali hii ina mwelekeo wa aina mbili kimaana. Kwanza, inatoa ndoto juu ya kufungwa kwa mhusika Rashidi na kumuachia ujumbe kuwa, huduma zake ndogo kama mume katika nyumba ile si sawa na huduma bora ambazo atafadhiliwa mke wakati yeye mwenyewe yupo gerezani. Methali hii ilitolewa na Amina, mke wa Rashidi, usiku wa siku ya mgomo, siku ambayo Rashidi alikamatwa na kuwekwa gerezani. Familia yake ikabakia kuhudumiwa na viongozi wa chama cha wafanyakazi kwa siku wanazopata nafasi ya kutoa huduma hizo. Dhamira nyingine ni kuwataka Wazanzibar kujua kuwa kujitawala wenyewe hata kama viongozi watakuwa wabaya, ni bora zaidi kuliko kutawaliwa na viongozi walio bora na makini lakini ni wageni (wakoloni). Hali hii inatokana na namna makuli walivyokuwa wakiteswa bandarini na kushindwa hata kusikilizwa juu ya kile wanachokidai kutoka kwa Waingereza.

ii) “Kikulacho kinguoni mwako” ( uk. 49).

Hii ni methali ambayo kwa maana dhahiri, ina maana adui wa mtu ni yule mtu/rafiki anayekujua mipango yako. Methali hii inatoa malalamiko ya Mzee Tindo juu ya Rashidi mtu ambaye amemsaidia kupata kazi na leo ndio anataka kumharibia Mzee Tindo ili aonekane mkorofi mbele ya tajiri wao, Moririji.

Kwa upande wa maana ya kitamathali, methali hii inatoa maana katika mitazamo miwili: kwanza, kuwazindua Wazanzibar kuwa suala la kuwepo ukoloni Zanzibar

linatokana na usaliti wa baadhi ya Wazanzibar kwa maslahi yao, kama Mzee Tindo. Mtazamo wa pili, harakati za kupigania uhuru wa Zanzibar ulikuwa unafanikiwa kupitia msaada wa wakoloni wanaokalia nchi nyingine. Hii ni kutokana na kuwa wakoloni kwa wakoloni wao wenyewe wakisalitiana kwa kuona mwezake anafaidi zaidi kuliko yeye au wivu wa mwezake kubakia katika koloni fulani. Maelezo haya yanakubaliana na msingi wa nadharia ya Umuundo kwa kuonesha maana dhahiri; iliyofasiliwa kama ni maana ya kawaida. Na maana maana ya kitamathali iliyofasiliwa kama ni upande wa methali hii.

iii) "*Let's see who will bell the cate*" (uk. 95).

Hii ni methali ya Kiingereza yenye maana ya "wacha tuangalie nani atamfunga paka kengele" (tafsiri yetu). Methali hii ambayo imetumia lugha ya kigeni imekusudiwa kuwaficha wenyeji waliokwenda kudai haki zao ambao ni Waswahili. Kimsingi maelezo haya ni ya maana iliyodhahiri. Maana za kitamathali ni kama zifuatazo: mosi, Waingereza walitumia methali hii kwa lengo la kuona nani ataanzisha mjadala wa madai  mbele ya watu waliokuja kudai haki zao. Kwa upande wa pili, ina maana harakati za kudai haki na kudai uhuru tayari zinapanda kileleni nani ataanza kujitoa muhanga kwa kuanzisha mapambano dhidi yao. Kwa mtazamo mwingine, wazungu wanajiuliza ni Mzanzibar gani ambaye yuko tayari kujitoa muhanga kwa ajili ya wengine.

#### 4.2.3.1.2 Riwaya ya *Vuta N'kuvute*

Katika riwaya hii, utafiti umebaini kuwa upo upande wa pili wa kazi kutokana na dhamira zilizofichama zinazopatikana. Miongoni mwa methali zinazojenga upande wa pili na kutoa dhamira zilizofichama ni kama zifuatazo:-

i) “Heri nusu ya shari kuliko shari kamili” (uk. 42)

Hii ni methali ambayo kwa maana ya dhahiri imetumika kuonesha namna Yasmin anavyokata tamaa ya kubakia kwao baada ya mama yake kumtukana na kumfukuza. Akaona ni vyema kubakia uswahilini kuliko kubakia kwao na kuendelea na ugomvi ule. Kwa upande wa pili, methali hii imetumika kama kejeli ya kukejeli ugomvi ule wa mama yake Yasmin. Hii ni kwa sababu, kwa hapa, Yasmin hakukubaliana na nusu ya shari kwa kuwa ilikukubaliana nayo ni kurudi kwa mumewe au kubakia pale katika hali ileile. Kaamua kukimbia kwa mumewe na kwao. Na kukimbilia Uswahilini. Kwa Wahindi, hili lilikuwa ni kosa juu ya kosa. Hivyo, methali hii ipo kinyume chake na kuonesha ni heri shari kamili ili kufikia malengo kuliko nusu ya shari na kubakia katika idhilali ya kutokufikia malengo yako. Maelezo haya yanatokana maana ya kitamathali, ambao ni msingi wa kinadharia.

ii) “Yache maji yafuate mkondo na upepo” (uk. 43).

Hii ni methali inayosema “maji hufuata mkondo”, methali hii ina maana kuwa Yasmin aliamua maisha yake yafuate majaliwa aliyopata ya kuishi uswahilini baada ya kufukuzwa kwao na akawa hana pa kwenda. Hii ni maana dhahiri. Kwa upande wa pili, ikichambuliwa kitamathali, methali hii ina mitazamo miwili: kwanza, inaonyesha ujio wa Yasmin katika mazingira ya uswahili si ujio wa makusudio bali imetokea kwa bahati mbaya. Hii ina maana kuwa ukitoa bahati mbaya hakuna Mhindi aliyetayari kuishi na kuchanganyika na Waswahili. Mtazamo wa pili wa methali hii ni kwamba ililenga kumuangalia mjomba yake Yasmin, Gulam, ambaye naye yuko Uswahilini. Huyu alioa mke Mswahili kwa siri bila hata Wahindi wenzake kujua, kama inavyoelezwa ukurasa wa 252. Hivyo Yasmin kuja Uswahilini ni kufuata mkondo.

iii) “Mwisho wa dhiki si dhiki ni faraja” (uk. 43).

Hii ni methali inayosema “Hakuna dhiki wa dhiki baada ya dhiki faraja”. Kwa maana ya dhahiri inamjenga Yasmin kuona kuwa siku moja ataondoka katika dhiki ya kutengwa na jamii yake pamoja na kuisha kwa dhiki anayopata kwa Mwajuma. Kwa upande wa pili katika maana ya kitamathali, methali hii ina mitazamo miwili: Kwanza, bado Yasmin anaamini kuishi Uswahilini ni dhiki na kuamini siku moja atarudi katika jamii yake ya Uhindini. Kama ilivyotekea mwisho kwa kuridhiwa na wazee wake hata kama aliolewa na Mswahili. Katika mtazamo wa pili, methali hii inaonesha namna gani dhiki hizi za ubaguzi zitakavyokwisha Zanzibar pamoja na mila potofu kama za kuozeshwa bila ya idhini ya muolewaji na ile ya muhindi kutoolewa na Mswahili.

iv) “Mzoea punda hapandi farasi” (uk. 207).

Hii ni methali ambayo kwa maana ya dhahiri imetumika kuonesha kuwa mtu akizoea jambo baya anakuwa mzito kufanya jambo jema hata kama njia ipo. Hii yaendana na jinsi Yasmin alivyozoea kuishi katika maisha ya geto na ya kuwa huru kule kwa Mwajuma. Hivyo, Yasmin anashindwa kustahamili kuishi na mumewe na starehe anazopewa kwa madai kuwa anatawishwa na mumewe, Shihab kule Tanga. Kwa upande wa pili, ikiangaliwa methali hii imejengwa kwa fumbo. Inaonesha kuwa Yasmin alikuwa tayari ana mapenzi ya dhati kwa Denge na hata kama Denge alikuwa hayuko tayari kumuoa. Aliona ni bora kuwa karibu yake na kufanya mapenzi nje ya ndoa. Kisiasa, methali hii inawakejeli Waswahili kwa kuonesha kuwa ni watu waliozoea kutawaliwa na hivyo hawawezi kujitawala wenyewe. Wazungu nao wamezoea kudhalilisha Waafrika kwa kuwatawala na kuwafanya watumwa, hivyo ni vigumu kuyachia makoloni yao na kwenda kuishi kwao.

v) “Mwangaza mbili, moja humponya” (uk. 230)

Hii ni methali ambayo katika maana ya dhahiri inaonesha namna gani Yasmin alivyopoteza fursa ya ndoa yake na Shihab na kumkimbilia mpenzi wake, Denge. Wakati Denge mwenyewe alikuwa tayari ameshakamatwa na kuwekwa gerezani. Hivyo, amekosa ndoa ya Shihab na kumkosa mpenzi wake, Denge. Kwa upande wa pili, methali hii inafafanua uhalisi wa Yasmin kwa Denge. Yasmin alikuwa akimtaka Denge na hakuwa mwanaharakati wa kupigania uhuru wa Zanzibar. Hatima yake, ili ampate Denge ilimbidi aingie katika siasa, lakini alifanikiwa katika siasa na kukosa mapenzi ya Denge. Maelezo haya yanatiwa nguvu na msingi wa Umuundo kwa kutafasiri fumbo lilojengeka katika maelezo ya methali hii.

vi) "Nazi haiwezi kushindana na jiwe" (uk. 251)

Kwa maana ya dhahiri, methali hii, imetumika kwa lengo la kuadilisha jamii na kuonesha kuwa mtu hawezi kuishi vizuri bila ya kuridhiana na kuishi vizuri na wazee wake. Inaonesha kuwa Yasmin hawezi kuishi bila ya kufahamiana na kuridhiana na wazee wake. Hivyo, anaamua kurudia na kuomba radhi kwa wazee wake. Kimsingi methali hii, ni fumbo ambalo lina mitazamo miwili: Kwanza, ni kushindwa kwa Yasmin kuishi Uswahilini na hivyo kuamua kurudi katika mazingira na maisha ya Uhindini. Yasmin alijiona ni nazi mbele ya wazazi wake ambao ni kama jiwe. Pili, methali hii ina maana ya kisiasa na kutoa mitazamo miwili: Wa kwanza, wakoloni kupewa taswira ya jiwe: Hivyo, Wazinzibar kushindwa kufikia lengo la ukombozi na mhusika Denge kukimbilia nje ya Zanzibar. Mtazamo wa pili unahusu bishara kwa Wazanzibar ya kuwa, kwa hali moja au nyingine, wakoloni iko siku wataondoka Zanzibar ikiwa kwa hiyari au kwa nguvu. Hii ni kwa sababu wao ni kama nazi na Wazanzibar ni jiwe.

vii) "Asiyekubali kushindwa si mshindani" (uk. 271)

Hii ni methali ambayo kwa maana ya dhahiri ilitumika kumtia moyo Denge na kumliwaza baada ya kushindwa kufikia lengo la kuwatoa wakoloni wa Kiingereza Zanzibar. Alitakiwa ajione bado ni mpambanaji hata kama kashindwa. Kwa upande wa pili, methali hii ina mitazamo miwili: Kwanza, inatoa kauli ya jamii kukubali kushindwa kupigania uhuru wao baada ya wakoloni kutumia nguvu na kuwaweka magerezani wapigania uhuru wa taifa hili. Denge anaiona kauli hii kuwa ni ya kejeli na kupingana nayo kwa kutoa kauli kuwa "Hatukushindwa mapambano bado yanaendelea, vuta nikuvute sisi au wao" (uk. 272). Mtazamo wa pili unaonesha ishara ya ushindi kwa jamii ya Zanzibar kwa kufanikiwa kumtorosha Denge kutoka gerezani. Kutokana na hali hii methali inawataka wakoloni wakubali kushindwa kwa kushindwa kumdhibiti mtu aliye mikononi (gerezani) mwao ambaye ni Denge.

#### 4.2.3.1.3 Riwaya ya *Haini*

Katika riwaya hii, utafiti umebaini kuwa upo upande wa pili wa kifasihi kutokana na dhamira zilizofichama. Miongoni mwa mambo yanayojenga upande wa pili na kutoa dhamira zilizofichama ni kama yafuatazo:-

i) "Dua la kuku halimpati mwewe." (uk. 46)

Hii ni methali yenye maana kuwa masingamizo na masononeko ya mtu wa kawaida haziwezi kumkuta mtu aliyejuu kihadhi au kiuongozi. Katika nadharia ya Umuundo tafasiri hii ni ya maana dhahiri. Pia, methali hii ina maana ya kitamathali ambayo inajenga dhamira iliyofichama kama inavyoweza kufafanuliwa: Hii inaonesha namna gani jamii inavyoweza kukata tamaa na maisha juu ya kutafuta au kupigania haki yao, kama alivyochorwa Hamza kwa kutoa maelezo haya ambayo yanaonesha kuvunjika moyo na jambo lolote katika kupigania haki yake.

ii) “Nguo ya kuazima haistiri matako” (uk. 85)

Hii ni methali ambayo katika mazingira mengine inajulikana kama “nguo ya kuazima haiendewi ngoma.” Katika maana dhahiri methali hii, ina maana kuwa kitu ambacho hakipo katika miliki yako si cha kutegemea. Kama ambavyo Hamza kaitumia kuonesha namna gani nguo ambazo kaazimwa anavyokuwa hana amri nazo. Kwa upande wa pili, methali hii ina maana kuwa pamoja na kupata uhuru wa taifa lao, uhuru huu ni wa bandia: yaani, kubakia katika ukoloni mambo leo. Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo hili ni methali yenye kutoa maana ya kitamathali na kujenga fumbo. Hivyo, kuna mambo mengi kama vile masuali ya kisheria, na ugawanyaji wa madaraka bado hayatoi haki kwa watu wachini na wao wanashindwa na njia ya kutatua hili. Hali hii ndiyo inayosononesha jamii, serikali ipo kwa ajili ya mamlaka ya watu wachache na wenye kudhalilisha jamii.

iii) “Heri hupatikana ndani ya tumbo la shari” (uk. 89)

Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo, maana dhahiri ya methali hii inaonesha kuwa jambo lolote jema haliwezi kufika bila ya kupata vikwanzo na kupitia shida mbali mbali. Methali hii imetumika kuonesha kuwa kuna wanajamii wengi ambao waliridhika kutokea kwa mapinduzi ya Zanzibar. Hali hii ilitokana na mateso waliyokuwa wakiyapata katika utawala wa waarabu na ukoloni wa waingereza, pamoja na dhiki za maisha walizokuwa wakipambana nazo. Kwa upande wa maana ya kitamathali, methali hii inaonesha jinsi gani watu wasivyopendelea matokeo na matendo yaliyofanywa na watendaji wa serikali baada ya mapinduzi. Chambilecho mwandishi[3] kuwa kuuwawa kwa Kigogo ilikuwa ni shari ambayo ilitegemewa kuzaa heri kwa jamii. Kwamba Mh. Karume alikuwa na sera na lengo zuri katika serikali

[3] Mahojiano yaliyofanyika kati ya mwandishi Shafi Adam Shafi na mtafiti yaliyofanyika nyumbani kwake Bunju tarehe 27/ 2/ 2015

yake ya Mapinduzi, lakini watendaji wake bado walikuwa wagumu. Wengine, hasa usalama, walipewa madaraka makubwa na kuyatumia vibaya kwa jamii. Hii ndiyo dhamira iliyofichama.

iv) " Sheria ya chui ndani ya zizi la mbuzi" (uk. 137).

Huu ni msemo ambao kwa nadharia ya Umuundo unajenga fumbo. Linaonesha namna gani jamii hii ilikosa kufuata sheria na kubakia na sheria ya kutumia nguvu kwa mwenye mamlaka ya kufanya hivyo bila ya kujali wanyonge. Kw upande wa pili, usemi huu unaonesha utabaka katika jamii juu ya matumizi ya sheria. Inaonesha kuwa sheria ni kwa ajili ya kuwakandamiza watu wa chini walionasibishwa na mbuzi, na kuwalinda watu walio juu walionasibishwa na chui. Hii ndiyo sababu hata wakubwa waliotuhumiwa kuhusika na uhaini kama kanali Bunju hawakukamatwa kwa sababu ya uchui wao; na wasiohusika na kesi hii kama akina Hamza ndio wanaoteseka kwa sababu ya umbuzi wao.

#### 4.2.3.2 Dhamira Zilizofichama Kupitia Nyimbo

##### 4.2.3.2.1 Riwaya ya *Kuli*

i. Usilie usilie,
Ukaniliza na mie
Machozi yako yaweke
nikifa unililie. (uk. 4)

Huu ni wimbo wa kubembelezea watoto. Katika hali ya kawaida wimbo huu unadhima ya kumchombeza mtoto asilie. Pia wimbo huu una maana ambayo hutoa dhamira fulani kwa jamii. Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo, wimbo huu una maana dhahiri na maana ya kitamathali. Utafiti umebaini maana zifuatazo: Maana ya kawaida ni kwamba usifanye jambo ambalo halijafikiwa na wakati muwafaka ila usubiri mpaka

litakapofikiwa na wakati wake. Maana iliyofichama: Ni kwamba wimbo huu unaonesha nafasi ya mama juu ya mapenzi ya watoto wake kwa kuwaonesha huruma ya hali ya juu na kutopendelea kuona wanakutwa na baya la aina yoyote lile. Kimaadili, mtoto anatakiwa asikate tamaa na mapambano ya aina yoyote yale hasa akiwa yupo chini ya ushauri na maelekezo ya wazee au viongozi wake. Maana nyingine: Ni kwamba wazee ni watu wenye kupambana katika kujenga msingi bora wa maisha ya watoto wao kwa juhudi kubwa. Hivyo wanaposhindwa kufikia malengo, watoto hawapaswi kuonyesha udhaifu wa wazee wao ili wasije wakawatia unyonge kwa udhaifu huo.

ii. Mapenzi yamenisibu,
ghafla usingizini,
nimepanda kitu ghali,
hakiuzwi madukani,
ningelipoteza mali,
hakitia mikononi (uk. 121).

Huu ni wimbo ulioimbwa na mlevi, lengo ni kutoa hisia zake za ndani ambazo zinamkereketa. Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo, wimbo huu usio na lugha ya mafumbo una geuka na kuwa na mafumbo ambayo yanatoa maana zifuatazo: Kwa upande mmoja wimbo huu unatoa hisia juu ya mapenzi ya Rashidi na Amina. Rashidi anaonesha thamani ya mapenzi kuwa si kitu ambacho huuzwa madukani au hugawiwa msikitini bali ni imani kutoka moyoni mwa mpendaji. Kwa upande wa pili, kuna dhamira iliyofichama ambayo ni kuonesha namna wanaharakati wa kupigania uhuru walivyoibuka katika ujahili na kuanza kupenda na kuwa wazalendo wa nchi yao. Mapenzi haya yamewafanya kudai haki zao katika kazi na kudai uhuru wa nchi yao kwa jumla.

#### 4.2.3.2.2 Riwaya ya *Vuta N'kuvute*

i) Jamani ujana, unanitoroka,
Mfano wa jua, linapotoweka,
Sasa wako wapi, walionitaka,
Uzuri hakika, kitu cha kukopa,
Hakika ni kweli, nilibahashuka,
Kuringia kitu, kisicho enzika,
Mithili ya ua, ukishalikata
Uzuri hakika, kitu cha kukopa (uk. 85 – 86).

Huu ni wimbo ambao uliimbwa na Mwajuma katika maruwe ruwe ya ulevi. Wimbo huu unajengwa na maana dhahiri na maana ya kitamathali. Kwa maana ya dhahiri wimbo huu ni wa kimaadili ukijaribu kuwaasa vijana kutoringa kwa sababu ya uzuri katika ujana wao, kwani ni hatua ya kupita kama mtu alivyopitia katika utoto wake. Kwa upande wa pili, wimbo huu unaweza kuangaliwa kisiasa, wakati wakoloni walipoingia kwa hatua yao ya kwanza watu waliwakubali na kufurahia huduma zao. Baada ya kuchosha na kuringia uzuri katika uongozi wao na kujisahau kwao, sasa kila mtu anawachukia na kutaka waondoke. Hali hii hutokezea kwa kila kiongozi katika jamii na hata kiongozi wa familia. Hizi ni maana za kitamathali.

ii) Wache waseme,
Sina budi naye,
Si hofu lawama,
Sababu ya yeye … (uk. 212).

Huu ni wimbo ambao umetolewa na mlevi; kwa mazingira uliyotolewa, huweza kuonekana hauna dhamira yoyote ispokuwa kuburudisha tu. Lakini kwa upande wa pili, wimbo huu huweza kutoa maana ya kitamathali juu ya siasa na jamii. Kwa upande wa kijamii, ni wimbo unaolenga mapenzi na kuonesha namna gani mtu yuko tayari

kubeba lawama kwa sababu ya mwanamke. Kwa upande wa kisiasa, wimbo huu una maana kuwa, kwa wale wapiganaji wako tayari kupigania uhuru kwa hali yoyote bila ya kuhofia kufungwa, kupingwa au hata kudhalilishwa kwa njia yoyote. Hizi ni dhamira zilizofichama katika wimbo huu.

#### 4.2.3.2.3 Riwaya ya *Haini*

Pamoja na kutumia matukio ya kihistoria katika kazi hii, pia mwandishi kasheheneza nyimbo hasa zilizoimbwa na mahaini gerezani ikiwa pamoja na kubembelezea watoto walioachwa na mahaini hao kwenye familia zao. Miongoni mwa nyimbo hizi ni:-

i) Msegeju ana ng'ombe
Nami nna ng'ombe zangu
Namwambia tuchanganye hataki,
Kwa heri nakwenda zangu. (uk. 58).

Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo wimbo huu unatoa fumbo. Utafiti ulibaini kuwa, wimbo huu unahimiza juu ya suala la ushirikiano katika jamii. Kwa upande mwingine, wimbo huu unatoa historia ya muugano wa Zanzibar na Tanganyika. Muungano uliokuwa na lengo la kuunganisha Afrika ya Mashariki na ikiwezekana Afrika yote kwa jumla. Lakini lengo hilo halikufikiwa na Zanzibar na Tanganyika wakaamua kubakia na muungano huo kama nchi moja hadi leo.

ii) Wajomba wamechacha, wamekuja juu harusini,
Wapi mahari mbona sisi hatujapata (uk. 109).

Wimbo huu una maana ya dhahiri na maana ya kitamthali. Maana dhahiri, unaangalia tabia ya jamii hasa katika masuala ya ndoa. Jamii hasa ya Zanzibar inapoozesha inakuwa inategemea kufaidika kutokana na mahari yanayotolewa kwa ajili ya mke. Kwa upande wa pili, maana ya kitamathli inaonesha namna ya mazingira ya baada ya mapinduzi yalivyokuwa Zanzibar. Wanamapinduzi walikuja juu kuona kuwa nao

wanataka kufaidika na matunda ya mapinduzi yale. Suala hili lilisababisha kuota kwa mizizi ya ubaguzi, hasa wa kisiwa kimoja hadi chengine. Hii ni kwa sababu madaraka yalihodhiwa na watu wa kisiwa fulani na kisiwa fulani hawakufaidika na mapinduzi hayo. Pia, kuna wanamapinduzi ambao walitegemea kupata madaraka baada ya kazi nzito waliyoifanya lakini hawakupata kitu na kujenga fitina katika serikali hii na hadi kufikia kuitwa kuwa ni makomred.

iii) Heshima kijana tanguliza kwanza mbele,
Ujeuri mbaya ohoo,
Uzuri si hoja, tabia njema ni silaha,
Utapendwa kokote ohoo (uk.114).

Huu ni wimbo ambao unazungumzia maadili juu ya kuwa na tabia njema katika jamii, kwa kusisitiza heshima na kuwa na tabia njema na kuonya juu ya ujeuri na kuringia uzuri. Kwa upande mwingine, wimbo huu unazungumzia juu ya uongozi na sifa za kumfanya mtu kuwa kiongozi bora, kama vile kuwaheshimu raia zake kwa kuzingatia haki zao, na kuwa na tabia njema juu yao. Pia, kuachana na jeuri ndio silaha za kumlinda kiongozi yoyote na sio kuwa na jeshi imara katika serikali. Maelezo haya yanathibitishwa na msingi wa nadharia ya Umuundo katika kuchambua maana dhahiri na maana ya kitamathali. Kwa kuihusha katika kazi, imeonekana kwa mhusika Kigogo pamoja na kuwa na ulizi imara lakini kwa sababu ya kasoro zake kwa jamii yake kashindwa kuwa na silaha imara, matokeo yake wale askari wake ndio walioshiriki katika kumuua.

iv) Lipochuka mimba,
Tabu na mashaka yangu,
Usiku kucha silali,
Nawania roho yangu,
Nambiwa mwana si wangu,
Mwana ni wa muume wangu (uk. 144).

Wimbo huu wa kubembelezea mtoto una maana dhahiri na maana ya kitamathali kama zilivyogawiwa na nadharia ya Umuundo. Kwanza unatoa maana kwa jamii juu ya dhiki na mashaka anayopata mama wakati anapokuwa mjamzito. Na baada ya dhiki zote hizi manufaa ya mtoto anayapata baba kuliko hata mama, pia baba ana hadhi kubwa mbele ya mtoto ukilinganisha na mama. Jina la mtoto hunasibishwa na jina la baba na sio la mama. Hii ni maana ya dhahiri, kwa upande wa maana ya kitamathali. Wimbo huu unatoa maana ya kisiasa kwa kuonesha namna gani wasomi walivyoshiriki katika harakati za kupigania uhuru. Kuelezea mwanzo wa kupambana na wakoloni wa Kiingereza kama akina Denge katika *Vuta N'kuvute*. Pia kupinduliwa serikali kama ilivyooneshwa katika riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuadi*. Matokeo ya yote hayo ni kusalitiwa kwa wanaharakati hao na serikali kuambiwa ni ya wakwezi na wakulima. Hivyo, madaraka kama ya mahakamani walipewa wauza samaki na maziwa. Mhusika Faraji, ambaye ni mwanasheria *Kuli* anaonekana kuasisi harakati kwa kuendesha vyama vya wafanyakazi. Hata hivyo aliachwa nje ya serikali, na baada ya kuuliwa Kigogo anatuhumiwa kama ni haini.

v) Kile kidau kijacho,
Hamkosi mnachangu,
Mna mkufu ni tunge,
Kadri ya shingo yangu,
Hupata si uvai,
Wala simpi mwezangu,
Nenda mpa mama yangu,
Msiri wa mambo yangu (uk. 144)

Huu ni wimbo wa kubembelezea watoto. Unatoa maana dhahiri na dhamira juu ya umuhimu wa mama anavyothaminiwa na mtoto wake wa kike kama ni msiri mkubwa juu ya mambo yake ya kijamii, kiutamaduni na hata kiuchumi. Kwa upande wa pili, wimbo huu ni fumbo ambalo linaonesha hali baada ya mapinduzi na harakati za

muungano. Mkufu unaweza kutafsirika kama ni Zanzibar na mama yangu ni Tanganyika ambako ndiko kukeni kwa Wazanzibar. Hivyo, wimbo huu ulikuwa unaelezea namna Zanzibar ilivyofanikiwa kupata uhuru na baada ya kupata uhuru huo bila hata ya kufikiri mara mbili wakajiunga na Muungano na Tanganyika ili kupata hifadhi dhidi ya maadui.

vi) Kombo we Kombo,
Kanipe mapesa yangu,
Kilichonitoa nyumba,
Wivu wa mke mwezangu,
Kahamia kianga Mselemu (uk. 227).

Wimbo huu una maana dhahiri na maana ya kitamathali. Maana dhahiri inalenga jamii katika suala la ndoa, hasa ndoa za mke zaidi ya mmoja. Ndoa hizi zinakuwa na kuoneana wivu unaoweza kusababisha migogoro ndani ya ndoa hadi mmoja wao kuachwa. Kwa upande mwingine, wimbo huu una maana ya kisiasa kwa kuonesha ni sababu ipi ilisababisha kufanyika kwa mapinduzi ya Zanzibar. Uhuru kutoka kwa Waingerza ulipatikana 1963 na mapinduzi yalifanyika 1964. Kwa mujibu wa nadharia ya Marx, uchambuzi wa kazi utazingatia tajiriba ya watu kimaisha, kisiasa, kiuchumi na mjengeko wa jamii yao. Mapuri (1996) anaeleza kuwa ni jambo lisiloyumkinika kwa Waafrika kwa visiwa vya Zanzibar ambavyo vina maili 45 kutoka bara la Afrika na elfu ya maili kutoka kutoka bara Arabu, na Warabu waijenge Zanzibar kama ni dola ya Kiarabu. Kutokana na wivu huu, ikasababisha ASP kufanya mapinduzi ili kuondoa mamlaka ya Sultani ndani ya Zanzibar.

#### 4.2.3.3 Dhamira Zilizofichama kupitia Vifungu vya Maneno yenye Maana ya Kimafumbo

##### 4.2.3.3.1 Riwaya ya *Kuli*

Kuli ni kazi iliyotumia mtindo wa kujenga maneno, sentensi na hata aya katika mfumo wa kimafumbo. Hali hii inaweza kumsaidia mhakiki na mchambuzi wa kazi hii kuibua dhamira zilizofichama. Kama zinavyofafanuliwa hapo chini:

i) Anayefahamiana na yule Mhindi anayegawa vile vipande anaweza kukipata kipande kwa urahisi. Mhindi huyo anawaelewa wale wenye nguvu na walio wahodari kwa kazi za uchukuzi.

Haya ni maelezo yanayojitosheleza kimaana kama yanavyosomeka. Ikiangaliwa maelezo haya kwa kuzingatia msingi wa nadharia ya Umuundo maelezo haya yanatoa fumbo ambalo linatoa upande wa pili kimaana. Maneno kama vile: Mhindi, kufahamiana, nguvu na uhodari yanatoa fumbo na kusaidia kutoa dhamira zilizofichama katika maelezo haya. Maelezo haya yana maana kuwa Wahindi na watu wengine weupe ndio waliokuwa mabepari huku wenyeji wakiwa watumiaji wa nguvu zao tu. Kazi zilikuwa zikitolewa kwa kujuana na hata kutumika rushwa katika kupata kazi hizo. Pia, Wazanzibar walikuwa wakithaminiwa wakati wakiwa na nguvu na uwezo wa kufanya kazi. Na hiki ni miongoni mwa kigezo kilichotumika katika kuwachukua watu na kuwatia katika utumwa.

ii) Kazi? Kazi gani? Hizo kazi zilizopo hapa zinakushinda! Leo maji hukuteka mitungi yote mikavu na unajua vizuri kwamba siku hizi serekali inafunga maji kutwa (uk. 21)

Kupita nadharia ya Umuundo tunapata maana dhahiri inayotoa maelezo yanayoonesha wasiwasi wa mama yake Rashidi kwa kumuona Rashidi bado hajamudu kufanya kazi za nje. Kwa upande mwingine, tukichambua fumbo kupitia vipengele vya kisemantiki, hasa matumizi ya mafungu ya maneno; "Kazi gani?, zilizopo hapa zinakushinda, serekali inafunga maji", yanatoa fumbo na kusaidia kutoa dhamira zilizofichama katika maelezo haya. Kwanza, mama yake Rashidi anaidharau kazi anayotaka kufanya Rashidi kwa kuiona haina thamani. Pia, analalamika juu ya serikali kwa kuwa na huduma mbovu kwa jamii. Kwa mujibu wa nadharia ya Umarx, uchambuzi wa kazi utazingatia tajiriba ya watu ya kimaisha, kisiasa, kiuchumi pamoja na mjengeko wa jamii yao. Kwa msingi huu, utafiti umebaini maana ya kiutamaduni, jamii ya Zanzibar huwapima vijana wake juu ya uwezo wa kufanya jambo kwa kuanza kutoa huduma za nyumbani. Kwa mfano, mwanamke hupimwa uwezo wa kuwa tayari kuolewa kwa kupewa majukumu ya nyumbani kwao kama kupika na kutunza nyumba. Mwanamme hupimwa uwezo wa kuongoza nyumba yake kwa kupewa majukumu ya nyumbani kwao kuyatekeleza, kama kulisha nyumba na huduma nyingine. Hivyo, uwezo wa Rashidi kuweza kufanya kazi ni kumudu kufanya kazi za nyumbani kwao.

iii) Si aghalabu kwa Morarji kupewa shauri na Mzee Tindo akakataa kwani kila shauri alilolitoa Mzee huyo lilikuwa ni la manufaa kwa tajiri huyo. Alikuwa ni mfanyakzi aliyeaminiwa sana na Morirji na kupata fursa nyingi za chini chini ambazo wezake walikuwa hawazipati. (uk. 28).

Haya ni maelezo ya kawaida ambayo yanaonesha uaminifu wa Mzee Tindo kwa tajiri wao Morirji. Kwa kupitia nadharia ya Umuundo, maelezo haya yanajenga fumbo na kupata fursa ya kuchambua semantiki ya maneno, kama "kila shauri kuwa na manufaa, kupata fursa za chini chini, wezake hawazipati" huweza kuwa fumbo na kutoa maana

zifautazo: Kwanza, Mzee Tindo alikuwa ni msaliti kwa wezake. Shauri analotoa ni la manufaa ya Wahindi au ni la kuwafitini wezake, hasa wanapotaka kudai haki zao au kufanya la maendeleo kwao. Pili, Mzee Tindo alikuwa anachukua rushwa kwa lengo la kuwa kibaraka cha mabepari na kuendeleza ukoloni kwa jamii yake.

iv) Yale mawingu mekundu yaliyochanganyika na mawingu ya rangi ya kijivu jivu yalianza kupotea na jua lilikuwa limekwisha anza kutoa ndimi zake kutokea upande wa mashariki

Maelezo haya yanatoa maana dhahiri na maana ya kitamathali, kama ilivyoelezwa katika nadharia ya Umuundo. Maana dhahiri: inamaanisha kuwa usiku unakucha na jua linachomoza upande wa mashariki. Kwa upande wa pili, maelezo haya yana maneno au vifungu vya maneno ambavyo kisemantiki vinajenga mafumbo na kutoa dhamira iliyofichama. Maneno au vifungu vya maneno hayo ni: mawingu, mekundu, kijivu jivu, jua, na ndimi. Maneno haya huweza kubeba maana zifuatazo: mawingu mekundu ni Waingereza, mawingu ya rangi ya kijivu jivu ni vibaraka wa Waingereza. Hawa ni wenyeji wa Zanzibar ambao pamoja na weusi wao hujinasibu na weupe; hivyo, kukosa sifa ya weupe na ile ya weusi na kubakia kijivu jivu. Jua ni muamko wa jamii na ndimi ni madai juu ya udhalilishaji na ukandamizaji wa wakoloni. Kwa jumla, maelezo haya kwa kuzingatia nadharia ya Umarx, kuwa uchambuzi wa kazi unazingatia tajiriba ya kimaisha. Utafiti umebaini kuwa maana ya maneno haya ni Wakoloni wa Kingereza na vibaraka wao wameanza kwisha nguvu kutokana na muamko na sauti za uhuru wa jamii ya watu wa Afrika ya Mashariki.

v) Wanaume wote husema vivyo hivyo, hutoa kila ahadi wanapotaka lakini inapodhihiri kweli huruka huko (uk. 112).

Maelezo haya yana maana dhahiri na maana ya kitamithi. kwa upande mmoja yana maana dhahiri juu ya kuwatuhumu wanaume wanaowadanganya wanawake baadaye wakawaacha bila ya kuwaowa hasa wanapopata ujauzito au kutekelezewa haja zao. Kwa upande maana ya kitamathali, maelezo haya yanajenga fumbo na kutoa dhamira iliyofichama kwa kuonesha namna gani wakoloni walipoingia mwanzo walivyokuwa wenye maneno ya busara na wenye kutoa misaada na ahadi mbalimbali. Baada ya kuotesha mizizi, walisahau wema na ahadi zao zote. Walifanya dharau, kejeli, kuwetesa wenyeji, kuwapa kazi ngumu zisizo maslahi na kuzipora mali za wenyeji wao.

vi) Mrefu, pua imenyooka na macho yake yalikuwa yanang'ara kama ya paka (uk. 91)

Katika sentensi hii, tunapata tashibiha "macho yanang'ra kama ya paka" katika tashibaha hii tunapata maana tofauti. Maana ya kwanza ambayo ni maana ya juu ni kuyanasibisha macho ya mtu na ya paka kutokana na mng'aro wa macho ya mhusika huyu. Kwa maana iliyofichama, mtu huyu ananasibishwa na paka moja kwa moja kwa kulinganishwa na vitendo vya paka. Paka anapoingia sehemu ni lazima amtawale panya. Sentensi hii ya kitashibiha ni ya kuwalinganisha Waingereza na paka mbele ya Wazanzibar ambao huweza kulinganishwa na panya walioingiliwa na paka. Kupitia nadharia ya Umarx, kuwa uchambuzi wa kazi utazingatia tajiriba ya watu ya maisha. Hivyo, Waingereza wamenasibishwa na Paka kwa sababu ni mnyama anayejipenda, ukimfuga ni mnyama anayependa ustarabu, anajisaidia kisha anafukia, anapenda kulala katika kitanda cha bwana wake. Hata hivyo kama hatatekelezewa kula yake kama vile maziwa, samaki, nyama na vitu vizuri ataanza kuiba na kukukera ndani kama walivyofanya Waingereza Zanzibar.

vii) “We kalb wee! Weye nashkua kibati mara mbili kwa kikabu moya” (uk. 15)

Sentesi hii imetumia neno la Kirabu “kelb” lenye maana ya mbwa. Hii ni sentensi inayoonesha athari ya ushihiri katika matumishi ya lugha ya Kiswahili. Kwa mfano neno moya lenye maana ya moja, nashkua lenye maana ya unachukua na kikabu lenye maana ya kikapu. Kwa upande wa kwanza, sentesni hii ina maana ya tusi ambalo tajiri anawatukana wafanyakazi wake kwa kuwaita mbwa. Hili ni tusi maarufu ndani ya mazingira ya Zanzibar kwa kutumia neno hili hili la “kelbu”. Kwa upande wa pili, sentensi hii inaonesha namna gani Waraabu, Wazungu na wakoloni wengine wanavyomiliki utajiri na kuwatumia wenyeji wa nchi za Kiafrika zilizokuwa zikitawaliwa. Pia, neno kelbu linaonesha hadhi ya wenyeji ambao walionekana kama ni mbwa na wasio na thamani yoyote isipokuwa ni kutumikishwa na bwana wake kwa tija ya kula ya wakati mmoja basi.

#### 4.2.3.3.2 Riwaya ya *Vuta N’kuvute*

*Vuta N’kuvute* nayo ni kazi iliyojengwa kwa maneno, sentensi au aya katika hali ya kimafumbo. Mafumbo haya yanamsaidia mhakiki na mchambuzi wa kazi hii kuibua dhamira zilizofichama kama zinavyoelezwa katika utafiti huu hapo chini:

i) Umbile hilo na ile rangi yake ya maji ya kunde lilimfanya aonekane kama morani wa kimasai (uk. 47).

Maelezo haya ni ya kawaida ambayo yalikuwa yakitowa wasifu wa Denge. Maneno kama “rangi yake ya maji ya kunde” na “morani wa kimasai”, kisemantiki, yanajenga fumbo na kutoa upande wa pili kimaana. Maelezo haya yanatokana na msingi wa nadharia ya Umuundo, lugha isiyokuwa ya mafumbo imegeuzwa kuwa ya kimafumbo. Kwa hali hiyo; rangi ya maji ya kunde inatoa maana kuwa ni mtu aliyechanganya damu ya Uarabu na Uswahili, hivyo kuthibitisha kuwa Denge ni Mzanzibar halisi. Pili,

maneno “morani wa kimasai” yanatudokeza ushajaa wake katika kupigania uhuru wa Zanzibar kama alivyoonekana katika kazi hii.

ii) Hatukushindwa mapambano bado yanaendelea, vuta nikuvute sisi au wao (uk. 272).

Kwa upande mmoja, maelezo haya ni yenye maana dhahiri. Maneno ya kujitia moyo kwa wapigania uhuru na kuonesha bado wanaendelea na mapambano na wakoloni wanatawala wa jamii yao. Kwa upande wa maana ya kitamthiliya, maelezo haya yanatoa suluhisho la kitabu hiki na kuonesha kuwa kimeibua hatua mpya kwa wapiganaji kwenda kujipanga na kutafuta nguvu mpya. Kulingana na mtiririko wa visa katika kazi za mwandishi huyu, kisa hiki kimeungwa na kisa cha *Kasiri ya Mwinyi Fuadi.* Hata kama *Kasri ya Mwinyi Fuadi* ni kazi ya kwanza kutungwa, lakini ni kazi ya tatu kimpangilio wa visa. Kwa mpangilio wa visa, kitabu cha kwanza ni *Kuli*, cha pili ni *Vuta N’kuvute*, cha tatu ni *Kasri ya Mwinyi Fuadi* na cha nne ni *Hain*i ambayo ina kisa cha baada ya uhuru. Hivyo, mapambano ya vuta n’kuvute yamekuja kuendelezwa katika kazi ya *Kasri ya Mwinyi Fuad*.

iii) Palitokea mlipuko mdogo wa moto wa rangi ya kibuluu na moto ule uliunguza tende ile kidogo kidogo mpaka ilipokauka na moto ukazimika. Unaona mambo hayo nimemwambia mie kwamba mali ya Mzee Kiroboto peke yake. (uk. 26).

Maelezo haya ni yenye maana ya kawaida. Kwa msingi wa nadharia ya Umuundo ina maana dhahiri na maana ya kitamathali. Maana dhahiri inaonesha na kuisifu tende ya Mzee Kiroboto kuwa ni kali kiasi cha kuwasha moto kama mafuta. Kwa upande wa maana ya kitamthiliya, maelezo haya yanaonyesha athari ya pombe kali kwa afya ya binadamu. Mwandishi kaonesha tende namna inavyowaka baada ya kuwashwa. Lengo

hapa ni kuitaka jamii kutafakari kama pombe hii ina ukali na kuwa kama hivi, ni kiasi gani inavyoweza kumuathiri mtu anayekunywa. Mwandishi anaonesha athari ya pombe kwa jamii. Jambo ambalo lilionekana ni la kawaida na kuzoeleka na jamii zetu.

#### 4.2.3.3.3 Riwaya ya *Haini*

Haini ni kazi ambayo imetumia mtindo wa kutumia maneno, sentensi na aya ambazo huweza kutoa mafumbo kwa wahakiki na wachambuzi. Hivyo kuwasaidia katika kuibua dhamira zilizofichama kama zinavyooneshwa na utafiti huu hapo chini:

i) *Pudding* ile waliiona kama msafiri wa jangwani anaposhikwa na kiu akaona dibwi la maji mbele yake na atakapo kuyachota akaona amechota gao la mchanga, ni mazigaziga tu ya mdanganya macho yake. Hivyo ndivyo ilivyo kuwa pudding ile iliyopikwa na Shadidi chumbani mle. Bado wanasononeka na njaa. (uk. 28).

Haya ni maelezo yanayoonesha namna gani gerezani watu wanavyotamani vitu vitamu na kuviandaa kwa mdomo, kuvila moyoni na kuvitamani bila ya uhalisi wenyewe kuwepo. Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo, maelezo haya yanajenga fumbo. Utafiti ulibaini kuwa, maelezo haya yana dhamira iliyofichika kwa kufumbuliwa fumbo linalopatikana kwayo. Maelezo haya yanaonesha uhalisi wa mapambano ya kuondoa ukoloni na hatima yake. Jamii ilitegemea baada ya mapinduzi itakuwa ni kula *pudding* iliyopikwa kwa kupitia mapinduzi hayo lakini kinachoonekana ni mateso na idhilali kama au kuliko zile za nyakati za kikoloni. Na kwa mujibu wa nadharia ya Marx, uchambuzi wa kazi unazingatia tajiriba ya watu ya kimaisha. Hivyo tunaona kuwa matumini ya maendeleo kwa jamii baada ya mapinduzi yalibakia kuwa ni mazigaziga (kutamani) tu na sio uhalisi wenyewe.

ii) Mmeyazika wapi? Mtumwa ni mtumwa tu na muungwana ni muungwana tu. Hamna chochote mlichokizika, usijidanganye bure? (uk. 29).

Kupitia nadharia ya Umarx, msingi unaeleza kuwa fasihi huonesha imani za jamii, muundo wa jamii na changamoto ili kukuza na kuonesha imani za wafanyakazi na watumishi wengine. Msingi huu unasaidia kueleza kuwa bado katika jamii kuna watu waliobakia na hadhi ya utumwa na wale wenye hadhi ya uungwana, na bado hayajamalizika. Upande wa pili, wa maana ya maelezo haya yanaonesha kuwa mapinduzi ya Zanzibar ya 1964 hayakufikia lengo la kuondosha utumwa na uungwana. Hii ni kutokana na ukweli kwamba hao walioshikilia madaraka wamegeuka kuwa waungwana na wale waliopindua na jamii kwa jumla imebakia katika utumwa.

iii) Kwao ile ilikuwa ni starehe ya mbwa tu, ya kukalia mkia wake (uk. 204).

Maelezo haya yana maana dhahiri na maana ya tamthiliya. Maana tamthiliya, ni maelezo yanayowanasibisha wale mahaini waliokubali kuwa ushahidi wa uongo na kupata starehe ya kula vizuri kule gerezani, ile ni starehe ya mbwa kukalia mkia wake. Sentensi ina maana ya kuwa walikuwa wanajiangamiza wao wenyewe bila ya kujijuwa. Pia, maelezo haya yana maana kuwa watu hawa waliokubali kukaa ushahidi ni vibaraka au vijibwa vya wakubwa kwa maslahi ya wakubwa hao bila ya wao kunufaika kitu, isipokuwa kukalia mikia yao. Hapa, vijibwa imenasibishwa na watu wanaofanya mambo ya manufaa kwa maslahi ya wengine na wao kubakia katika hali ya udhalili.

iv) Mahakimu wa mahakama hizo akawateuwa yeye mwenyewe na watatu katika hao ndio hawa waliopo hapa mwuza samaki, mwuza maziwa, na mwalimu wa

> chuoni. Wanahukumu kesi ya mahaini waliomuuwa Kigogo mwenyewe mfadhili wao … (uk. 233).

Haya ni maelezo ambayo yanafafanua namna mahakimu walivyopatikana na uzoefu wa kazi walizokuwa nazo kabla ya kupewa nafasi hizo. Kwa mujibu wa nadhari ya Umarx, kuzingatia tajiriba ya kimaisha katika jamii, maelezo haya yanayoonesha kutoridhika na uteuzi wa watu wenye sifa hizi. Kwa upande mwingine, maelezo haya yanatutaka turudi nyuma katika kazi zilizopita kama vile *Kasri ya Mwinyi Fuadi*, *Kuli* na *Vuta N'kuvute*. Kisha, tuangalie ni nani waliokuwa wakiongoza harakiti hizi. Je, watu hawa wamepewa nafasi gani katika serekali hii ya mapinduzi? Kinachoonekana ni kuwa wapiganiaji wa uhuru walitengwa na kubakia nje ya serikali; na baada ya kuuliwa Kigogo ndio waliokamatwa na kutiwa ndani. Ndiyo maana walibakia na majina yale yale waliyoitwa wakati wa ukoloni kama vile makomredi, makomunist na watu wasioamini Muungu. Kwa mfano, Faraji ni mhusika aliyejitokeza katika *Kuli* kama ni kiongozi wa chama cha wafanyakazi, wakati katika *Haini* alijitokeza kama msomi wa sheria aliyebakia mitaani bila ya kazi. Baada ya kuuwawa Kigogo akawa ni miongoni mwa watuhumiwa wa uhaini. Hali hii haikuwaridhisha wasomi na jamii kwa jumla.

#### 4.2.3.4 Dhamira Zilizofichama kupitia Jina la Kitabu

Mwandishi katumia majina ya kazi zake kuelezea muhtasari juu ya maudhui yanayopatikana katika kazi hizi. Pia, majina haya yana nafasi ya kudokeza dhamira zilizofichama katika kazi hizi kama zinavyodokezwa na utafiti huu.

##### 4.2.3.4.1 Riwaya ya *Kuli*

Jina la kitabu hiki ni *Kuli*, kwa maana ya kawaida kuli ni mtu anayefanya kazi ya kubeba mizigo bandarini (BAKIZA, 2010). Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo, jina hili lina kiashiria fulani. Kulingana na utafiti uliofanyika, yumkini, kuli ni neno linalojenga hali halisi ya Wazanzibar wakati wa enzi za utawala wa Kiingereza. Wazanzibar walikuwa wanachukuliwa kama ni makuli kwa maana ya watu wasiojithamini wala kuthaminiwa na serikali ya Waingereza. Pia nadharia ya Umarx, jina hili limezingatia tajiriba ya maisha ya jamii, inaoneshwa kupitia jinsi walivyokuwa makuli katika kazi hii ya *Kuli*, Zanzibar. Walikuwa hawajithamini kwa kusalitiana wenyewe kwa wenyewe katika suala lenye maslahi ya taifa kama vile uhuru na maendeleo. Suala hili linasawiriwa kupitia mhusika Mzee Tindo. Pia, walikuwa hawathaminiwi kwa sababu Waingereza walikuwepo Zanzibar kwa maslahi yao tu, na si kwa maslahi ya taifa hili. Maelezo haya yanathibitishwa pale mwandishi anaposema:

> Si aghalabu kwa Morarji kupewa shauri na Mzee Tindo
> akakataa kwani kila shauri alilolitoa Mzee huyo lilikuwa
> ni la manufaa kwa tajiri huyo. ( uk. 28).

Maelezo haya yanathibitisha ukuli wa Wazanzibar, kwa sababu hata vichwa vyao vipo kwa ajili ya kubeba akili za kuwanufaisha wakoloni.

Maana nyingine ya kuli kwa mujibu wa nadharia ya Umarx, jina hili linaurejelezi wa sifa za kijamii. Hawa ni watu waliokuwa wakibeba usaliti kwa maslahi ya Waingereza na kuwatumikia. Kwa mfano, mkalimani ni kuli aliyekuwa akibeba maneno ya Waingereza kwenda kwa Waswahili na Waswahili kwenda kwa Waingereza. Hili linadokezwa vema kwa maneno yafuatayo: “Baada ya Rashidi kumaliza kula yamini yule hakimu alianza kusema kwa Kingereza na mkalimani alitafsiri”

Pia Kuli ina maanisha wale askari Wazanzibar waliokuwa na kazi ya kubeba mizigo kwa kubeba amri kutoka kwa maofisa wa Kiingereza. Walitii kila amri bila hata ya kuhoji na kupima amri hiyo na kuwafanyia ndugu zao kama anavyoeleza mwandishi:

> askari hao walifululiza mbio gatini na walipofika humo wote walijipanga kwa mstari na kusimama namna moja baada ya kupewa amri na yule ofisa wa Kiingereza. (uk. 163)

Hizi ndizo baadhi ya maana za kuli zilizojificha katika jina hili la *Kuli*.

#### 4.2.3.4.2 Riwaya ya *Vuta N'kuvute*

Maana ya kawaida ya jina la kitabu hiki *Vuta N'kuvute*, ni kuvutana kwa watu wawili au pande mbili. Mvutano huu huweza kuwa juu ya migogoro kama vile ya kisiasa kama ilivyojitokeza kwa Denge na wakoloni wa Kingereza; migogoro ya kiutamaduni kama ilivyo kwa Yasmin na jamii yake; mvutano wa kisaikolojia; au kuvutana ya katika michezo kama ulivyo mchezo wa kuvuta kamba ua mchezo wa singale.[4] Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo, jina hili lina kiashiria fulani. Kulingana na utafiti uliofanyika, yumkini, vuta n'kuvute inayojitokeza katika jina hili inatoa maana kama zifuatazo: Kwanza, ni vuta n'kuvute ya Yasmin. Mhusika Yasmin alikuwa na vuta n'kuvute ndani ya akili yake kwa kutaka kuishi Uswahilini wakati bado Uhindini anakutaka damu. Pili ni mvutano wa ushiriki wa harakati za ukombozi. Kiuhalisi Yasmin hakuwa mwanaharakati bali alikuwa anavutwa kwa tamaa ya kupata mapenzi ya Denge. Pia, Denge alikuwa na mvutano katika akili yake. Katika suala la mapenzi, Denge hakuwa anampenda Yasmin kidhati, bali alimpenda kwa lengo la kukamilisha shahawa (Hamu ya kimapenzi na kutaka kufanya tendo la ndoa).

[4] Singale ni mchezo wa watoto ambao hucheza wakichaguana kwa bahati nasibu. Mwisho huvutana baina ya pande zile mbili zilizochaguana na kupatikana mshindi.

#### 4.2.3.4.3 Riwaya ya *Haini*

Kwa maana ya kawaida, haini ni kudhulumu mtu au serikali kwa kitendo cha usaliti. Kwa maana nyingine, ni mtu afanyae dhulama au avunjae ahadi. Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo, jina hili lina kiashiria fulani. Kulingana na utafiti uliofanyika, yumkini, haini ni neno linalotoa taswira juu ya hali ilivyokuwa baada ya mapinduzi ya Zanzibar ya 1964. Jamii kubwa ya Wazanzibar ilikuwa ikilalamikia juu ya hali ilivyokuwa ikiendeshwa na serikali yao kwa kuchukuliwa watu ovyo na kwenda kuuliwa kwa madai ya uhizibu, uwarabu, au kutaka kupindua serikali. Suala hili lilijenga dhana ya kuona kuwa serikali yao ni ya kihaini.

Pia, kwa upande wa nadharia ya Umarx, jina hili inadokeza tajiriba na muundo wa jamii hii. Hivyo, haini huweza kutoa kitendawili kwa kujiuliza ni yupi haini kati ya watu waliotuhumiwa uhaini bila ya ushahidi au wale usalama waliokuwa wakiwasulubu watuhumiwa na hadi kufikia kuuliwa kabisa. Pia, upangaji wa serikali ulikuwa na uhaini ndani yake dhidi ya wasomi. Wasomi ndio walioshirki kupanga na kutekeleza mapinduzi lakini kilichotokea ni kuuliwa kwa baadhi yao na waliobaki wakatengwa na serikali yao.

### 4.2.3.5 Dhamira Zilizofichama kupitia Majina ya Wahusika

Kwa jumla, mwandishi hakutumia majina ya wahusika wa majazi. Hivyo, mbinu ya kuibua dhamira zilizofichama kupitia majina ya wahusika haina nafasi kubwa katika kazi hizi. Kama imetokea kama ilivyoelezwa hapo chini ni sadifa tu, katika uteuzi wake wa majina lakini si kwa nia ya kutumia mtindo huu.

#### 4.2.3.5.1 Riwaya ya *Kuli*

*Kuli* ni kazi ambayo kwa kiasi kikubwa haikutumia majina ya majazi katika kuwapa majina wahusika wake. Majina ya wahusika hao mengi ni ya kawaida kiasi kwamba hayawezi kutoa maana iliyofichama. Majina haya yaliteuliwa kwa kuashiria utabaka unaopatikana katika jamii. Majina ya Wazanzibar ni kama Rashid, Salum, Bakar na wengineo, majina ya Wahindi kama Marirji, na majina ya Waingereza kama George, na Willium Davis. Hata hivyo, yapo majina ambayo huweza kutoa maana iliyofichama ni:

Jina la kwanza ni, Majaliwa. Majaliwa ni jina la baba yake Rashidi. Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo, jina hili huweza kutoa kiashrii ndani yake. Kwa maana ya dhahiri, majaliwa ni kukadiriwa juu ya jambo fulani na Mungu. Kwa maana ya kitamathali, majaliwa inatupa taswira halisi ya baba yake Rashidi, kuwa ni mtu aliyejaliwa kizazi cha shida, kazi ngumu isiyo maslahi, na maisha magumu ya familia yake. Suala hili pia likawa ni majaliwa ya Rashidi kwa kurithi hali ngumu ya maisha pamoja na kufanya kazi ile ile aliyofanya baba yake, bila ya kuiridhia.

Jina jingine ni, Faraji. Faraji ni jina la mhusika ambaye alikuwa kuli na pia alikuwa ni kiongozi katika chama cha wafanyakazi. Faraji ni jina linalotoa kiashirii. Utafiti ulibaini kuwa hili ni neno linalotoka katika mnyambuliko wa neno faraja, lenye maana ya pozo la moyo juu ya shida au dhiki fulani. Kwa maana iliyofichama, faraji ni jambo lililokuja kuziba pengo la Rashidi dhidi ya hamu ya kutaka ukombozi lakini kushindwa kutekeleza azma yake kwa kusalitiwa na Mzee Tindo. Pia, hii ikawa ni faraja kwa makuli wote waliokuwa na hamu ya kupata uhuru wao.

#### 4.2.3.5.2 Riwaya ya *Vuta N'kuvute*

Kama ilivyo katika *Kuli*, *Vuta N'kuvute* ni kazi ambayo kwa kiasi kikubwa haijatumia majina ya majazi katika kuwapa majina wahusika wake. Majina ya wahusika hao mengi ni ya kawaida kiasi kwamba hayawezi kutoa maana iliyofichama. Majina haya yaliteuliwa kwa kuashiria utabaka unaopatikana katika jamii. Majina ya Wazanzibar ni kama Mwajuma na Denge; na majina ya Wahindi ni kama vile Yasmin, Raza, Kermali, Kulsum. Majina ya Waingereza ni kama vile Wright.

Jina ambalo huweza kutoa maana iliyofichama ni Koplo Matata. Koplo ni cheo katika jeshi na Matata hili ndilo jina halisi la mhusika. Jina la Matata linatoa kiashirii na kumaanisha kuwa ni mashaka juu ya jambo fulani. Maana iliyofichama katika jina hili inatoa picha halisi ya Waafrika au wenyeji wa wakoloni walivyokuwa na matata au mashaka zaidi ya wakoloni katika kuwatesa ndugu zao na kuwa vikwazo kutika kufikia malengo yao ya kujikomboa. Hii ndivyo ilivyokuwa kwa Koplo Matata katika *Vuta N'kuvute*.

#### 4.2.3.5.3 Riwaya ya *Haini*

*Haini* ni kazi ambayo imechanganya majina ya majazi na majina ya kawaida. Majina haya, tofauti na kazi zilizopita, hayaoneshi utabaka, hasa wa kijamii, kwa sababu ni kazi iliyoeleza mazingira ya baada ya mapinduzi. Hivyo, hakukuoneshwa Uhindi, Uarabu na wala Uingereza katika uteuzi huu wa majina. Kama majina haya yalidokeza utabaka, basi ni kwa upande wa hadhi ya kikazi, na ni kwa uchache na hasa kupitia vyeo vyao katika kazi. Baadhi ya majina ni majazi na huweza kudokeza maana iliyofichama. Nayo ni haya yafuatayo:-

Jina la kwanza ni Azizi. Azizi ni jina la mhusika ambaye alikuwa ni mkubwa serikalini na pia alikuwa akijulikana sana. Mhusika huyu ni mtu aliyekuwa akimfuata Khadija, mke wa Hamza kwa lengo la kutaka kufanyanae mapenzi huku akitumia kivuli cha kutaka kumsaidia kwa kumfanyia mipango Hamza ya kutoka gerezani. Azizi, kwa maana ya kawaida, lina maana ya mpenzi. Pia, hutumika kumaanisha hadhi, kitu cha thamani au zawadi (BAKIZA, 2010). Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo, jina hili ni kiashirii. Utafiti ulibaini kuwa mwandishi katumia jina hili kumaanisha watu waliokuwa wakitumia nguvu za kiutawala kwa lengo la kufanya mapenzi na wake wa watu waliodhulumiwa au wanawake wanaowaona kuwa ni wazuri. Tunamuona Azizi akifanya hili kwa Khadija.

Jina la pili ni Kanal Bunju. Kanal Bunju ni mhusika aliyekuwa mkubwa katika usalama wa serikali ya Kigogo. Ni mhusika aliyetumia nguvu kuwalazimisha mahaini kukiri kosa au kukubali kuwa mashahidi juu ya kesi ya uhaini. Pia, mhusika huyu aliwahi kupata tuhuma ya kuhusika na uhaini wa kumua Kigogo kwa lengo la kuchukua ukubwa wa nchi. Bunju, kwa maana ya kawaida, ni aina ya samaki mwenye sumu kali (Haji, 2006). Bunju wako wa aina mbili; kuna bunju ambao huliwa na kuna yule mwenye sumu, ambayo inapatikana katika ini lake. Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo jina hili lina kiashiria fulani. Kulingana na utafiti uliofanyika yumkini mwandishi katumia jina hili kufichamisha maana juu ya mhusika huyu. Hii ni kwa sababu alionekana mkali wa kufuatilia kesi ya uhaini wakati yeye alikuwa ni mmoja wa watuhumiwa wa kesi hiyo tena kwa ushahidi na kwa sababu ya kutaka madaraka. Hivyo sumu yake iliweza kuathiri kwa wenye hatia na wasiohatia.

Jina la tatu ni Haramia. Haramia ni mhusika aliyekuwa akishutumiwa juu ya uhaini. Alipata mateso makubwa hadi kufika kuwekwa chumba kimoja na chatu lakini

alifanikiwa kumuuwa chatu huyo. Mhuska huyu ndiye aliyetoa siri juu ya kuhusika kwa Kanal Bunju katika mauwaji ya Kigogo. Haramia, kwa maana ya kawaida ni mtu anaofanya uhalifu kwa kutumia nguvu katika vyombo vya majini (BAKIZA 2010). Hivyo, haramia anaonekana kama jambazi, mnyang'anyi au gaidi. Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo jina hili lina kiashirii. Utafiti umegundua kuwa mhusika kapewa jina hili kwa njia ya kejeli. Hii ni kwa sababu mateso aliyopata mhusika huyu ni zaidi ya mateso anayostahiki haramia wakati yeye ni mtuhumiwa tu. Kwa matazamo mwingine, huyu alikuwa haramia kweli kutokana na vigezo vifuatavyo: kwanza, kwa kujua siri ya Kanal Bunju kuhusika katika mauaji ya mkubwa. Pili, kwa kushtukia mtego wa akina Kanal Bunju. Na tatu, kwa kupambana na chatu aliyeekewa chumba kimoja kama ni adhabu ya mwisho.

## 4.3 Miktadha Iliyomsukuma Mwandishi Kutumia Mtindo Huu

Sehemu hii imejadili na kuchambua muktadha na mazingira mbalimbali yaliyomsukuma Shafi Adam Shafi kutumia mtindo aliotumia. Data za utafiti zimebainisha kuwa mwandishi Shafi Adam Shafi katumia mtindo mchanganyiko, ukiongozwa na mtindo wa kihistoria; yaani, kueleza matukio kupitia historia ya jamii husika. Huu ni mtindo uliotumika katika kazi zake zote za kifasihi kama zilivyotajwa huko nyuma. Pia, mwandishi katumia mtindo wa kutumia barua, mtindo huu umetumika katika *Kuli* ambako kuna barua ya Amina kumpelekea mume wake akiwa gerezani (uk. 196). Pia, katika *Vuta N'kuvute*, barua ya Shihabu akiwa Tanga kumpelekea Mpenzi wake Yasmin akiwa Unguja (uk. 149). Katika *Mbali na Nyumbani* katumia maelezo ya barua bila ya kuiwasilisha barua yenyewe kama alivyoeleza "Mimi lilinijia wazo la kumwandikia barua baba yangu, nilimwomba aniletee pesa ili niweze kufanya safari ya kurudi nyumbani" (uk. 63).

Mtindo mwingine aliotumia ni kuchanganya fasihi simulizi ndani ya fasihi andishi. Shafi Adam Shafi kutumia nyimbo za kubembelezea watoto kama kipengele cha fasihi simulizi takribani katika kazi zake zote. Katika *Kasiri ya Mwinyi Fuadi*, Kijakazi anamuimbia Fuadi;

Lala mtoto lala, katika kitanda lala,
Baba ni mtukufu, mama ni mtukufu,
Lala mtoto lala, katika kitanda lala… (uk. 66)

Katika *Kuli*, Bi Mashavu anamchuchia mtoto wake Rashidi kwa wimbo ufuatao:

Usilie, usilie
ukaniliza na mie,
machozi yako yaweke,
nikifa unililie. (uk. 4)

Katika *Vuta N'kuvute*, mwandishi pia katumia wimbo huu:

Wache waseme
Sina budi naye
Sihofu lawama
Sababu ya yeye… (uk. 189)

Pamoja na kutumia nyimbo lakini pia alionesha kuitukuza nafasi ya nyimbo au fasihi simulizi kama anavyoeleza katika riwaya ya Vuta n'kuvute: "bwana Shihab, mshabiki mkubwa wa tarabu na mpenzi wa cheusi dawa," (uk. 144).

Kwa upande wa kitabu cha *Haini*, pia mwandishi katumia nyimbo kwa wingi sana kama kipengele cha fasihi simulizi. Miongoni mwazo ni huu:

Kile kidau kijacho,
Hamkosi mna changu,
Mna mkufu nitunge,
Kadri ya shingo yangu,
Hiupati siuvai,
Wala simpi mwezangu,
Nenda mpa mama yangu,
Msiri wa mambo yangu. (uk. 144)

Pamoja na mitindo hiyo, utafiti umegundua kuwa mwandishi Shafi Adam Shafi katamalaki katika mtindo wa matukio ya kihistoria. Mtindo huu umelazimisha kutoa maudhi makubwa na ya ndani na kuonekana dhahiri wepesi wa fani yake, hasa kipengele cha lugha. Hali hii inatokana na miktadha mbalimbali iliyomsababisha kutumia mtindo huu. Tasnifu hii imezigawa sababu hizo katika sehemu tatu: sababu za kitaaluma, sababu za kijamii na sababu za kisiasa, kama inavyoelezwa hapo chini.

### 4.3.1 Kitaaluma

Hoja ya kwanza ni kiwango cha elimu alichokuwanacho wakati alipoanza kuandika kazi zake. Kwa mujibu wa nadhari ya Umarx, mazingira ya kuishi yanachukua nafasi ya msingi yakilinganishwa na mawazo ya maisha ya binadamu. Hivyo, utafiti ulibaini kuwa miongoni mwa sababu zilizofanya kazi za Shafi Adam Shafi kuwa ni zenye lugha nyepesi kisanaa na mtindo ambao hauvutii kwa baadhi ya wasomaji inatokana na kiwango cha elimu cha mwandishi wakati alipoaza kuandika. Shafi Adam Shafi alianza kuandika wakati akiwa Chuo Cha Saidi Khalifa Teacher Training College, kwa

sasa ni Nkrumah kampasi ya Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), mwaka 1957 - 1959.

Katika chuo hiki walikuwa wakisoma masomo ya sekondari na ualimu wa msingi kwa miaka mine. Mwandishi[5] anaeleza kuwa wakati wakiendelea kusoma masomo ya sekondari alipata hamu na ushawishi wa kuandika kazi ya fasihi. Anaongezea kuwa Katika wakati huu aliamua kuandika kazi yake ya kwanza aliyoiita, "Mabwana Shamba wa Visiwani." Baada ya kushauriwa na wataalam na wachapishaji, kazi hii ikapewa jina la "*Kasri ya Mwinyi Fuadi*". Kazi hii ilichukua muda hadi ilipochapishwa mwaka 1979. Hii ilitokana na ukweli kuwa kazi hii chapwa na nyepesi kifasihi.

Jambo la pili ni ujuzi wa kisanaa katika uandishi wa kazi zake za kifasihi. Nadharia ya Umarx inahusu nyanja mbalimbali kama uchumi, historia, jamii na mapinduzi. Kupitia nadharia hii, utafiti ulibaini kuwa mwandishi katika hatua za mwanzo hakuwa mwanafasihi; hali hii ilisababisha kuandika na kutumia mtindo aliotumia kama ilivyoelezwa hapo juu. Hadi mwandishi anaanza kuandika kazi yake ya kwanza ambayo ni riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuadi* alikuwa ni mweledi sana katika tasnia ya uandishi wa habari. Pia, mwandishi alikuwa hajapata kusoma kazi za kifasihi za kutosha ambazo zingempa ujuzi na kumfanya abobee katika uandishi wa kazi za kifasihi. Hivyo, utundu wa kuanza kuandika na kupata muongozo kutoka kwa wachapishaji ndio uliomsaidia kuingia kikamilifu katika tasinia hii na kupata matunda haya waswahili wanayojivunia.

Jambo la tatu ni utumiaji wa historia, ni mtindo aliojifunza na kuwa dira katika uandishi wake. Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo, historia, hasa mapinduzi ni imani ya mwandishi. Utafiti huu umebaini kuwa mwandishi alitumia mtindo huu

1 Maelezo ya Shafi Adam Shafi katika mahojiano yaliyofanyika baina yake na mtafiti mnamo tarehe 25 / 2 / 2015 huko nyumbani kwake Bunju, Dar es Salaam.

baada ya kuamua kuandika juu ya masuala ya ukombozi badala ya yale ya kimapenzi na kiupelelezi yaliyokuwa yakiandikwa sana wakati ule. Kutokana na hali hiyo mwandishi alipata kujifunza mtindo huu kupitia mswada wa kazi ya Michele[6], (haikutajwa jina lake) kazi hii ilitumia mtindo wa matukio ya kihistoria. Mwandishi alipata ujuzi kupitia kazi hii, na kwa kuwa alitaka kuandika juu ya masuala ya kihistoria au mambo ya ukombozi, ikawa kwake ni mtindo muwafaka kuutumia.

Jambo la nne, ni kutoa hisia kwa matukio aliyoshuhudia na aliyoshiriki. Nadharia ya Umarx, unaeleza juu ya harakati za matabaka za kijamii katika kukuza imani za watu. Utafiti umebaini kuwa mwandishi katumia mtindo huu ili kupata fursa ya kutoa hisia zake juu ya matukio aliyoyaona na yale aliyoshiriki mwenyewe. Mtindo huu ulikuwa muwafaka zaidi kutumika katika kutoa hisia juu ya yale aliyoshuhudia katika maisha yake. Hizi ni kazi zinazoelezea matukio ambayo yamemgusa mwandishi kwa hali moja au nyingine. Chambilecho mwandishi mwenyewe kuwa "Kazi hizi ni matokeo ya yale niliyoshuhudia na hata kunikabili mimi mwenyewe[7]". Mwandishi alipata kushuhudia mgomo wa makuli Zanzibar wakati akiwa ni mwanafunzi. Hali hii ikazua riwaya ya Kuli. Aidha kitabu cha *Vuta N'kuvute* kinasawiri jinsi mwandishi alivyokutwa na masaibu mengi kama vile kuwa katika harakati za ukombozi wa Zanzibar na kuwa na mpenzi, mtoto wa kihindi. Matukio haya anambebesha Denge katika Vuta n'kuvute. Katika *Haini*, kushutumiwa kesi ya uhaini wa kumuuwa Raisi wa kwanza wa Zanzibar Sheikh Abeid Amani Karume. Na kitabu cha *Mbali na Nyumbani* ni tawasifu ya maisha yake kwa jumla.

Jambo la tano, ni maudhui makubwa yaliyo katika kazi hizi. Utafiti umebaini kuwa miongoni mwa sababu zilizomsababisha Shafi Adam Shafi kutumia mtindo huu ni

---

[6] Ni mwandishi wa kazi za kifasihi na aliyekuwa akitumia mtindo wa kihistoria katika uandishi wake.
[7] ibd

maudhui aliyokusudia kuwasilisha kwa hadhira yake. Kazi za Shafi Adam Shafi zimebebwa na kuegemezwa kwenye matukio ambayo yanamkereketa na kutaka kuyawasilisha kwa jamii kwa njia ya sanaa. Kwa mujibu wa nadharia ya Umarx, kazi ya kifasihi inakuwa bora ikiwa itazingatia tajiriba ya watu ya kimaisha. Kutokana na hali hii ilibidi katika kazi hizi fani yake ibebwe na kutolewa na maudhui; na siyo fani kuibua maudhui. Suala hili linadhihirika katika takribani kazi zake zote; na ndio maana zimepungua matumizi ya tamathali za semi, methali pamoja na mbinu zinyinge za kifasihi. Mbinu hizi huweza kubeba na kuibua dhamira mbalimbali katika kazi ya kifasihi pale zinapotumiwa katika kazi iliyotayarishwa zaidi kifasihi kama vile kazi za Shaaban Robert (*Kusadika*, *Adili na Nduguze*), na Mohamed Suleiman Mohamed (*Kiu* na *Nyota ya Rehema*).

### 4.3.2 Kijamii

Kwanza, kuonyesha hali halisi ya jamii ya Zanzibar. Kwa kuangalia tajiriba ya watu ya kimaisha, ikiwa ni msingi wa nadharia ya Umarx. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa pamoja na kuwa kazi hizi zimeonesha matukio ya kweli yaliyowahi kutokea Zanzibar, pia zimeonesha hali halisi ya jamii ya Zanzibar. Kazi walizokuwa wakifanya watu wa Zanzibar kama vile ukuli, kama ilivyooneshwa katika kitabu cha *Kuli*, ni miongoni mwa kazi maarufu kwa jamii ya Zanzibar hadi hii leo.

Pili, kuonyesha kuwa jamii ya Zanzibar na utamaduni wake vimejengwa na mchanganyiko wa watu kutoka sehemu tofauti kama vile Warabu, Wahindi, watu kutoka bara na sehemu nyingine, kama ilivyooneshwa katika *Vuta N'kuvute*. Katika kitabu hiki mwandishi anaeleza kuwa:

> Mwajuma alikuwa ni msichana wa Kiafrika na tabia yake ya ucheshi na masihara ilimfanya Yasmin avunje miko ya Kihindi ya kutoingiana na Waafrika. (uk. 4).

Na kwa upande wa utamaduni, Wazanzibar asilimia kubwa ni waumini wa dini ya Kiislamu. Wanapopatwa na majanga huwa wanaomba dua kwa Mungu ili kuepushwa na majanga au mitihani iliyowakuta, kama ilivyooneshwa katika kitabu cha *Haini*. Mwandishi anaeleza: "Dua zote alizoomba Khadija kumuombea Hamza bado hazikutakabaliwa." (uk. 193)

Tatu, kuficha tawasifu yake ndani ya kazi zake za kifasihi. Mwandishi ametumia kazi hizi kwa kiasi kikubwa kutoa na kueleza tawasifu yake ya maisha kwa jumla. Hii ni kabla ya kuandika kitabu cha tawasifu yake cha *Mbali na Nyumbani*. Kwa mujibu wa Umarx, imani za jamii ina tukunza mapendekezo ya mtu. Hivyo, utafiti ulibaini kuwa kabla ya kazi hii mwandishi alitumia kazi zake za nyuma kutoa tawasifu yake. Hali hii, kwa kiasi, ilimfunga na kumlazimisha kutumia mtindo huu wa kihistoria. Shafi Adam Shafi alikuwa ni mwanaharakati na aliwahi kuwa kiongozi wa vyama vya wafanyakazi kama anavyoeleza;

> Baada ya mapinduzi ya Zanzibar tuliunganisha Vyama vya Wafanyakazi na kuunda Federation of Revolution of Trade Union.[8]

Hali hii pia imeelezwa katika kitabu cha *Kuli* kwa maneno haya

> Bakari, Faraji na viongozi wengine walikuwa wamekaa juu ya viti mbele ya wafanyakazi waliokuwa wakingojea kwa hamu nini wataambiwa na hapo tena Faraji alisimama na kuaza kusema. (uk. 157).

---

[8] Mahojiano ya mtafiti na Shafi Adam Shafi yalifofanyika siku ya 25/ 2 / 2015, huko nyumbani kwake Bunju Dar es Saalam.

Kwa upande wa *Vuta N'kuvute*, matukio mengi ya mhusika Denge yanamhusu kama kushiriki katika mapambano ya ukombozi. Kwa upande wa kazi ya *Haini*, pia alikuwa ni mtu aliyepata kufungwa baada ya kifo cha Sheikh Abedi Amani Karume kwa kosa na kutuhumiwa kuwa ni haini kama ilivyotokezea kwa muhusika Hamza; "Nyote nyinyi hammo lakini…" (uk. 266).

Nne, muda wa kazi zilipoandikwa. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa mtindo wa kazi hizi umeathiriwa na muda wa kazi zilipoandikwa. Kwa mujibu wa maelezo ya mwandishi, alipata ushawishi wa kuandika kutoka kwa wenzake baada ya kuona kazi nyingi zilizoandikwa Zanzibar ni za mapenzi na upelelezi. Maelezo haya yamechambuliwa kutokana na nadharia ya Umarx kuhusika na jamii na mapinduzi. Kipindi hiki kilikuwa ni kipindi cha vugu vugu la kutafuta uhuru wa Zanzibar na kipindi cha mchakato wa mapinduzi ya Zanzibar yaliyofanyika 1964. Hali hii ya kuwepo kwa kazi za kifasihi zinazozungumzia ukombozi zaidi kuliko mapenzi. Iliwavutia wasomi na wanafasihi wa Zanzibar kutokana na hali hiyo ndio maana kazi zote hizi zikaandikwa kwa mtindo wa kimatukio ya kihistoria zaidi ili kukidhi mahitaji ya wakati.

### 4.3.3 Kisiasa

Kwanza, matukio ya kisiasa yaliyotokea katika historia ya Zanzibar. Tajiriba ya watu ya kimaisha, Zanzibar imesaidiau utafiti kubaini kuwa: Zanzibar tokea awali ilikuwa ni nchi inayoendesha mapambano ya kisiasa kupitia tawala na wakoloni wa zama tofauti na kutoka sehemu tofauti. Kama anavyoeleza Al-Ismaily (1999:101):

> Ni vigumu kuweza kusema kwa yakini ni lini khasa ulianza msisimko wa siasa na harakati zake Zanzibar

> katika kugombania kujivua na utawala wa ukoloni wa Waingereza.

Matukio haya, pamoja na wingi na umaarufu wake, yalikosa waandishi wa kuyaandikia katika uhalisi wake. Hali hii ilimtia hamasa ya kupata hamu ya kuyaandika kupitia tasinia ya fasihi. Matukio haya ni mgomo mkuu wa wafanyakazi wa bandarini uliowahi kutokea visiwani Zanzibar mwaka 1948, na kuelezwa katika kazi ya *Kuli* kama anavyoeleza; "Sasa hatuna njia yoyote iliyobakia ispokuwa kugoma," (uk. 157). Haya ni mapambano ya kudai uhuru na harakati za kupambana na ukoloni. Maelezo haya pia, yanathibitishwa katika *Vuta N'kuvute*, kama anavyoeleza mwandishi: "Kufa au kupona tunataka uhuru" (uk. 166).

Pili, nguvu na ushawishi wa kisiasa. Matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa pamoja na matukio ya kisiasa yaliyomsababisha mwandishi kutumia mtindo huu wa kihistoria, lakini pia ni nguvu na ushawishi wa kisiasa alioupata mwandishi. Mwandishi alikuwa ni mwanasiasa na alikuwa karibu zaidi na watu waliokuwa wakishiriki kikamilifu katika mchakato wa kupigania uhuru wa Zanzibar. Kwa mujibu wa nadharia ya Umarx, hii inatokana na tajiriba ya watu ya kimaisha, kisiasa pamoja na mjengeko wa jamii yao. Hali hii ilimuandaa kisaikolojia kupenda kutoa elimu juu ya suala la ukombozi wa Zanzibar na hata baada ya ukombozi huo. Pia, ukaribu wake na wanasiasa ulimchangia kwa kiasi kikubwa kuandika kazi za namna hii pamoja na kutumia mtindo wa moja kwa moja wa matukio ya kihistoria. Kama anavyoeleza mwenyewe[9]:

> Kwa nini hujaribu kuandika riwaya? Na hasa aliyenitia ushawishi huu, kuna rafiki yangu mmoja anaitwa

[9] Mazungumzo ya Adam Shafi juu ya uandishi wake wa riwaya yaliyofanyika tarehe 19/07/2003. Na Lutz Diegner.

> Khamis Abdalla Ameir. Yeye alikuwa kiongozi wakati niko katika chama cha wafanyakazi kabla ya mapinduzi …

Ushawishi huu kwa kiasi kikubwa ulichangia na kumuathiri Shafi Adam katika uwandishi wake na mtindo aliotumia katika kazi zake.

## 4.4 Athari za Mitindo yake kwa Wasomaji wa Kazi Hizi

Sehemu hii inajadili athari za mtindo uliotumika katika riwaya teule za Shafi Adam Shafi. Utafiti umegundua athari zifuatazo katika mtindo aliotumia Shafi Adam Shafi. Athari hizi zimegawiwa katika athari chanya na athari hasi.

### 4.4.1 Athari Chanya

Mosi, utafiti umebaini kuwa, kupitia mtindo aliotumia Shafi Adam Shafi unasaidia kufahamika kazi zake kwa wepesi. Kazi za Shafi Adam ni kazi ambazo wasomaji wengi wanazijua dhamira alizokusudia mwandishi. Hali hii inatokana na kuwa lugha aliyotumia ni ya kawaida na haina tamathali za semi, methali, na lugha ya mafumbo kwa wingi. Pia, mtindo wake kwa jumla unamuongoza msomaji wa kazi hizi kujua unakusudia kueleza mambo gani kwa hadhira yake. Maelezo haya yamechambuliwa kutokana na nadharia ya Umuundo, kwa kuwa kufahamika kwa kazi ni urejelezi wa sifa fulani za kiutamaduni katika kazi hizi. Utafiti ulibaini kuwa, kazi hizi zinafahamika na takribani kila mtu mwenye kuweza kusoma, bila ya kutegemea kiwango kikubwa cha maarifa ya uchambuzi na uhakiki wa kazi za fasihi.

Pili, kurahisisha kufikisha ujumbe kwa haraka na kusoma bila ya uchovu. Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo, ujumbe huu ni urejelezi wa sifa za kiutamaduni katika

jamii. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, wanafunzi wengi wanazipenda kazi za Shafi Adam Shafi kuliko kazi nyingine. Hali linathibitika kutokana na asilimia kubwa ya wanafunzi tuliowahoji walithibitisha hilo na wengi wao kuwa tayari wamesoma kazi ya Vuta n'kuvute miongoni mwa zile kazi wanazolazimika kusoma katika muhtasari wao. Sababu ya mapenzi yao ni urahisi wa lugha na urahisi wa kuibua dhamira ukilinganisha na kazi nyingine za kifasihi. Kwa mfano, kitabu cha *Vuta N'kuvute* huvutia kwa kusoma na kutoa picha halisi ya umbo la wahusika, picha halisi ya mazingira yaliyotumika pamoja na kupata picha halisi ya dhamira iliyokusudiwa kuwasilishwa na mwandishi. Jambo hili husaidia wanafunzi kuelewa vyema kazi hii na kupata ushahidi mzuri wa dondoo wakati wa kujibu maswali.

Tatu, ni nyezo ya kufundisha historia ya Zanzibar kwa uwazi. Kwa mujibu wa Umarx, historia inahusu jamii na mapinduzi. Hivyo, utafiti umebaini kuwa kazi za Shafi Adam Shafi zinakubalika na kufaa kufundishia historia ya Zanzibar. Kazi zote hizi zimetungwa kulingana na matukio ya kihistoria. Matukio haya ni ya kweli, na yametokea katika jamii ya watu wa Zanzibar. Mwandishi katumia tajiriba yake ya maisha na ushiriki wake katika harakati za kisiasa kutunga kazi hizi. Kwa mfano *Kasri ya Mwinyi Fuadi* ni kazi inayoeleza mchakato mzima wa mapinduzi ya Zanzibar. Imeangalia matayarisho, mbinu zilizotumika, na hata matukio yaliyofanyika baada ya mapinduzi ya Zanzibar. Pia, *Kuli* imealezea namna wafanyakazi wa bandarini walivyokuwa wakinyanyaswa na Waingereza huko bandarini na njia walizotumia kuondokana na dhiki hiyo. *Vuta N'kuvute* imeelezea harakati za kupigania uhuru wa Zanzibar chini ya usimamizi wa muhusika Denge na suala la ubaguzi katika jamii. *Haini* imeeleza udhalimu na maovu yaliyokuwa yakifanyika Zanzibar kwa wananchi wa kawaida baada ya mapinduzi na hasa baada ya kifo cha Kigogo.

Nne, zimesawiri hali halisi ya mazingira na utamaduni wa Zanzibar. Kwa mujibu wa nadharia ya Umuundo, mazingira na utamaduni ni urejelezi wa sifa fulani za kiutamaduni katika kazi. Hivyo, utafiti umebaini kuwa Shafi Adam Shafi, kupitia mtindo aliotumia katika kazi zake, ameweza kusaidia jamii na wasomaji kwa jumla kuona mazingira halisi ya Zanzibar kwa kuchora ramani ya mitaa ya Zanzibar kwa maelezo na kuyataja majina. Katumia mitaa kama Chaani, Fuoni, Malindi, Kizimkazi, Beit-el-ajaib, kisiwa cha Tumbatu, Gulioni, katika kitabu cha *Kuli*. Maeneo haya hadi leo ni miongoni mwa maeneo maarufu kwa Zanzibar kiasi cha kuwa kila mtu anayeishi Zanzibar amekwishawahi kuusikia mtaa huo kama bado hajafika. Katumia Mombasa Kenya, Tanga, Dar es Salaam katika kitabu cha *Vuta N'kuvute*. Hii ni milango mikuu ya kuingilia na kutokea Zanzibar; ndio maana hata wenyeji wa maeneo haya wanauhusiano mkubwa na watu wa Zanzibar. Kwa upande wa *Haini* katumia maeneo kama vile Kwabamkwe, Kinua miguu, Mashakani Hotel, Mahakama kuu iliyopo Vuga. Hizi ni sehemu ambazo hadi leo zinatisha na zinaogopwa na wenyeji wa Zanzibar kwa udhalilishaji wa watu bila ya hatia ya msingi. Pia, mwandishi katumia utamaduni halisi wa Zanzibar kama vile masuala ya ndoa, ambayo yamegusiwa katika kazi zote tatu. Masuala ya imani ya kidini na sherehe yamezungumziwa zaidi katika *Kuli* na *Vuta N'kuvute*. Haya yote yamekuwa yakionekana kwa uhalisi katika kazi zake.

### 4.4.2 Athari Hasi

Kwa upande wa athari hasi, utafiti umebaini kuwa kutumika kwa mtindo huu kunasababisha kubezwa kwa kazi hizi na kuonekana mwandishi kutobobea katika ubunifu wa kimitindo. Jamii, kwa kukosa weledi katika fasihi na kutokuwa na tajiriba ya kutosha katika kusoma kazi za kifasihi hususan riwaya, imekuwa ikitoa hukumu ya

kuona kuwa Shafi Adam Shafi hajabobea katika utunzi. Dhana hii inakuja kwa kuamini kazi ya fasihi ni lazima iwe na visa vya kubuni. Ikiwa ni vya kweli basi vitatolewa katika ubunifu usiodhihirisha uhalisi wake. Hali hii inatokana na tajiriba ya watu ya kimaisha. Kutokana na dhana hii, kazi za Shafi Adam Shafi zimekuwa zikihesabiwa ni kazi chapwa na kuonekana mwandishi kutobobea katika ubunifu.

Utafiti umebaini kuwa mtindo aliotumia Shafi Adam Shafi umekuwa wa wazi na wenye kutoa matukio yake bayana.  Hali hii imekuwa ikiwafariji wanafunzi wanotumia kazi hizi kama ni vitabu vya ziada na kutumika katika mitihani yao. Kifasihi, hali hii imekuwa ikiwalemaza kwa kutotumia upeo wa akili zao na kuchanganua mambo ya ndani yawezayo kupatikana katika kazi za kifasihi. Pia, mtindo huu humfanya mchambuzi na mhakiki wa kazi za fasihi kuona urahisi wa kuchambua kazi baada tu ya kujua historia ya maisha ya jamii iliyoandikiwa. Hii ni kwa sababu kazi hizi hazina matumizi ya tamathali za semi, mafumbo, taswira na mambo mengine yanayohitaji kuchambuliwa kiundani.

Pia, utafiti umebaini kuwa kazi hizi zinachosha kutokana na kuwa na mwelekeo mmoja wa kimaudhui. Kazi zote hizi zina mwelekeo wa ukombozi wa kisiasa na kiutamaduni kwa kuzungumzia zaidi siasa na utamaduni wa Zanzibar. Jambo hili linaonesha namna gani kazi hizi zimekosa upana katika uchambuzi wa kimaudhui. Katika mfumo wa siasa ya sasa, kazi hizi zinaonekana kushadidia na kushikilia itikadi ya chama kimoja ambacho ni Chama Cha Mapinduzi ( C C M ). Chama ambacho kinashikilia sera ya mapinduzi na kujinasibu na sera hiyo kama ndio msingi mkuu wa kuendelea kuwepo kwake nchini Zanzibar. Kutokana na itikadi hii, wachambuzi na wahakiki walio kinyume na itakadi ya chama hiki wanazichukulia kazi hizi kama sehemu ya kueneza sera na propaganda zakei.

### 4.5 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura hii imefafanua dhamira zilizofichama, sababu zilizofanya kutumia mtindo wa matukio ya kihistoria, na athari za mtindo huu kwa wasomaji wa kazi hizi. Dhamira zilizofichama katika kazi hizi ni kuwa harakati za kupigania uhuru zilikuwa ngumu kutokana na vibaraka vya kikoloni kufaidika na utawala huo. Hivyo kuamua kuwasaliti ndugu zao, kama mhusika wa *Kuli* Mzee Tindo alivyofanya kwa makuli wenzake. Sura hii pia, inajadili la matatizo ya kijamii na kiuchumi. Inaonekana kuwa suala la utabaka ni gumu kuvunjika ghafla kwa sababu ni suala lenye mizizi ya kiuchumi, kiutawala na hata kiutamaduni, kama inavyooneshwa kwa mhusika Yasmin anamtuma mtu aende kwao kumuombea radhi ili arudi. Hata kama inaonekana kila upande watu wanaibia kuoa upande mwingine, lakini ni wale wenye hadhi maalum. Mfano Mswahili mwenye uwezo mkubwa wa kifedha au cheo serikalini ndie anayeweza kuozeshwa Muhindi au Mwarabu, na mwanamke anayetoka katika familia yenye hadhi Uswahilini ndie anayeweza kuolewa na Mhindi au Mwarabu.

Ama kwa upande wa mtindo, tasnifu imeonesha kuwa kazi hizi zimetumia mtindo wa matukio ya kihistoria, mtindo wa barua na kuchanganya fasihi simulizi ndani ya fasihi andishi kwa kutumia nyimbo. Sababu za kutumia mtindo huu ni kuathiriwa na mazingira aliyokuwa akiishi, kiwango cha elimu na uzoefu wa kutunga kazi za kifasihi na shughuli alizokuwa akijishughulisha nazo.

Zaidi ya hayo, sura inajadili athari za mitindo yake kwa wasomaji wa kazi hizi. Nazo zipo chanya na hasi. Athari chanya, kufika kwa urahisi juu ya lengo lililokusudiwa kwa jamii husika na kupata mazingira halisi ya Zanzibar na matukio yake. Na athari hasi, jamii imekuwa ikizidharau kazi hizi kwa kuona kuwa hazijabobea kiubunifu na

pia jamii ya Zanzibar kuziona kazi hizi ni zenye kumili katika mrengu mmoja wa kisiasa katika mfumo huu wa vyama vingi.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumetoa hitimisho kuhusu utafiti wetu. Sura yenyewe ina sehemu tano. Sehemu ya kwanza imebeba muhtasari wa tasnifu hii; ya pili imedokeza kuhusu utoshelevu wa mkabala tulioutumia katika uchambuzi wa data za utafiti huu; ya tatu imezungumzia mambo mapya ambayo yameibuliwa na utafiti wetu. Sehemu ya nne inatoa maoni ya utafiti juu ya mambo mbalimbali yaliyobainika kuhusiana na utafiti wetu; na ile ya tano inatoa mapendekezo kwa tafiti zijazo kuhusiana na maeneno yaliyogusiwa na utafiti huu.

## 5.2 Muhutasari wa Tasinifu

Utafiti huu ulijikita kuchunguza Upande wa Pili wa kazi za fasihi, ambapo vipengele vinavyotoa dhamira zilizofichama vinavyopatikana katika riwaya tatu za Shafi A. Shafi vilibainishwa na kujadiliwa. Riwaya zilizotumika ni *Kuli*, *Vuta N'kuvute* na *Haini*. Utafiti ulilenga mambo matatu yafuatayo: Kuchunguza upande wa pili wa riwaya teule za Shafi Adam Shafi, kwa kuangalia dhamira zilizofichama katika kazi hizo. Kuchunguza na kubainisha muktadha mbalimbali iliyomsukuma Shafi Adam Shafi kutumia mtindo wa matukio ya kihistoria katika kazi zake. Pia, kubainisha athari za mtindo huo katika kazi za Shafi A. Shafi kwa wasomaji wake.

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya kwanza imetambulisha tatizo la utafiti. Utambulisho umeanza kwa kueleza historia fupi ya mwandishi, kisha usuli wa tatizo kwa kueleza dhana ya upande wa pili, maana zilizofichama, dhamira zilizofichama,

dhana ya riwaya kwa ufupi ikiwa pamoja na sababu za kuchagua riwaya hizi. Vile vile, imeeleza tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na manufaa ya utafiti. Sura ya pili imefafanua maandiko mbalimbali yanayozungumzia kuhusu dhamira zilizofichama katika kazi za fasihi pamoja na maandiko yanayozungumzia kazi za Shafi Adam Shafi. Maandiko haya, hatimaye, yametumika kubainisha mapengo ya kimaarifa kuhusiana na mada hii.

Katika sura ya tatu, utafiti umeelezea kuhusu mbinu na vifaa vilivyotumika katika mchakato mzima wa utafiti huu. Vipengele vilivyojumuishwa katika sura hii ni mpango wa utafiti, eneo la utafiti, na walengwa wa utafiti wanaoundwa na jamii ya watafitiwa na sampuli ya watafitiwa. Vipengele vingine ni ukusanyaji wa data kwa kujumuisha zana na mbinu za kukusanyia data, mchakato wa ukusanyaji wa data na udhibiti, uchambuzi na uunganishaji wa data, nadharia zilizotumika, mipaka ya utafiti pamoja na vikwanzo vilivyoukumba utafiti huu.

Sura ya nne imejadili matokeo ya utafiti. Sura hii imegawanyika katika sehemu nne. Imeanza na kutoa muhtasari wa kazi teule ambazo ni *Kuli*, *Vuta N'kuvute* na *Haini*. Kisha, kufuatiwa na sehemu tatu kulingana na maswali yaliyouongoza utafiti huu. Sehemu ya pili ilibeba swali la kwanza kwa kujadili vipengele vinavyotoa dhamira zilizofichama kutoka katika kazi tatu za Shafi A. Shafi na kujenga upande wa pili kimaana. Sehemu ya tatu inabeba swala la pili kwa kujadili sababu zilizomsukuma Shafi Adam Shafi kutumia mtindo huu wa matukio ya kihistoria. Sehemu ya nne imeweka wazi athari za mtindo huu kwa wasomaji wa kazi za Shafi A. Shafi. Kisha kumalizia kwa kutoa muhutasari wa jumla wa sura nzima.

Sura ya tano imehitimisha kwa kutoa muhutasari wa utafiti kwa jumla yakiwemo matokeo ya utafiti. Pia, imetoa mapendekezo kuhusu mambo ambayo yanafaa

kuzingatiwa kuhusu tafiti zijazo katika maeneo yanayohusiana ama na Shafi Adam Shafi au maana zilizofichama.

## 5.3 Utoshelevu wa Nadharia

Nadharia zilizotumika katika uchambuzi huu ni U-muundo na Umarx. Kiini cha nadharia hizi ni, Umuundo ni uundaji wa matini za kimafumbo na zisizo za kimafumbo kuwa za kimafumbo. Pia nadharia ya Umarx ni kuangalia historia ya jamii kwa kuzingatia tajiriba ya watu kimaisha, siasa, mahusiano ya kiuchumi pamoja na mjengeko wa jamii yao.

Nadharia hizi zilifaa katika utafiti huu. Kwa sababu dhana na matini yaliyobebwa na kazi za Shafi Adam Shafi kupitia nadharia hizi, utafiti ulipata uhuru wa kuibua maana za methali, nyimbo na vifungu vya maneno vilivyo katika hali ya mafumbo na vile visinyo katika mafumbo kuvijengea mafumbo katika tasnifu hii. Vile vile, nadharia hii ilisaidia kuibua mazingira yaliyomfanya Shafi Adam Shafi kutumia mitindo hii pamoja na athari yake kwa wasomaji. Nadharia ya Umarx ilisaidia kutumia tajriba ya maisha ya Wazanzibar kuibua dhamira zilizofichama katika vifungu mbali mbali vya maneno na kujua mazingira yaliyomsababisha mwandishi kutumia mtindo huo. Kupitia Umuundo, imebainika kuwa Shafi Adam Shafi alitoa mambo mengi yaliyojificha katika kazi zake na ni yenye kuathiri jamii ya Wazanzibar.

Kupitia nadharia hizi, utafiti umeibua namna Shafi Adam Shafi alivyoweza kuzungumzia hali halisi ya Zanzibar ya miaka 1947 – 1977, hali ambayo inaathiri Zanzibar hadi katika miaka ya mfumo wa vyama vingi na chaguzi zake kutoka 1992 hadi sasa.

### 5.4 Mchango wa Tasnifu hii

Mchango wa kwanza ni kuibua dhana mpya, dhana ya Upande wa Pili wa kazi ya fasihi kimaana. Utafiti umetumia dhana hii ili kupanua hali ya uchambuzi wa kazi ya fasihi kwa kuangalia dhamira zilizofichama. Matokeo ya utafiti huu yamethibitisha uwezo wa kutumika kwa dhana hii kwa kutoa upande wa pili wa kazi za Shafi A. Shafi.

Mchango wa pili ni kutoa vijenzi vya dhana ya Upande wa Pili. Katika kuangalia upande wa pili, utafiti umemakinikia katika kuangalia dhamira zilizofichama. Vitu hivi hupatikana kwa kuangalia mtindo na vipengele vya lugha ambavyo huweza kutoa maana zaidi ya moja. Pia, dhamira zilizofichama hupatikana katika uteuzi wa maneno, maneno ambayo huweza kujenga lugha ya mafumbo.

Mchango wa tatu ni kuibua mpangilio wa matukio yaliyomo katika kazi za Shafi Adam Shafi. Matukio hayo yanaanza na tukio linalopatikana katika kazi ya *Kuli* ikiwa ni hatua ya kwanza ya mapambano kwa kuundwa vyama vya wafanyakazi vilivyotayarisha mgomo uliofanyika 1948 Zanzibar. Tukio la pili ni la katika *Vuta N'kuvute* ambalo linaonesha kupea kwa harakati za ukombozi wa Zanzibar wa kupambana na Waingereza. la tatu ni *Kasri ya Mwinyi Fuad*, ni kazi inayoonesha mapambano ya baada ya kuondoka Waingereza na Zanzibar kupata uhuru chini ya himaya ya Sultani. Kazi hii ndio iliyoonesha tukio la mapinduzi ya Zanzibar yaliyofanyika 1964. Mwisho ni tukio la katika *Haini*, kazi hii inaonesha mazingira ya baada ya mapinduzi na hasa baada ya kuuwawa kwa Mheshimiwa Abeid Amani Karume aliyekuwa raisi wa kwanza wa Zanzibar.

Mchango mwingine ni kuibua sababu za Shafi Adam Shafi kutumia mtindo wa kusimulia matukio ya kihistoria. Suala ambalo lilisababishwa na mazingira ya mwandishi kama vile hamu ya kutaka kusimulia watu ukweli wa matukio, uzoefu mdogo katika utungaji wa kazi za fasihi ikiwa pamoja na kutaka kuwa na mtindo wa kipekee katika utunzi wa kazi za fasihi ya Kiswahili ili kukwepa mtindo wa kipelelezi na wa kimapenzi.

Mchango wa tano ni kuibua dhamira zilizofichama katika kazi za Shafi Adam Shafi. Jamii kubwa inaziangalia kazi hizi kwa mtazamo wa ukombozi wa kisiasa moja kwa moja katika mtazamo chanya. Bali, kazi hizi zimekuwa zikionesha upungufu wa kila hatua ya ukombozi wa Zanzibar. Utafiti umegundua kuwa, kwa hatua ya kwanza, Zanzibar ilishindwa kupata uhuru wake kutokana na usaliti wa vibaraka wa wakoloni wa Kiingereza, kama alivyokuwa Mzee Tindo katika *Kuli*. Pili, harakati za ukombozi wa Zanzibar ni harakati zilizoendeshwa nje ya Zanzibar na kuja kutekelezwa tu Zanzibar. Hali hii inaonekana kupitia harakati za mhusika Denge katika kazi ya *Vuta N'kuvute*. Na kuuwawa kwa Kigogo katika *Haini* kunatokana na jamii kubwa ya Wazanzibar kutoridhika na uongozi wake, ikiwa ni pamaoja na wasomi kutoshirikishwa katika uongozi.

Mchango wa sita ni kuwa utafiti ulibaini kuwa Shafi Adam Shafi ni mwanaharakati katika ukombozi wa Zanzibar. Tawasifu ya harakati kaamua kuitoa kupitia kazi hizi kwa kubebesha baadhi ya mambo hayo kwa wahusika wake wakuu. Hapa yanakusudiwa mambo kama vile, baadhi ya majukumu na sifa za Denge katika *Vuta N'kuvute*, baadhi ya masaibu yaliyompata Hamza katika *Haini*, na kushuhudia mwenyewe mgomo wa makuli wa 1948 ulioelezwa katika *Kuli*. Hivyo, kazi hizi zinadhihirisha ubobevu wa Shafi Adam Shafi kwa siasa ya Zanzibar.

## 5.5 Maoni ya Utafiti kwa Jumla

Kutokana na mchakato wa kazi hii utafiti umeweza kubaini maoni yafutayo: Mosi, jamii wazisome kwa wingi kazi hizi za Shafi Adam Shafi ili kujua uhalisi na historia ya Zanzibar. Utafiti umebaini kuwa imani ya wanajamii, hasa waliosoma kazi za Shafi Adam Shafi, ni kwamba kama watu watazisoma kazi hizi watapata fursa nzuri ya kujua hali na historia halisi ya Zanzibar kiutamaduni, kisiasa na hata kiuchumi. Kwa upande wa utamaduni, limetolewa mfano wa suala la ndoa za kubaguana kikabila, suala ambalo hadi leo linapatikana katika mazingira ya Zanzibar. Pia, suala hili halikuwa katika makabila ya Wahindi au Warabu peke yao, hata Waswahili wa kutoka sehemu moja kwenda nyingine ilikuwa ni ngumu kuozeshana. Mfano watu wa kisiwa cha Tumbatu walikuwa hawapendi kuwaozesha watoto wao wa kike sehemu nyingine ambayo ni nje ya kisiwa hiki.

Utafiti ulibaini kuwa jamii bado ina hamu ya kazi za mwandishi huyu. Suala hili lilijitokeza kutokana watu wengi kati ya waliotafitiwa, kuonesha kuhitaji mwandishi aendelee kuandika kazi nyingine za kifasihi. Suala ambalo limejenga hamu ya kazi hizi kwa wasomaji wa kazi zake ni hatua anazopiga mwandishi katika maendeleo ya kifasihi siku hadi siku. Maelezo hayo yanabainika kutokana na ufafanuzi wa mfatano wa ubora wa kisanii katika kazi zake. Kwa mfano, kazi ya *Kuli* ina ubora wa kisanaa kuliko *Kasiri ya Mwinyi Fuadi*, kazi ya *Vuta N'kuvute* ina ubora wa kisanaa kuliko *Kuli*, *Haini* ina ubora wa kisanaa kuliko *Vuta N'kuvute* na *Mbali na Nyumbani* ina ubora wa kisanaa kuliko hata *Haini*. Hivyo, matumaini ya wasomaji wa kazi hizi ni kuwa kazi itakayofuatiya itakuwa ni bora kuliko *Mbali na Nyumbani*.

Kwa mujibu wa utafiti huu, bado jamii inahitaji wahakiki na wachambuzi kuchambua zaidi na kuzichambua kitaaluma zaidi kuliko kuchambua kibiashara. Utafiti

unaonyesha kuwa bado kazi za mwandishi huyu hazijachambuliwa vya kutosha na uchambuzi uliokuwepo upo wa kijuu juu zaidi. Uchambuzi uliochambuliwa kazi hizi ni mwepesi na upo zaidi kuwasaidia wanafunzi wanaosoma kazi hizi kama sehemu ya mtaala wao kuweza kufanikiwa katika mitihani yao. Kinachohitajika ni kupata uchambuzi utakaosaidia jamii kupata dhamira halisi ya kazi hizi.

Baada ya maoni hayo, tasnifu hiii inapendekeza juu ya walimu wa somo la historia mashuleni kuzitumia kazi za Shafi Adam Shafi kama ni rejea zao. Historia halisi ya Zanzibar ilifichwa na haikuwa katika maandishi kwa uhalisi wake. Hali hii imesababisha wanafunzi kupotoshwa juu ya historia ya Zanzibar. Kazi hizi zikitumika kama ni rejea huweza kujenga muongozo mzuri wa kujua ukweli juu ya historia ya Zanzibar.

Utafiti unashauri juu ya viongozi na taasisi zinazohusika na lugha na utamaduni kwa jumla kuwaenzi waandishi wa kazi za fasihi. Waandishi pamoja na kufanya kazi kubwa ya kutunza utamaduni, historia na amali nyingine za kijamii, lakini bado ni watu wasiothaminiwa. Hali hii imejitokeza kwa kiasi kikubwa hasa katika jamii ya Zanzibar. Wasanii wengi maarufu waliokufa na walio hai ni wenye kudharauliwa na hakuna juhudi yoyote ya kuwaenzi mashuja hao. Mfano halisi kwa waliokufa ni Mohamed Said Abdallah, Mohamed Suleiman Mohamed na Amour Abeid. Wale walio hai kama vile Shafi Adam Shafi, na Said Ahmed Mohamed.

## 5.6 Mapendekezo juu ya Tafiti Zijazo

Kama zipo tafiti zilizoangalia Upande wa Pili wa kazi za fasihi, na hii itakuwa miongoni mwa kazi hizo chache ambazo zimeangalia jambo hili. Kutokana na upya na

umuhimu wa dhana hii, kuna haja ya kuangalia Upande wa Pili wa kazi za kifasihi katika mashairi.

Kuna haja ya kutafiti, kwa kuchunguza uteuzi wa wahusika katika kazi za Shafi Adam Shafi na uhalisi wake katika historia ya jamii ya Zanzibar.

Kuna haja ya kutafiti matumizi ya mbinu ya Fasihi simulizi ndani ya Fasihi andishi katika kazi za Shafi Adam Shafi na dhima zake katika kutoa uhalisi wa matukio ya jamii.

Pia, kuna haja ya kutafiti kwa nini waandishi wa fasihi wakiwemo wa Zanzibar wanatengwa na taasisi zinazohusika na masuali ya fasihi au lugha na utamaduni, pamoja na serikali kwa jumla. Hali hii inathibitika kupitia maelezo ya Shafi Adam Shafi mwenyewe:

> Kuna watu hawapendi kutuona kule Zanzibar, na hata nilipokuwa natoa mchango wangu, mfano nilipokuwa mwenyekiti wa UWAVITA nilipeleka mswada wa kujenga maktaba, lakini hawakujali na hawakuthamini kabisa suali hilo.[10]

Maelezo haya yanaonesha kuwepo kwa pengo lililokuwepo baina ya waandishi wa fasihi wa Zanzibar na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

---

[10] Mahojiano ya Shafi A. Shafi na Mtafiti yaliyofanyika nyumbani kwake Bunju Dar es Salaam, tarehe 25/2/2015

## MAREJEO


Al-Ismaily, I. N. I. (1999), *ZANZIBAR Kinyang'anyiro na Utumwa*, Ruwi, Sultanate of Oman.

BAKIZA (2010), *Kamusi la Kiswahili Fasaha*, Oxford University Press, Nairobi.

Bakhressa, S. K. (1992), Kamusi ya Maana na Matumizi, Oxford University Press, Nairob.

Burton, S. H. (1962), *The Criticism of Poetry*, Green and Co. Ltd, Hong Kong.

Enon, J. (1998), *Educational Research, Statistic and Measurement*, Department of Distance Education, Kampala.

Haji, H. G. (2006), *Kamusi ya Kitumbatu*, Express Printing Services, Zanzibar.

Haji, H. G. (1994), *Kimbunga*, TUKI, Dar es Salaam.

Kezilahabi, (1983), "Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi" *Fasihi*; *Makala ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III*, TUKI, Dar es Salaam.

Khatibu, M. S. (1983), "Kuli", *MULIKA*, Na. 15, Pp. TUKI, Dar es Salaam.

Kiango, S. D. (1987), "Tone la Mwisho" *MULIKA*, Na. 19, pp. TUKI,Dar es Salaam.

King'ei, G. K. (1987), "Usanifu wa Lugha katika Uandishi wa Ebrahim Hussein" *MULIKA*, Na. 19, pp. TUKI, Dar es Salaam.

Kitula, K. na Ahmed, N. (2008), "*Kamusi ya Methali; Toleo jipya*". East Africa Educational Publisher, Nairobi.

Kothari, C. R. (2004), "*Research Methodology; Methods and Techniques* (2nd ed)", New Age International (P) Ltd, New Delh.

Madumulla, J. S. (2009), "*Riwaya ya Kiswahili"*, Mture Educational Publishers Ltd, Dar es Salaam.

Maneno, S. K. (h.t), *Uchambuzi wa Mashetani na Masaibu ya Ndugu Jero*, The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Mapuri, O. R. (1996), *Zanzibar The 1964 Revolution: Achievements and Prospects*, TEMA Publishers Company Ltd, Dar es Salaam.

Margaret, K. (1997), "Uchambuzi wa Visiki" *Makala ya Kiswahili ya Kitaifa*, Kenya Kiswahili Association, Nairobi.

Masebo, J. A. na Nyangwine, (2010), *Kiswahili, Kidato cha 3 na 4*, Nyambari Nyangwine Publishers, Dar es Salaam.

Mgeni, A. (1983), "The Element of Mystery in the Novel of Mohamed Said Abdalla" *Kiswahili* Vol. 50, no. 2, pp, TUKI, Dar es Salaam

Mlacha, S. A. K. na Madumulla, J. S. (1991), *Riwaya ya Kiswahili*, Dar es Salamm University Press, Dar es Salaam.

Mohamed, M. (2003), *Malenga wa Mrima Nimerudi*, Oxford University Press, Dar es Salaam.

Mohamed, S. A. (2010), Nyuso za Mwanamke, Longhorn Publishers Ltd, Nairobi.

Mulokozi, M. M. na Kahigi, K. K. (1979), *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Mussa, F. K. (2007), "Mchango wa Suala la Ukombozi katika Riwaya za Shafi A. Shafi", Tasnifu katika Shahada ya Kwanza ya Elimu na Sanaa, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Nguro, A. (2005), *Fasihi Simulizi; kwa Shule za Sekondari*, Phoenix Publishers Ltd, Nairobi.

Semzaba, (1997), OSW 208, *Tamthilia ya Kiswahili*, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.

Senkoro, (2011), *Fasihi*, KAUTTU Limited, Dar es Salaam.

Shafi, A. S. (2013), *Mbali na Nyumbani*,Longhorn Publishers (T) Ltd, Dar es Salaam.

-------------- (2003), *Haini*, Longhorn Publishers (K) Ltd, Nairobi.

--------------- (1999), *Vuta N'kuvute*, Mkuki na Nyota, Dar es Salaam.

--------------- (1979), *Kuli*, Longhorn Publishers (T) Ltd, Dar es Salaam.

---------------- (1978), Kasri ya Mwinyi Fuad, Vide˜Muwa Publishers Ltd, Nairobi.

Shella, A. M. (2012), "Athari ya Uhalisia Mazingaombwe kwa Msomaji katika Kuzielewa Kazi za Kifasihi za Said Ahmed Mohamed", Tasnifu katika Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu Cha Dodoma.

Simiyu, W. F. (2011), *Kitovu cha Fasihi simulizi*, Serengeti Bookshop, Mwanza.

Songoyi, E. M. and Masele, E. J. (2013), *Prose and Poetry; A teaching manual*, Heritage Tanzania Educational Limited, Dodoma.

Wamitila, K. W. (2004), "Fantansy and Realism in the Modern Kiswahili Novel: A Critical Look at "Babu Alipofufuka", *Kiswahili* Vol. 67, TUKI, Dar es Salaam.

--------------------- (2002), *Uhakiki wa Fasihi; misingi na vipengele vyake*, Phoenex Publishers Ltd, Nairobi.

------------------- (2003), *Kamusi ya Fasihi; Istilahi na Nadharia*, Focus Publications Ltd, Nairobi.

## VIAMBATANISHO

### A: Picha za Utafiti



Mwandishi Shafi Adam Shafi (kulia) akiwa na Mtafiti wakati wa mahojiano, yaliyofanyika nyumbani kwake Bunju, Dar es Salaam, tarehe 25/2/2015.



Mwandishi Shafi Adam Shafi akielezea juu ya historia yake pamoja na kazi zake za kifasihi wakati wa mahojiano na Mtafiti huko nyumbani kwake Bunju, Dar es Salaam, tarehe 25/2/2015.

**B: Zana Zilizotumika Kukusanyia Data**

## B. 1 MUONGOZO WA USAILI KWA WATAALAM WA FASIHI

**Maswali:**

1. Nini maana ya maana/dhamira katika uwanja wa fasihi?
2. Je maana/dhamira katika fasihi huweza kufichama katika maana/dhamira nyingine? Kwa vipi?
3. Je, ni vipengele gani vya kazi ya fasihi vinavyoweza kutoa maana au dhamira zilizofichama?
4. Ni kwa njia zipi tunaweza kuziibua maana au dhamira zilizofichama katika kazi ya kifasihi?
5. Ni kazi zipi za Shafi A. Shafi ambazo umewahi kuzisoma, kuzihakiki au kuzitafiti?
6. Baadhi ya wahakiki wa kazi hizi wanadai kuwa lugha iliyotumika katika kazi hizi ni nyepesi. Una maoni gani juu ya suali hili?
7. Kuna vipengelele vyovyote katika kazi hizi ambavyo vinaweza kutoa maana au dhamira zilizofichama katika kazi za Shafi A. Shafi?
   a) Vitaje.
   b) Ni maana/dhamira zipi zinazopatikana katika vipengele hivyo?
8. Kwa maoni yako, kuna miktadha (mazingira) gani yaliyomsukuma Shafi A. Shafi kutumia mtindo na lugha ya aina hiyo?
9. Unadhani Shafi A. Shafi alikuwa na lengo gani la kutumia mtindo na lugha aliyotumia katika kazi zake au kiwango chake cha uwandishi?
10. Una maoni gani kuhusu athari ya mtindo na lugha iliyotumika kwa wasomaji wa kazi hizi?
11. Maana/dhamira zilizofichama huweza kujenga upande wa pili wa kazi ya fasihi kimaana? Hali hiyo tutaiitaje kifasihi?
12. Ni kazi zipi zingefaa zaidi kutumika katika kutunza historia ya Zanzibar?
13. Toa maoni yako kwa ujumla juu ya kazi za kifasihi za Shafi A. Shaf

**B.2 MUONGOZO WA HOJAJI KWA WANAFUNZI WA FASIHI WA SEKONDARI NA VYUO**

Tafadhali jaza taarifa zako kwa usahihi, umakini na kwa ridhaa yako

1. Wewe ni mwanafunzi wa kiwango gani? Kidato cha Tano ☐
   Kidato cha sita ☐ Stashahada ☐ Shahada ya Kwanza ☐
2. Je, unasoma fasihi katika kiwango hiki? Ndiyo………… Hapana ……….
3. a) Umeshawahi kusoma riwaya za Shafi A. Shafi? Ndio …. Hapana ………
   b) Kama ndio, ngapi? Moja ……… Mbili …………. Tatu …………
   Nne ………. Zaidi ya nne …………….
   c) Taja kazi za Shafi Adam Shafi ulizowahi kusoma.
   i) …………………………. iii) ………………… iii)
   iv) ……………………………. v) …………………………….
4. a) Lugha iliyotumika katika kazi uliyosoma ni i) Nyepesi ………… ii) Ngumu ………...
   b) Ni vigezo gani unaweza kusema lugha ni nyepesi au lugha ni ngumu ……………………………..……………………………………………
   ………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………
5. Unadhani kwanini mwandishi katumia lugha hiyo (Nyepesi/Ngumu) ..…..........
   ………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………
6. Lugha hiyo (Nyepesi/Ngumu) ina athari gani kwa wasomaji wa kazi hizo? ………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………
7. Unafahamu nini juu ya maana/dhamira zilizofichika katika kazi ya kifasihi………
   ………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………

8. Ni mtindo au lugha ipi iliyokuvutia katika kazi za Shafi A. Shafi (Toa mfano wa mtindo au lugha na kitabu unamo/inamopatikana) ……………………………
……………………………………………………………………………………
9. a) Je, kuna vipengele vyovyote vya kifani katika kazi za Shafi A. Shafi, ambavyo vinaweza kutoa maana/dhamira zaidi ya moja? Ndio…………. Hapana ………
b) Kama ndio toa mfano ………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
c) Kama hapana, unadhani kwanini …………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
10. Toa maoni yako juu ya vipengele vya mtindo na lugha pamoja na athari kwa wasomaji wa kazi za Shafi A. Shafi ……………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………T
oa maana zaidi ya moja juu ya vipengele vifuatavyo kama vilivyotumika katika kazi (riwaya) za Shafi A. Shafi.

i. “Usilie usilie,
ukaniliza na mie,
machozi yako yaweke,
nikifa unililie” (*Kuli* uk. 4)

a) ……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
b) ……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………

ii. “Hakuna msiba usiokubali kushikwa na usingizi ukalala”. ( *Vuta n’Kuvute* uk.229)

a) ……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
b) ……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………

“Hakuna shida inayozaa shida, shida maisha huzaa kheri”. (*Haini* uk. 60)

a) …………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………

b) …………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………

11. Andika maneno/vifungu vya maneno vingine kama hivyo hapo juu vyenye maana zaidi ya moja vinavyopatikana katika vitabu vya Kuli, Haini na Vuta n’Kuvute.

i. …………………………………………………………………………

ii. …………………………………………………………………………

iii. …………………………………………………………………………

iv. …………………………………………………………………………

v. …………………………………………………………………………

12. Maana/dhamira zilizofichama huweza kujenga upande wa pili wa kazi ya fasihi kimaana? ……………………………………………………………………
Hali hii (yaani upande wa pili wa kazi ya fasihi ) tutaiitaje kifasihi? …………………………………………………………………………
………………………… ……………………………

13. Ni kazi zipi za kifasihi za Shafi Adam Shafi zingefaa zaidi kutumika katika kutunza historia ya Zanzibar?

i. ……………………………………………

ii. …………………………………………....

iii. ……………………………………………

iv. ……………………………………………

14. Toa maoni yako kwa ujumla juu ya kazi za kifasihi za Shafi A. Shafi.

…………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………
………

## C: MAELEZO YA MAFUPI YA MTAFITI NA UTAFITI:

Jina langu ni GORA AKIDA HAJI, ninafanya utafiti kutoka Chuo Kikuu Cha Dodoma, kilichopo Tanzania. Ni utafiti unaojitegemea na hauna uhusiano wowote na masuala ya kisiasa na serikali.

Lengo la utafiti huu ni kuangalia dhamira zipi zinazojitokeza katika mtindo na lugha ya kitamathali iliyotumika katika kazi za Shafi Adam Shafi; Athari ya mtindo na lugha iliyotumika katika kazi hizi kwa wasomaji wake pamoja na kujua mazingira yaliyomsukuma mwandishi huyu kutumia mtindo na lugha iliyotumika katika kazi zake.

Taarifa utakazotoa ni siri ya mtafiti, na huhitajiki kutaja jina, nambari ya simu wala taarifa yoyote itakayokutambulisha wewe kwa mtafiti. Ushiriki wako ni wa kujitolea; na hakuna hatua yoyote itakayochukuliwa kwa kutoshiriki kwako katika utafiti huu.

Tunakushauri kushiriki kikamilifu ili utowe mchango wako wa kitaaluma katika uwanja wa fasihi.

Tunatanguliza shukrani zetu kwako kwa ushirikiano wako.



GORA AKIDA HAJI

CHUO KIKUU CHA DODOMA

Simu: 0773 127095 /0653 385632

Barua pepe

hajigora82@gmail.com